# Nipashe

Ijumaa Septemba 6, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580016

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Sinema ya mwanamke aliyeibiwa fedha na waliomuuzia gari

UKURASA 3




UKURASA 13

## YALIYOMO


**UKURASA WA 4**

**UPINZANI WAONYESHA HOFU UCHAGUZI MITAA**

JOTO la uchaguzi wa serikali za mitaa limeendelea kupanda kwa kasi, huku wabunge wa upinzani wakionyesha hofu yao kuhusu kanuni za uchaguzi huo...

**UKURASA WA 7**

**DC ANASA MITAMBO, LITA 4,800 ZA GONGO**

OPERESHENI ya siri inayoongozwa na Mkuu wa Wilaya, ya kuwabaini wafanyabiashara sugu wanaotengeneza na kusambaza pombe haramu ya gongo, imenasa lita 4,800 na mitambo sita katika kiwanda ...

**UKURASA WA 26**

**WAANDISHI RUKSA KURIPOTI KESI UGAIDI**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imeruhusu waandishi wa habari kuripoti kesi ya ugaidi inayowakabili viongozi wa Uamsho na Mihadhara ya Kiislamu...




Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Adelardus Kilangi

# Ukikiri makosa adhabu kiduchu

Ni kuhusu mabadiliko ya sheria mbalimbali, kibano zaidi 'wazungu wa unga', mawakili wa serikali...*Uk. 2*



Waziri wa Mambo ya Nje, Prof. Palamagamba Kabudi



Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa



Rais wa Nigeria, Muhamad Buhari



Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson

# Kilio chatanda dunia nzima kulaani ubaguzi

UN, Uingereza zatoa neno, Nigeria yaondoa raia wake Afrika Kusini...*Endelea ukurasa wa 2*

## Safari za ATCL 'Sauzi' zasimama

UKURASA 3


TAIFA STARS vs BURUNDI

SEPTEMBA 8, 2019 • UWANJA WA TAIFA




215393302

HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.



Rais John Magufuli akimjulia hali Mkurugenzi Mkuu mstaafu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Apson Mwang'onda anayepatiwa matibabu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Wanaokiri makosa kupunguziwa adhabu

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imewasilisha bungeni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2019 kwa lengo la kurekebisha sheria 11.

Sheria zinazopendekezwa kufumuliwa ni pamoja na Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256 kwa lengo la kuipa mahakama uwezo wa kutaifisha mali tofauti na iliyopatikana kwa uhalifu endapo itagundulika upatikanaji wake si halali, kufichwa au kutoroshwa nje ya nchi.

Katika marekebisho hayo, pia inapendekezwa uwapo wa kifungu kipya cha 14B kitakachoipa mahakama uwezo wa kuzuia uhamisho wowote wa mali ambao umefanyika kwa lengo la kukwepesha mali kutaifishwa.

Akiwasilisha bungeni jijini Dodoma jana muswada huo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelardus Kilangi, alisema marekebisho hayo yanalenga wahalifu kutonufaika na mali zozote zitokanazo na makosa ya rushwa, usafirishaji dawa za kulevya, utakatishaji fedha na makosa mengine yanayohusiana.

Alisema kabla ya maombi ya kutaifisha hayajafanywa au ndani ya miaka mitano kuanzia siku ya mwisho ya tukio kutokea, mali hiyo itahesabiwa ni zao la uhalifu.

Prof. Kilangi alisema mapendekezo katika kifungu cha 38 yanalenga kumwezesha Mkurugenzi wa Mashtaka kuwasilisha mahakamani maombi ya upande mmoja ya kuzuia mali pale ambapo mhusika anachunguzwa au hawezi kufika mahakamani au alishahukumiwa kwa kosa linalohusiana na mali iliyotaifishwa.

"Kifungu cha 56 kinapendekezwa kufutwa kwa lengo la kuondoa mahitaji yasiyo ya lazima dhidi ya serikali ya kulipa gharama za madhara yanayotokana na amri ya zuio iliyowekwa," Prof. Kilangi alisema.

**KIBANO MAWAKILI**

Katika muswada huo, serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 ili kuwazuia maofisa sheria au mawakili wa serikali na wanasheria walioko kwenye utumishi wa umma, kufanya kazi za uwakili wa kujitegemea isipokuwa kushuhudia viapo na uhakiki wa nyaraka.

"Mawakili wa serikali wanaweza tu kufanyakazi za uwakili wa kujitegemea kwa kibali maalum cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa sababu maalum.

"Wanasheria wanaokusudiwa ni wanasheria wote katika utumishi wa umma ambao wanaongozwa na Kanuni za Maadili ya Wanasheria katika Utumishi wa Umma," alisema.

Katika muswada huo, serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, Sura ya 108, kwa lengo la kupanua wigo wa mfumo wa usajili wa vizazi na vifo vikijumuisha vifo vinavyotokea nje ya nchi.

Prof. Kilangi alisema marekebisho hayo pia yanalenga kuwatambua watendaji wa kata na vijiji kama wasajili wasaidizi baada ya kukasimiwa mamlaka hayo na Msajili Mkuu.

Prof. Kilangi pia alisema serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Urejeshaji Wahalifu, Sura ya 368, kwa lengo la kuboresha utaratibu wa kisheria wa ushirikiano wa kimataifa katika kusaidiana kurejesha watuhumiwa katika kesi za jinai.

Alisema muswada huo pia unalenga kufanya marekebisho katika Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11, kwa lengo la kuongeza kiwango cha thamani ya kifedha katika mashauri ya madai yanayosikilizwa katika mahakama hizo kutoka Sh. milioni 50 cha sasa hadi Sh. milioni 100.

Kilangi pia alisema muswada huo unalenga kufanya marekebisho katika Sheria ya Chama cha Msalaba Mwekundu Tanganyika, Sura ya 66, ili itumike pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupanua wigo wa majukumu ya chama hicho kwa mujibu wa viwango vya kimataifa.

MAONI KAMATI YA BUNGE

Akiwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu muswada huo, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mohamed Mchengerwa, alisema wamebaini serikali ina nia njema ya kuweka zuio la mawakili na maofisa wa sheria katika utumishi wa umma kujihusisha na huduma za uwakili wa kujitegemea, ikiwa ni pamoja na kuondoa mgongano wa maslahi binafsi kwa mashauri ambayo yanaihusu serikali.

Mchengerwa pia alisema kamati yake inashauri Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka ishirikiane kwa ukaribu na Ofisi za Takukuru katika ngazi za wilaya na mikoa yote nchini ili kupunguza mlundikano wa majalada kwa kurahisisha utoaji haki jinai kwa wakati.

**MAONI YA UPINZANI**

Akiwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu muswada huo, Msemaji Mkuu wa kambi hiyo katika Wizara ya Katiba na Sheria, Lathifah Chande, alisema kuzuia mawakili wa serikali kupewa hati au kibali cha kufanya shughuli za uwakili nje ya mfumo wa serikali kutawaondolea motisha ya kufanya kazi na kuwafanya wakabiliwe na ugumu wa maisha.

Alisema kambi hiyo inaamini mawakili wana haki ya kufanya shughuli binafsi za kiwakili baada ya muda wa kazi kama ambavyo waajiriwa wengine wa serikali walivyoruhusiwa binafsi zinazohusiana na taaluma zao baada ya muda wa kazi.

Alisema kambi hiyo pia inaona kitendo cha Takukuru kutokuwa na mamlaka ya kupeleka mahakamani mashtaka ya rushwa kubwa, kinatoa picha kwamba taasisi hiyo ya kiuchunguzi haiaminiki katika utendaji wake na ndiyo maana inakuwa taasisi ya kupewa maelekezo ya nini cha kufanyika na kwa wakati gani.

"Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri serikali, kama kweli inataka kupambana na rushwa kwa vitendo, basi ilete muswada wa sheria utakaoifanya Takukuru kuwa taasisi huru," alisema.

Chande pia alisema kambi hiyo inaona marekebisho yanayopendekezwa na serikali katika Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu Sura ya 256, yana nia ovu ya kuwalenga baadhi ya watu hususan wenye mtazamo tofauti na serikali ili kuwababmbika kesi za uhujumu uchumi na kuwafilisi kwa kutaifisha mali zao hata kabla ya kesi hizo kutolewa uamuzi na mahakama.

# Kilio chatanda kulaani ubaguzi

**Na Gwamaka Alipipi**

VITENDO vya ubaguzi vinavyofanywa na raia wa Afrika Kusini dhidi ya wageni wanaoishi nchini humo, vimelaaniwa na viongozi mbalimbali duniani huku wengine wakichukua hatua kadhaa.

Wakati dunia ikilaani vitendo hivyo, serikali ya Tanzania kupitia Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, imesema hadi sasa hakuna taarifa kuhusu Mtanzania aliyeuawa au kuharibiwa mali zake.

Wakizungumza kwenye mitandao ya kijamii jana na juzi, viongozi hao walieleza kuchukizwa na matukio ya vurugu yanayofanywa na wazawa wa Afrika Kusini dhidi ya wageni wanaofanya kazi, biashara na kuishi nchini humo.

Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, kupitia akaunti yake ya Twitter alisema: "Hatuwezi kukunja mikono yetu na kuacha kile kinachotokea Afrika Kusini. Ninashauri Rais wa Afrika Kusini (Cyril Ramaphosa) awajibike katika kudhibiti matukio hayo. Mataifa ya Ulaya yako tayari kujiondoa katika uwekezaji nchini humo".

Naye Waziri wa Mambo ya Nje wa Nigeria, Geoffrey Onyeama, alisema kutokana na vurugu zinazoendelea Afrika Kusini dhidi ya wageni, Shirika la Ndege la Air Peace limejitolea kuwasafirisha bure kuwapeleka makwao wale wote watakaotaka ili kujiepusha na kadhia hiyo.

Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari, kwenye mtando wa Twitter alisema: "Ninatuma salamu zangu kwa Rais Ramaphosa kumweleza huzuni tuliyo nayo kuhusu usalama wa maisha ya Wanaigeria na mali zao Afrika Kusini. Serikali ya Afrika Kusini ihakikishe inafanya liwezekanalo kwa kuchukua hatua kuhusu tukio hili."

RAMAPHOSA AFUNGUKA

Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa akizungumza jana kupitia televisheni ya taifa, alilaani vurugu zinazofanywa na raia wa taifa hilo dhidi ya wageni wakiwamo wa kutoka Nigeria, Malawi na Lesotho.

Alisema serikali yake haitafumbia macho vitendo hivyo na kwamba kwa yeyote atakayekamatwa atafikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Ramaphosa alisema waafrika wote ni wamoja na wanapaswa kuishi kwa amani na upendo bila kubaguana.

"Tutaendelea kama nchi kuonyesha upendo na umoja kwa wenzetu wanaoishi hapa nchini. vitendo ya uvunjifu wa amani vinapaswa kukemewa na kila mtu," alisema Rais Ramaphosa.

Alisema taifa la Afrika Kusini limepitia katika kipindi kigumu cha kupata uhuru wake, hivyo ni wakati wa kujenga uchumi

INAENDELEA UK. 8

HABARI KITAIFA

## Serikali kuisapoti TMA mpya

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imesema ili kufikia malengo ya kuwa na uchumi wa kati, huduma za Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) zinahitajika zaidi kufika huko.

Akizungumza jana kwenye uzinduzi rasmi wa iliyokuwa Wakala wa Hali ya Hewa ambayo sasa imekuwa Mamlaka ya Hali ya Hewa, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alisema kuwa kwa kutambua mchango wa mamlaka hiyo katika kuchangia uchumi wa nchi, serikali imejipanga kuendelea kushirikiana nao ili kufikia malengo.

Kufuatia sheria mpya ya bunge iliyopitishwa, sheria namba mbili ya mwaka 2019, TMA sasa imekuwa mamlaka kamili na kupewa uwezo kisheria kusimamia na kutoa taarifa zote za hali ya hewa.

Kamwelwe alisema kuwa kwa kutambua umuhimu wa taarifa za hali ya hewa, serikali imenunua rada nyingine tatu na kufanya Tanzania kuwa na rada tano ambazo zitasaidia kupatikana kwa taarifa za hali ya hewa nchi nzima.

"Katika rada saba zinazotakiwa, tayari tuna rada mbili zilizofungwa kwenye mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza na sasa tumenunua rada nyingine ambazo zitafungwa kwenye mikoa ya Mtwara, Kigoma na Mbeya.

"Nawapongeza sana TMA chini ya usimamizi wa Mkurugenzi mama Kijazi (Dk. Agnes Kijazi) kwa hatua hii mliyofikia...Serikali itaendelea kushirikiana nanyi kuhakikisha malengo yote yanafikiwa," alisema Kamwelwe.

Aidha, alisema kwa kuunga mkono maamuzi ya Rais John Magufuli ya kuhamia Makao Makuu Dodoma, serikali tayari imetoa eneo jijini humo litakalo jengwa jengo la Makao Makuu ya TMA.

Injinia Kamwelwe mbali na kuzindua mamlaka hiyo pia aliiaga Bodi ya Ushauri ya Mamlaka hiyo iliyokuwa ikiongozwa na Mwenyekiti, Burhuan Nyenzi.

Dk. Kijazi, alisema katika kipindi ambacho mamlaka hiyo ilikuwa wakala, wamepata mafanikio makubwa ikiwa pamoja na kufikia usahihi wa utabiri wake kufikia asilimia 87 mpaka 96.

"Mafanikio mengine ambayo tumeyapata ni pamoja na kuona Shirika la Kimataifa la Hali ya Hewa (WMO) imetambua huduma zinazotolewa na TMA na kutoa cheti cha kimataifa kwa vituo vya Songea mkoani Ruvuma na Bukoba mkoani Kagera," alisema Dk. Kijazi.

Awali, akiaga wafanyakazi wa mamlaka hiyo, mwenyekiti wa bodi iliyomaliza muda wake, Burhuan Nyenzi, alisema licha ya changamoto walizokutana nazo, kwa kipindi chote cha bodi hiyo, TMA imekuwa ikifanya vizuri kiasi cha kuwa mfano kwa nchi nyingine za Afrika na duniani kwa ujumla.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni (kulia), akipokea zawadi iliyotolewa na Kiongozi Mkuu wa Kiroho wa Madhehebu ya Kihindu, Mtukufu Mahant Swami Maharaj (kushoto), kwa ajili ya Rais John Magufuli, alipokutana na kiongozi huyo, jijini Dar es Salaam jana. Kiongozi huyo wa kiroho yuko nchini kwa ziara ya kikazi. **PICHA: WMNN**

# Tukio la kutaka kutekwa gari mwanamke kama sinema

**Na Rahma Kisilwa**, TUDARCO

TUKIO la mwanamke kutaka kutekwa gari na fedha eneo la Sinza Mori na madalali waliokuwa wanamuuzia gari hilo Jumanne iliyopita, liligeuka kama sinema baada ya watu hao kujaribu kuliiba wakati mnunuzi huyo akiingia benki kuchukua fedha.

Madalali hao na mwanamke huyo waliongozana wakiwa ndani ya gari aina ya IST toleo jipya hadi kwenye benki eneo hilo, jijini Dar es Saalam.

Sinema hiyo ilianza wakati mnunuzi huyo alipoteremka kutoka kwenye gari hilo na kuingia benki, huku akiwaacha madalali hao ndani ya gari hilo na fedha nyingine alizokuwa nazo.

Akisimulia tukio hilo shuhuda Abdallah Suleiman, alisema kabla ya kuingia benki, mwanamke huyo alishtuka kusikia gari aliyokuwa amepanda ikiondolewa kwa kasi na ndipo akatoka na kupiga kelele.

Alidai mwanamke huyo alikuwa na fedha taslimu Sh. milioni 10 aliyoicha ndani ya gari ambayo ilikuwa ni sehemu ya malipo ambayo fedha nyingine ya kuongeza ndiyo aliyokwenda kuchukua benki.

"Benki iko karibu na kituo cha mafuta, baada ya kelele za mwanamke huyo huku akielekea kituo cha mafuta cha Big Bon wakati gari yake ikikaribia kutoka eneo hilo, ilikuja gari aina ya Nissan ikalizuia kwa mbele kwa kuligonga na aliyekuwa akiliendesha alitoka na kukimbia na kuwaacha wenzake waliokuwa viti vya nyuma," alisema.

Shuhuda huyo alisema baada ya purukushani hiyo watu walijitokeza na kuanza kuwakagua vijana hao ambao inadaiwa walikuwa wamekwisha gawana fedha hizo kila mmoja Sh. milioni tatu.

"Baada ya kuvamia na kufungua mlango ndipo walipowakuta vijana wengine wawili kwenye gari, mwanamke aliwahi haraka kwenye gari kudai fedha zake," alisema na kuongeza:

"Ndani ya bahasha moja yenye nembo ya NMB kulikuwa na Sh. milioni mbili na pia kulikuwa na vitita viwili vya Sh. milioni tatu kila kimoja ambavyo tayari vijana wale walikuwa wamegawana."

Alisema askari wanaolinda benki ya NMB ndiyo waliosaidia kuwakamata watu hao, baada ya kelele za mwanamke huyo za kuomba msaada.

Video iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii iliwaonyesha vijana wawili wakiwa chini wamedhibitiwa nyuma ya gari na baadaye kuchukuliwa na polisi.

Nipashe lilimtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, Musa Taibu, kuzungumzia tukio hilo ambaye alisema yuko mkoani Shinyanga na kuagiza atafutwe msaidizi wake ambaye naye alipotafutwa alisema yupo masomoni na kuelekeza atafutwe Mkuu wa Upelelezi wa mkoa huo (RCO).

RCO Malulu alipotafutwa alisema hawezi kuzungumzia tukio hilo kwa kuwa msemaji ni Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, ambaye hata hivyo, hakupatikana kupitia simu yake ya mkononi.

# ATCL yasitisha safari zake za Afrika Kusini

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI ya Tanzania imetangaza kusitisha safari za ndege za Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) kwenda Afrika Kusini kutokana na vurugu zinazoendelea nchini humo.

Akitangaza hatua hiyo, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, akisema jana kuwa wamesitisha kwa muda safari zote za Afrika Kusini mpaka watakapojiridhisha hali ya usalama imetulia nchini humo.

Alisema ratiba ya shirika hilo inaonyesha ilikuwa ingesafiri leo saa tisa kuelekea Afrika Kusini, lakini sasa safari hiyo imefutwa ingawa abiria waliokata tiketi za shirika hilo watasafirishwa kupitia kampuni nyicngine ya ndege.

"Hatuwezi kuendelea kupeleka watu katika eneo ambalo tunaona hakuko sawa, vurugu zimekuwa kubwa na kila mtu anaona kinachoendelea Afrika Kusini," alisema Kamwelwe.

Aidha, alisema kuwa serikali inafuatilia kwa karibu kile kinachoendelea Afrika Kusini na hali itakapokaa sawa watarudisha safari hizo.

Aidha, baada ya kurejea nchini ndege ya Tanzania aina ya Airbus iliyokuwa ikishikiliwa Afrika Kusini, safari za ndege hiyo kwa maeneo mengine itaendelea kama kawaida.

"Niwatoe hofu Watanzania, ndege yetu ipo kwenye hali nzuri na leo (jana) wataalamu walikuwa wakiikagua baada ya kukaa karibu wiki mbili bila kufanya kazi ilipokuwa kule Afrika Kusini, safari zake zitaendelea kama kawaida na mipango yetu ni kuhakikisha tunaruka nchi nzima," alisema.

Katika hatua nyingine Kamwelwe, aliwapongeza wanasheria na viongozi waliofanikisha kuirejesha ndege hiyo hapa nchini baada ya kushinda kesi iliyokuwa ikiendeshwa Afrika Kusini.

"Baada ya maamuzi ya Mahakama na ndege yetu kuachiliwa, wanasheria wetu wanaendelea kufuatilia kuhakikishia gharama za kesi ile zinalipwa...nitumie nafasi hii kuwapongeza wanasheria wetu na viongozi waliopambana kuona ndege yetu inarudi."

"Nimemwagiza Naibu Waziri wangu atoe taarifa hii bungeni na kuwahakikishia Watanzania ndege yetu ipo vizuri na itaendelea na ratiba yake kama kawaida," alisema.

Ndege hiyo ilishikiliwa Afrika Kusini tangu Agosti 23, mwaka huu kabla ya kuachiwa juzi na kurejea nchini.

# Upinzani waonyesha hofu uchaguzi mitaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JOTO la uchaguzi wa serikali za mitaa limeendelea kupanda kwa kasi, huku wabunge wa upinzani wakionyesha hofu yao kuhusu kanuni za uchaguzi huo.

Hata hivyo, serikali imewaondoa hofu na kusema uchaguzi utakuwa huru na haki kwa hiyo hakuna sababu ya kuhofia.

Wabunge hao walionyesha hofu hiyo jana bungeni wakati wa kipindi cha 'Maswali na Majibu' baada ya Mbunge wa Kibamba (Chadema), John Mnyika, kuhoji ni kwa nini serikali imeogopa kupeleka bungeni Sheria ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Kaika swali lake la nyongeza, Mnyika alisema sheria hiyo ingeondoa mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa na ingeweka daftari la kudumu kutumika na ingepeleka majukumu yote kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi(NEC) badala ya waziri.

"Wanasema kanuni zimeandaliwa kwa kushirikisha wadau. Tumekaa vikao vya vyama Aprili lakini Aprili hiyo hiyo Waziri akatoa kanuni hizo kwa siri zilizochapishwa na zimetolewa Agosti na hazijazingatia maoni ya wadau na tayari zimeanza kutumika vibaya," alisema.

Mnyika alisema wakuu wa mikoa, wilaya na maofisa tarafa wamepewa jukumu la kusimamia uchaguzi huo wakati ni makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Hivi kweli kutakuwa na uchaguzi huru na haki katika mazingira kama hayo?" alihoji.

Naye Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe, alisema inawezekana mambo ya uchaguzi yakaonekana ni mepesi lakini amani ya taifa itapotea au itaathiriwa na masuala ya uchaguzi.

"Kanuni zozote zinazotungwa kwenye nchi yetu hii leo, lazima kwa njia moja au nyingine ziridhiwe na Bunge. Sheria ndogo ndogo tunazotunga kabla hazijaanza kutumika kimsingi zinastahili kuletwa na kuridhiwa na bunge. Vikao vya wadau vinavyokaa ni maombi hata vikao vya wadau haviwezi kuwa mbadala wa Bunge," alisema.

Mbowe ambaye ni Mbunge wa Hai, alisema Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo Ndogo haijawahi kuona au kupitia, kuridhia au kuzikubali kanuni zilizotungwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

"Katika utamaduni huo kanuni zimeshaingizwa kazini, kamati ya sheria ndogo ndogo haikuzipitia kwa kisingizio kuwa wadau walizipitia wakati sio bunge, je jambo hili ni sahihi?" alihoji.

Akijibu swali la Mnyika, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tamisemi), Mwita Waitara, alisema uchaguzi huo unasimamiwa na waziri mwenye dhamana kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Aidha alisema kanuni hizo zimezingatia miongozo huku akidai kuwa si kila wanapoitwa kutoa maoni ni lazima kichukuliwe kila kitu bali watalaam hukaa na kuangalia Katiba, sheria na miongozo mbalimbali halafu inaamuliwa.

Akijibu swali la Mbowe, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Aderaldus Kilangi, alisema madai kuwa sheria ndogo ndogo ni lazima zinapotungwa kupelekwa bungeni kabla ya kuanza kutumika si sahihi.

"Sheria ndogo huwa zikishatayarishwa huwa zinapelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa serikali kwa ajili ya kufanyiwa uchambuzi (vetting) na baada ya hapo mwanasheria humrudishia Waziri mhusika na Waziri yule ana zitangaza," alisema.

Prof. Kilangi alisema baada ya hapo hupelekwa katika kikao kinachofuata cha bunge kwenye Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo Ndogo kwa ajili ya kuchambuliwa.

"Mtu anaweza kusema labda mchakato huo hautoi nafasi ya kuweza kuziangalia vizuri zile sheria ndogo, kimsingi sheria ndogo zote zinatungwa chini ya Sheria mama na ipo misingi ya kisheria inayoelekeza namna gani sheria ndogo zitungwe na moja wapo ni sheria hiyo isipingane na sheria mama," alisema.



Mafundi wakijiandaa kuzibua mfumo wa maji taka ulioziba katika eneo la Stesheni, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOHN BADI.**

# Magari 54 ya mtu mmoja kunadiwa Dar

**Na Joseph Mwendapole**

JINAMIZI la nyumba kuuzwa kutokana na wamiliki kushindwa kurejesha mikopo sasa limehamia kwa mtu mmoja anayemiliki magari 54 aina ya IST, ambayo yanauzwa kesho baada ya kushindwa kurejesha mkopo.

Mmiliki wa magari hayo anadaiwa kukopa benki ya ICB na kununua magari hayo kwa ajili ya kuyafanyia biashara, lakini muda ulipopita bila kukamilisha mkopo huo, benki hiyo iliamua kuyakamata na kuamuru yauzwe kufidia mkopo huo.

Benki hiyo ilitoa zabuni kwa kampuni ya udalali ya Yono Auction Mart kuendesha mnada wa kuuza magari hayo kesho Jumamosi, maeneo ya Bahari Beach jijini Dar es Salaam kuanzia asubuhi hadi jioni.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Yono, Scholastica Kevela, aliliambia gazeti hili jana kuwa wameweka masharti makali ya kuingia kwenye mnada huo ili kuwaepuka watu aina ya Dk. Shika, ambao huingia kwenye minada hiyo kwa ajili ya kuivuruga.

"Safari hii tumejipanga sawa sawa tumeweka utaratibu mzuri kuhakikisha kwamba hakutakuwa na watu wa aina ya Dk. Shika kwa sababu utapoingia kwenye mnada utatakiwa kuacha getini Sh. 2,000,000 tunaweka kama dhamana ukiharibu mnada hatutakurudishia na kama hutaharibu mnada unarudishiwa," alisema Scholastica.

Mkurugenzi huyo alisema tangu kutangazwa kwa mnada huo mamia ya watu wamekuwa wakifurika kwenye yadi ya Yono Bahari Beach kwa ajili ya kukagua magari hayo ambayo mmiliki wake alikuwa akiyatumia kibiashara kwa usafiri wa mitandanoni.

"Kuna usemi wa Kiswahili kwamba kukopa harusi kulipa matanga. Mtanzania mwenzetu alikopa IST zaidi ya 54, lakini ameshindwa kulipa mkopo, hivyo ICB ilitupa kazi ya kuzikamata na kuziuza ili kurejesha fedha benki, nawashauri Watanzania mkikopa msimamie vizuri fedha ili mrejeshe mikopo kuepuka adha kama anayopata mwenzetu," alisema.

"Magari haya yanatumia mafuta kidogo sana hivyo nawahamasisha hata wanawake wenzangu wachangamkie fursa hii ya kupata IST kwa bei nzuri kwa sababu kwa mujibu wa bei elekezi ukija huwezi kukosa kuondoka na gari," alisema.

Mbali na IST hizo, Mkurugenzi huyo alisema kwenye mnada huo watauza magari mengine ya aina mbalimbali ambayo yamekamatwa kutokana na makosa mbalimbali yakiwamo ya ukwepaji wa kodi.

Matukio ya kunadiwa mali zikiwamo nyumba yamejitokeza mara kwa mara baada ya watu kushindwa kurudisha mikopo benki.

# Songas yaipa serikali gawio la bil. 8.8/-

**Na Moshi Lusonzo**

KAMPUNI ya kuchakata umeme kutokana na nishati ya gesi ya Songas imetoa gawio la Sh. bilioni 8.8 kwa serikali inayotokana na faida.

Akizungumza jijini Dar es salaam jana wakati akikabidhi gawio hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Songas, Nigel Whittaker, amesema kiasi hicho kinatokana na hisa ilizonazo kupitia Shirika la Umeme nchini (Tanesco) na Shirika la Taifa la Maendeleo ya Petroli (TPDC).

Alisema kiasi hicho kinatokana na uwiano wa hisa ndani ya kampuni, Tanesco imepata gawio la Sh. bilioni 2.2 na TPDC imepokea Sh. bilioni 6.6.

"Serikali kama mwanahisa wa kampuni kupitia mashirika yake tumeamua kulipa kiasi hicho kama gawio la faida kwa mujibu wa sheria na sisi kama kampuni tunajivunia kutokana na tukio hili muhimu," alisema Whittaker.

Alisema Songas hadi sasa inaongoza kwa uzalishaji wa umeme wa gesi Afrika Mashariki kwa asilimia 20 kwamba mikakati inaendelea kuongeza uzalishaji kutoka megwati 180 mwaka 2012 hadi kufikia 250.

"Tunaipongeza serikali kwa juhudi zake za kuhakikisha nishati ya umeme inazidi kuongezeka na kusababisha kupata matokeo chanya katika uchumi wa viwanda. Songas tutazidi kuchangia juhudi hizi kwa kuongeza uzalishaji maradufu," alisema.

Ofisa Mkuu wa Fedha, Anael Samuel, alisema Songas itazidi kutoa gawio kwa wanahisa wake kila mwaka na kwamba serikali inanufaika kutokana na uwekezaji katika kampuni hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya serikali, Kaimu Mkurugenzi wa Fedha wa TPDC, Godwin Kailembo, aliishukuru kampuni hiyo kwa kutoa fedha hizo ambazo zitatumika kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Aliipongeza kampuni hiyo kwa kutoa fedha hizo ambazo zitaelekezwa kutatua kero za wananchi maskini.

## HABARI KITAIFA

# Kesi uhujumu yakwama kisa jalada kwa DPP

**Na Cynthia Mwilolezi,**

**ARUSHA**

KESI ya utakatishaji fedha na uhujumu uchumi inayowakabili washtakiwa watano akiwamo Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Arusha, Bernad Nganga, imekwama kusikilizwa kutokana na jalada kuwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP).

Mbali na hakimu hiyo, washtakiwa wengine ni Mwanasheria wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Maneno Mbunda na Mwanasheria wa Serikali Fortunatus Mhalila.

Akiomba kuahirishwa kesi hiyo jana mbele ya Hakimu Rose Ngoka wa Mahakama ya Wilaya ya Arusha, Wakili wa Serikali, Eliainenyi Njiro, alidai kuwa kesi hiyo imekuja kwa ajili ya kutajwa japo upelelezi umekamilika.

"Mheshimiwa kesi imekuja kwa ajili ya kutajwa japo upelelezi umekamilika ila hatuwezi kuendelea nayo kwa sababu tunasubiri jalada la kesi hii litoke kwa DPP kwa ajili ya uamuzi," alidai wakili huyo.

Hakimu Ngoka alisema kesi hiyo inaahirisha hadi Septemba 17, mwaka huu, itakapotajwa.

Washtakiwa hao na wenzao Nelson Kangero na Tumaini Mdee mbali na mashtaka hayo, pia wanakabiliwa na mashtaka mengine tisa.

Mapema, washtakiwa hao walifikishwa mahakamani hapo Mei 6, mwaka huu, na kusomewa mashtaka yao 11 na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Javelin Rugahuruza, yakiwamo ya kujihusisha na rushwa, kughushi na kujipatia mali kwa njia ya rushwa kati ya Juni Mosi, 2018 na Aprili 15, mwaka huu, katika maeneo mbalimbali.

Mashtaka mengine waliosomewa ni pamoja na kuchukua rushwa ya Sh. milioni 31.5 toka kwa Kangero, utakatishaji fedha Sh. milioni 31.5, kughushi nyaraka za uongo za nyara ya serikali za kilo 15 za meno ya tembo yenye thamani ya Sh. milioni 9.8.

Mshtakiwa Kangero kwa upande wake anakabiliwa na shtaka la uhujumu uchumi kwa kukutwa na meno ya tembo vipande 15 vyenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 15 sawa na Sh. milioni 108 za Kitanzania bila kuwa na kibali cha Mkurugenzi wa Wanyamapori.




Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mhandisi Isack Kamwelwe (kulia), akionyesha picha kuashiria uzinduzi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Leonard Chamuriho na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Dk. Agnes Kijazi. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

# RAS aishauri NMB ubunifu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imetoa wito kwa benki ya NMB kuendeleza ubunifu wa bidhaa zitakazo rahisisha matumizi ya huduma za kifedha, kuwafikia wateja wengi nchini na kutoa elimu juu ya faida zake katika maendeleo ya uchumi.

Wito huo umetolewa jana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mhandisi Aisha Amour, wakati wa hafla ya Siku ya NMB na Walimu kwa Mkoa wa Kilimanjaro, iliyofanyika mjini Moshi.

"Huduma hizi hazina budi kwenda sambamba na elimu kwa wananchi mbalimbali haswa wale waliopo maeneo ya vijijini ili watu wengi zaidi wapate huduma bora zinazotolewa na ambazo hazijawafikia wengi," alisema katika taarifa iliyosomwa kwa niaba yake na Fulgence Mponzi kutoka Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro.

Alisema takwimu zinaonyesha asilimia kubwa ya wananchi wengi hasa wanaoishi maeneo ya vijijini hawajaanza kutumia huduma za fedha zinazotolewa na taasisi za kifedha, ambapo alisema wanaotumia huduma

hizo na takribani asilimia 40 tu.

"Huu ni ushahidi tosha ya kuwa warsha kama hii ni muhimu na kwamba mnachohitaji ni kuzifanya katika ngazi mbalimbali haswa kwa wale wanaoishi maeneo ya vijijini," alisema.

Mhandisi Amour aliipongeza benki hiyo kwa ushirikiano wa karibu iliyonayo kwa serikali kupitia huduma zake ikiwamo mikopo kwa wafanyakazi wa Serikali Kuu na wale wa Serikali za Mitaa.

"Takwimu zinaonyesha ya kuwa benki ya NMB imeshatoa mikopo yenye thamani ya Sh. trilioni mbili kwa wafanyakazi wa Serikali Kuu

pamoja na wale wa Serikali za Mitaa, wengi wao wakiwa walimu," alisema

na kuongeza kwa walimu wengi mikopo hiyo imewawezesha kuishi kwenye

maisha mapya ya ustaafu wakiwa wenye furaha na bila wasiwasi.

Meneja Mwandamizi wa kitengo cha wateja binafsi wa benki hiyo, Ally Ngingite, alisema taasisi hiyo imeendelea

kubuni bidhaa mpya mara kwa mara lengo likiwa ni kuboresha maisha ya

Watanzania wa ngazi zote.

"Huduma zetu zinalenga kuunga mkono juhudi za serikali katika

kuboresha maisha ya wananchi na uchumi wa Taifa, ikiwamo kuhakikisha

wananchi wanatumia huduma za kibenki badala ya kutumia fedha taslimu, ili kwenda na wakati katika ulimwengu wa matumizi mbalimbali ya fedha," alisema.

Aliongeza katika kutimiza azma hii, benki ina matawi 229 nchini kote, mawakala zaidi ya 7,000, huduma mashine za huduma za kifedha za kielektroniki (ATM) zaidi ya 800 na zaidi ya wateja milioni 2.5 ambao wanatumia huduma za kifedha za NMB kupitia simu za kiganjani."

Awali Meneja wa benki hiyo Kanda ya Kaskazini, Aikasia Muro, alisema inafarajika kuwa sehemu ya maisha ya wateja wake mbalimbali wakiwamo walimu ambao alisema ni kutokana na ukweli kuwa ni wateja wenye mchango mkubwa kwa taasisi hiyo.




# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Bodaboda sasa wajifunze, wafuate sheria barabarani

**UKAIDI** unaofanywa na waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda, ni kero kwa wananchi wengi kwa sababu unawasababishia usumbufu, zikiwamo ajali zisizo kuwa na ulazima.

Usumbufu huo hauwapati wananchi pekee, bali hata mamlaka za serikali, kikiwamo Kikosi cha Usalama Barabarani hususan wanapowatoza faini kutokana na makosa mbalimbali.

Kutokana na tatizo hili sugu, Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Fortunatus Musilim, amewataka askari wa usalama barabarani kuwakamata madereva wa bodaboda wanaokiuka sheria za usalama barabarani na kuwachukulia hatua kama ilivyo kwa madereva wengine.

Aliwataka madereva hao wanaodaiwa faini za muda mrefu kulipa mara moja kuepuka misukosuko barabarani.

Alisema dereva wa bodaboda akikamatwa mmiliki ataitwa ili kuchukua pikipiki na dereva atafikishwa mahakamani ili kuondoa mrundikano wa vyombo hivyo katika vituo vya polisi.

Alisema anaamini kuwa hakuna mmiliki ambaye anapenda kuona dereva wake wa bodaboda anavunja sheria barabarani, na kuwa ikitokea mmiliki ataitwa kuchukua pikipiki, lakini dereva ataendelea kushikiliwa na kumfikisha mahakamani.

Aliongeza kuwa wanachotaka ni pikipiki zote kuchukuliwa na kuondolewa kwenye vituo vya polisi, baada ya watuhumiwa kufikishwa mahakamani ili kuondoa mrundikano katika vituo hivyo.

Mkuu huyo wa trafiki ametoa onyo hilo kutokana na mwenendo mbovu wa madereva wa bodaboda katika maeneo mengi ya nchi kukiuka sheria, taratibu na kanuni za usalama barabarani kwa makusudi.

Tunasema kuwa wanafanya hivyo makusudi kwa kuwa wamekuwa wakipewa maelekezo, elimu na hata kuonywa, lakini wanapuuza badala yake kuendesha pikipiki zao kama wanavyotaka wao.

Kwa mfano, wamekuwa wakisisitizwa kuvaa kofia ngumu kila wakati kwa ajili ya usalama wao hususani pale zinapotokea ajali, lakini wanakaidi kuzivaa, hivyo mara kwa mara kukamatwa na askari na kuwatoza faini.

Makosa mengine ni kupita katika maeneo ambayo wanapaswa kusimama kusubiri waruhusiwe na taa za kuongoza magari, lakini hawasimami, hivyo wakati mwingine kusababisha ajali.

Bodaboda wanatakiwa kuvaa viatu, lakini wengi wao wanakiuka badala yake kuvaa ndala au viatu vya wazi, hivyo kujikuta mara kwa mara wakiandikiwa kulipa faini, ambazo huwa wagumu kuzilipa.

Matokeo yake pikipiki zao hukaa muda mrefu katika vituo vya polisi na kusababisha mrundikano.


Hali hiyo huwasababishia usumbufu mkubwa wamiliki wa pikipiki hizo kutokana na kutakiwa kwenda kuzikomboa katika vituo vya polisi, hivyo tunapendekeza kuwa kuna haja ya kuangaliwa upya biashara ya usafirishaji abiria kwa kutumia bodaboda na ikiwezekana itungwe sheria mahususi.

Sheria hiyo iwalazimishe madereva wa bodaboda kuhudhuria mafunzo katika taasisi zinazotambuliwa na serikali ili wawe na ujuzi pamoja na kuzijua sheria za usalama barabarani, badala ya mhusika kujifunzia vichochoroni chombo hicho siku moja kisha anaanza kuendesha kwenye barabara kuu!

Kwa kufanya hivyo, vitendo vya kihuni, ubabe vitapungua kwenye barabara zetu pamoja na ajali za kizembe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace, MKURANGA

## Hongera TGNP ya robo karne iliyobeba vikokotoo vya Beijing

**MIAKA** 25 si mchezo. Kwa binadamu, ni mtu mzima tena ametimia kisawasawa, kwa haki zote za ki- utu uzima. Ikihesabiwa miaka inatisha. Ni simulizi ya robo karne hivi. Kama uliganishi na umri wa mnyama simba, basi ni 'mbabu' kama siyo 'mbibi.'

Nikirudi katika kinachonituma kuandika hivi sasa, nikiwa mshabiki na mtetezi wa jinsia, ni umri sawa na yanayotendwa na chombo chetu kinachotetea pande zote za jinsia, ikitaka kushuhudia haki.

Lakini, mzizi wa mwanzo wa chombo hicho ninachoanza kukieleza kwa mafumbo, asasi ya TGNP Mtandao, ni utetezi wa haki za kinamama, katika mustakabali mpana na mafanikio iliyoyapata, kwani ni ya kutupa furaha. Laiti ningekuwa jukwaani, ningehamasisha watu kuitikia 'oyee' na kuomba vigelegele kwa kinamama.

Ni rasmi imetimu miaka 25 tangu TGNP Mtandao kuanzishwa na harakati zake za kumkomboa mwanamke kitaifa. Iko katika hatua ya umri robo karne.

Katika kutimiza miaka hiyo, limeandaliwa tamasha la jinsia ambalo litakutanisha watu zaidi ya 1m 500 kutoka ndani ya nchi na nje ya nchi.

Kuwapo tamasha hilo, naimani kutasaidia washiriki kufahamu mambo mengi ambayo yamekuwa yakifanywa na asasi yetu TGNP Mtandao, sisi wanahabari kina dada kwa kina kaka, ni wadau wake hasa.

Mbali na TGNP Mtandao, kuandaa tamasha hilo, pia ni siku ambayo Beijing inatimiza miaka 25 toka watoke kupigania harakati za kumkomboa mwanamke kutoka alipokuwa hadi sasa alikofikia.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi anasema katika kutimiza miaka hiyo,wameandaa tamasha la jinsia, litakalojumuisha zaidi ya washiriki 1500 na la siku nne, kati ya Septemba 23 hadi 27.

Anasema kuandaliwa tamasha hilo, kutatoa fursa mbalimbali kwa washiriki kunufaika nazo, kutokana na kubadilishana mawazo yao.

Lilian anasema, katika tamasha hilo maudhui ya mjadala wa Beijing yatajadiliwa na kutoa picha ya tangu walipofanya kikao hicho Beijing na kuzungumzia mafanikio tangu walipotoka jijini Beijing.

Anasema, ni historia ya harakati za ukombozi kwa wanawake, kuwa azimio la mkakati wa Beijing, katika mpango kazi wa harakati za ukombozi kuwalinda wanawake.

Mkurugenzi huyo wa TGNP Mtandao, anasema asasi hiyo za kiraia ilianzishwa ili kutetea haki za wanawake, mzizi wake ni walioratibu safari hiyo kati ya mwaka 1991 hadi 1995. Kuanzishwa kwake rasmi ni mwaka 1993.

Lilian anasema, watu wengi hawajui uhalisia wa dhana ya jinsia na kuona kuwa ni neno linalomhusu mwanamke pekee yake.

Kwa mujibu wa Lilian, baada ya kuanzishwa ikiwa na idara moja pekee, idara ya pili ilibuniwa baada ya kugundua upana na haja ya jamii kufahamu masula yanayohusu jinsia.

Anasema ni idara iliyokuwa inatoa uelewa mpana kwa masuala mbalimbali ya kiserikali na asasi za kiraia na idara ya tatu ilisaidia masuala ya ushawishi usuluhishi na utetezi, kuleta mabadiliko kwa katika masuala ya sera, baada ya kubaini uhaba katika masuala hayo ya kijinsia.

# Wakumbushwa agizo la Rais

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), imeagizwa kutekeleza agizo la Rais John Magufuli la kufanya utafiti ili kujua sababu za ongezeko la magonjwa ya kansa nchini hasa katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Agizo hilo lilitolewa jana jijini hapa na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alipokuwa anafungua mkutano wa wadau wa utafiti wa masuala ya afya wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema Rais alitoa agizo hilo muda mrefu, lakini bado halijatekelezwa, hivyo akawataka kuharakisha na taarifa yake itolewe ili kurahisisha utoaji wa elimu kwa wananchi.

Dk. Ndugulile alisema NIMR imekuwa ikifanya utafiti mbalimbali wa magonjwa ya binadamu lakini hayaisaidii Tanzania na badala yake inayanufaisha mataifa mengine duniani kutokana na taarifa hizo kutokuwa za wazi.

Alizitaja baadhi ya utafiti uliofanywa na taasisi hiyo kuwa ni wa chanjo ya Ukimwi, ebola na kansa na magonjwa mengine, lakini wataalamu hao hawazisemi zikajulikana kwa wadau wengine wakiwamo watunga sera.

Alisema taarifa hizo zimesaidia kutokea kwa mabadiliko hata kwenye dawa za chanjo ya magonjwa hayo, lakini zimebaki kwenye maabara na hata yeye amezijua baada ya kuingia kwenye maabara ya taasisi hiyo.

"Nimeona nitumie muda huu kutoa changamoto hii. Rais Magufuli alitoa maelekezo ya kufanya utafiti wa kansa Kanda ya Ziwa ili tujue sababu ya kuongezeka kwake, lakini bado sijaona utekelezaji wake," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NIMR, Prof. Yunus Mgaya, alisema agizo la Naibu Waziri litatekelezwa kwa wakati na kwamba wamebaini kuwa taarifa nyingi ziko kwenye hospitali, vituo vya afya na zahanati lakini bado hazijafanyiwa kazi.

Alisema watahakikisha wanazitumia taarifa hizo kwenye tafiti zinazotakiwa kufanyika na kwamba lengo la mkutano huo ilikuwa ni kuendeleza ushirikiano kati ya watafiti, watunga sera, watoa huduma za afya na watekelezaji wa sera.




Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, wakati akitambulisha Tamasha la Utalii Festival linalotarajiwa kufanyika kwa baadhi ya mikoa hapa nchini kwa kuratibiwa na wizara hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo. Kushoto ni Naibu Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Juliana Shonza. **PICHA; WMU**

# DC anasa mitambo, lita 4,800 za gongo

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

OPERESHENI ya siri inayoongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, ya kuwabaini wafanyabiashara sugu wanaotengeneza na kusambaza pombe haramu ya gongo, imenasa lita 4,800 na mitambo sita katika kiwanda kidogo kilichojitenga na makazi ya watu.

Jana, Ole Sabaya alikwenda kimya kimya katika Kijiji cha Mtakuja, Kata ya KIA bila ya kuwa na askari polisi na kuwanasa watu wanne ambao wanadaiwa kuwa wamiliki wa mitambo hiyo.

"Ni kweli nimekwenda mwenyewe kijiji cha Mtakuja na nimewakamata hao watu na kuita polisi wakaja kuwachukua. Nilikuta kiwanda kimoja kina lita 4,800 za pombe hiyo, mapipa 42 na mitambo sita ya kuzalisha gongo," alisema.

Alisema mbali na wafanyabiashara hao wanne, pia ameagiza uongozi wa serikali ya kijiji cha Mtakuja na Ofisa Mtendaji wa Kata ya KIA kuwapelekea taarifa ya wito ya kujisalimisha katika ofisi yake ndani ya saa 72.

Baada ya kuwanasa wafanyabiashara hao waliokuwa wakidhani ni mteja, Mkuu huyo wa Wilaya alipiga simu kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo, Lwelwe Mpina, na kufika eneo hilo akiwa na askari katika magari matatu na kuchukua miundombinu yote pamoja na watuhumiwa hao.

Akiwa katika kijiji hicho, Ole Sabaya aliagiza polisi kuwahoji watuhumiwa hao ili kubaini wenzao wanaoshirikiana nao katika biashara hiyo haramu na uchunguzi ukikamilika wapelekwe mahakamani.

Ulevi wa kupindukia, unazitesa baadhi ya kaya katika Wilaya ya Hai hasa vijiji vya pembezoni vilivyoko katika ukanda wa tambarare kutokana na kuendelea kukithiri kwa unywaji na uuzwaji wa pombe ya moshi, maarufu kama gongo.

Ziko taarifa kwamba wako pia baadhi ya wanafunzi wamejiingiza katika unywaji wa pombe hiyo, kitu ambacho kinaelezwa kumtia hasira Mkuu huyo wa Wilaya.

Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini, Leonard Minja, akizungumzia kadhia hiyo, alisema taifa linapoteza vijana wanaotegemewa kukuza uchumi kutokana na watu ambao hawana nia njema ambao wamekuwa wakifanya biashara ya gongo.

Mchungaji Minja alisema kutokana na serikali kuwa na mkono mrefu, anaunga mkono mkakati huo wa kudhibiti pombe hiyo, huku akiitaka serikali isifanye operesheni hiyo kuwa moto wa kifuu.

# Serikali yawataka wauza madini kuyaongezea thamani

**Na Adelina Charles**

WIZARA ya Madini imeziomba nchi za Afrika kuangalia uwezekano wa kufunganisha biashara ya madini na shughuli nyingine za kiuchumi.

Pia imewataka wauzaji na wachimbaji wa madini nchini kuyaongezea thamani kwa kutengeneza vitu mbalimbali badala ya kuuzwa kama madini.

Akizungumza na vyombo vya habari hivi karibuni, Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Profesa Simon Msanjila, alisema jitihada za pamoja zitawezesha nchi husika kunufaika na madini moja kwa moja kwa kuwa bidhaa zitanunuliwa nchi husika.

Alisema iwapo wachimbaji na wauzaji wa madini watajishughulisha na shughuli nyingine za kiuchumi kama kutengeneza mikufu, cheni na bidhaa nyingine za madini na kuacha kutegemea madini peke yake, watapiga hatua kubwa kwenye maisha.

"Tujitahidi kuongeza thamani ya madini tuweze kuuza madini ya thamani na tuende zaidi tusiuze madini, tuuze mazao ya madini ambayo tutajua tumetengeneza wenyewe na faida itakuja kwetu ikiwamo kuongeza ajira kwa watu wetu," alisema.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu huyo, kufunguliwa kwa masoko ya madini kumeleta mabadiliko makubwa na wizi wa madini kwa sasa umepungua kwa kuwa dhahabu iliyokuwapo sokoni ndio iliyokuwa ikitoroshwa bila kulipa kodi.

Mathalani, alisema soko la Geita dhahabu iliyouzwa katika soko hilo ni kilo 500 ndani ya mwezi mmoja kwa wachimbaji wadogo hali ambayo haikuwahi kutokea.

Masoko mengine yanayofanya vizuri ni Chunya na Kahama huku la Mererani likivunja rekodi.

# 'Machangudoa' watangaziwa kiama Dom

**Na Adelina Charles, TUDARCO**

JESHI la Polisi mkoani Dodoma, limetangaza kiama kwa wanawake wanaouza miili yao kwa kuchukua hatua za kisheria ikiwamo kuwafikisha mahakamani.

Kauli ya jeshi hilo umetolewa siku chache baada ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani Hamad Yusuph Masauni, kulieleza bunge kuwa hatua zitaanza kuchukuliwa dhidi ya wanaume wanaonunua 'changudoa'.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma Gilles Muroto, alisema tayari 'changudoa' 15 wamekamatwa na kufikishwa katika Mahakama ya Mwanzo Makole na kufungwa miezi sita bila kulipa faini.

"Kwa siku ya jana wamekamatwa 'changudoa' saba, na polisi wanaendelea kufanya msako sehemu mbalimbali ili kupata wahalifu wanaokuja kuchafua jiji letu na makao makuu yetu ya nchi kuhakikisha kwamba hawapati nafasi katika mkoa wetu,"amesema Muroto.

Muroto alisema lengo ni kumaliza tabia hiyo mbaya kwa kuwa inachangia ongezeko la maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Alitoa tahadhari kwa waliobaki au wenye mpango wa kwenda Dodoma kuuza miili yao kuacha kwa kuwa watachukuliwa hatua.

Alimshukuru Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Mariam Salum Msabaha, aliyeibua suala hilo bungeni na waziri kutoa kauli.

# Pasi kielektroniki zabaini Watanzania wengi nje

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, amesema utaratibu wa utoaji wa hati mpya za kusafiria za kielektroniki umesaidia nchi kujua Watanzania wengi wanaoishi ugenini.

Prof. Kabudi aliyasema hayo juzi alipokuwa akikabidhi tiketi za ndege kwa vijana 100 kati ya 1,440 ambao wamechaguliwa kwenda Israel kujifunza ujuzi wa kilimo hasa kinachofanyika kwenye maeneo yenye ukame.

Akizungumza baada ya kukabidhi tiketi hizo kwa vijana hao ambao jana walianza safari ya kuelekea Israel, Prof. Kabudi alisema utaratibu mpya wa utoaji hati hizo za kusafiria umewezesha kuwabaini Watanzania wengi ambao wanaishi kwenye mataifa mbalimbali duniani.

"Mfano katika nchi ya Australia peke yake wapo Watanzania 3,000 wanaoishi huko na siyo kwamba hawana kazi ni watu wenye taaluma zao, New Zealand wapo Watanzania 1,500, hizi ni nchi za mfano, lakini kwenye mataifa mengi wapo na ni wengi. Hawa ni wale waliokwenda kwa utaratibu, bado wale ambao walizamia," alisema.

Akizungumza na vijana hao wanaokwenda Israel, Prof. Kabudi, aliwataka wakifika Israel wahakikishe wanajiepusha na vitendo vya ulevi na mambo yanayoendana na hilo.

Pia aliwataka wahafamu kuwa nchi hiyo kwenye suala la usalama ni la kiwango cha juu, hivyo wajue jinsi ya kuishi na kuenenda kwa kipindi chote cha mwaka mzima.

"Mlijitokeza vijana 1,440 kuomba nafasi hii ya kwenda kusoma Israel, lakini kati ya hao mmechaguliwa 100. Ujuzi mtakaoupata mnatakiwa mrudi nao hapa na mje kuleta mapinduzi katika kilimo.

"Ipo mikoa ambayo ina ukame kama Dodoma, Singida, Shinyanga, na Manyara, tunategemea mtakaporudi ubunifu, ujuzi na uzoefu mtakaoupata mtawezesha mikoa hii uzalishaji wa mazao kuongezeka na duniani maeneo yenye ukame yanaongoza kwa uzalishaji. Dodoma ni sehemu pekee duniani inayovuna zabibu mara mbili kwa mwaka."




Meneja wa Kanda ya Tanzania Freight in Time (FIT), Fred Mlay (katikati), akitoa ufafanuzi kwa wateja waliotembelea banda la kampuni hiyo, katika maonyesho yanayoenda sambamba na mkutano wa mwaka wa mashauriano wa Bodi za AQRB, CRB, ERB pamoja na wadau wa sekta ya ujenzi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

# Kilio chatanda kulaani ubaguzi

INATOKA UK. 2

na kufanya shughuli za kijamii kuliko kuendekeza vitendo vya uvunjifu wa amani.

Naye kiongozi wa chama kikuu cha upinzani Afrika Kusini cha Economic Freedom Fighters (EFF), Julius Malema, akizungumza na waandishi wa habari juzi, aliwataka wananchi wa Afrika Kusini kutoendelea na vurugu.

Alisema kuwapiga wageni na kuwanyang'anya mali zao hakutakuwa msaada kwao kumaliza matatizo yao na kwamba ukosefu wa ajira na umaskini havijasababishwa na raia wa kigeni bali serikali iliyoko madarakani.

Alisema matatizo yaliyopo Afrika hayatamalizwa na kutokuwa na umoja bali yatamalizwa kwa umoja na ujamaa.

**UN YALAANI**

Ofisa wa Umoja wa Mataifa (UN) anayejihusisha na masuala ya wanawake, Dk. Phumzile Mlambo-Ngcuka, akihojiwa na Shirika la Utangazaji la Afrika Kusini (SABC), alisema vitendo vinavyofanywa na raia wa Afrika Kusini ni kinyume cha haki za binadamu.

Alisema UN inalaani vitendo hivyo na kuwataka viongozi husika kuvidhibiti kabla madhara makubwa hayajatokea.

**MSIMAMO WA TANZANIA**

Naye Prof. Kabudi alisema Tanzania inaungana na serikali ya Afrika Kusini kulaani vikali vitendo vya ubaguzi na mashambulizi vinavyofanywa na raia wachache wa nchi hiyo dhidi ya raia wa nchi zingine za Afrika na kuziasa nchi zingine kutolipa kisasi kutokana na vitendo hivyo.

"Hadi sasa hakuna taarifa kuhusu Mtanzania kuuawa, kujeruhiwa au kuharibiwa mali kutokana na vurugu hizo. Wizara itaendelea kutoa taarifa za uhakika kadri zinavyopatikana kutoka kwenye vyanzo vya uhakika ukiwemo Ubalozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini," alisema Prof. Kabudi.

Alisema vitendo vinavyofanywa na raia wachache wa Afrika Kusini vya kuwashambulia raia kutoka nchi zingine za Afrika na kuharibu mali zao vinasikitisha na kuivunjia heshima nchi hiyo.

Prof. Kabudi alisema serikali ya Tanzania inaunga mkono kauli ya Rais Ramaphosa aliyoitoa hivi karibuni ya kukemea na kulaani vikali vitendo vinavyofanywa na raia hao wachache.

"Ni jambo la kusikitisha lakini serikali ya Afrika Kusini inalisimamia kikamilifu na sisi tuko tayari kushirikiana nao ili kulitafutia ufumbuzi wa kudumu. Nawasihi Watanzania wenzangu tusilipize kisasi na tutaendelea kuwalinda raia wa Afrika Kusini waliopo Tanzania kwani tunaamini kuwa Afrika ni moja na waafrika ni ndugu zetu," alisema Prof. Kabudi.

Aliongeza kuwa vitendo hivyo ambavyo vinatokana na raia hao wengi kukosa ajira, ardhi na pia kutopenda kujishughulisha havihalalishi watu wengine wakiwamo Watanzania kulipa kisasi kwa namna yoyote ile.

HABARI MIKOANI

# Bosi wa trafiki aagiza kibano kikali kwa bodaboda wakaidi

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

KAMANDA wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Fortunatus Musilim, amewataka askari wa usalama barabarani kuwakamata madereva wa bodaboda wanaokiuka sheria za usalama barabarani na kuwachukulia hatua kama ilivyo kwa madereva wengine.

Alisema hakuna mtu yeyote aliyezuia kukamatwa kwao, na kuwataka madereva wanaodaiwa faini ya muda mrefu kulipa mara moja kuepuka misukosuko barabarani.

Musilimu alisema hayo alipozimama na kuzungumza na askari wa kikosi hicho wa Mkoa wa Morogoro waliokuwa kwenye shughuli za ukaguzi na ukamataji wa madereva wazembe kwenye barabara kuu ya Morogoro-Dodoma wakati njiani akitokea Dodoma kuelekea Dar es Salaam.

Alisema bodaboda akikamatwa mmiliki ataitwa ili kuchukua pikipiki na dereva atafikishwa mahakamani ili kuondoa mrundikano wa vyombo hivyo katika vituo vya polisi.

"Tunaamini hakuna mmiliki ambaye anapenda kuona dereva wake wa bodaboda anavunja sheria barabarani, mmiliki ataitwa kuchukua pikipiki na tutaendelea kumshikilia dereva na kumfikisha mahakamani," alisema Musilim.

Aliongeza kuwa wanachotaka ni pikipiki zote kuchukuliwa na kuondolewa kwenye vituo vya polisi, baada ya watuhumiwa kufikishwa mahakamani ili kuondoa mrundikano katika vituo hivyo.

Aliwaonya madereva wa magari waliotozwa faini kwa makosa mbalimbali kulipa ndani ya siku saba kwa mujibu wa sheria kupitia mifumo mbalimbali ya kifedha, na wanaokiuka na kulimbikiza madeni hayo watakamatwa katika operesheni ya 'nyakua nyakua' inayoendelea na kufikishwa mahakamani.

Mkuu wa kikosi hicho Mkoa wa Morogoro, Michael Deleli, aliahidi wataendelea kuwakamata madereva wote wazembe na wasiofuata sheria hadi maeneo ya katikati ya mji ambako wanaanzisha operesheni kabambe.



Mwendesha guta akiwa amepakia mzigo na abiria aliyeuchapa usingizi, katika Barabara ya Kawawa, eneo la Ilala, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**.

## NEMC, wafanyabiashara taka hatarishi wakubaliana

**Na Enock Charles**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limekubaliana na wafanyabiashara namna bora usimamizi na udhibiti wa taka hatarishi baada ya kupata ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili wafanyabiashara hao.

Akizungumza katika mkutano wa wadau kuhusu usimamizi na udhubiti wa taka hatarishi ulioandaliwa na NEMC jijini Dar es Salaam, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, alisema wadau hao wamekuwa ni muhimu katika kuzalisha ajira, kuliingizia taifa pesa za kigeni na katika kutunza mazingira.

"Serikali inatambua nafasi yenu katika safari ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati na viwanda kwani mmekuwa wazalishaji wakubwa wa ajira, mnasaidia utunzaji wa mazingira kwa kukusanya taka hizo hatarishi na hata kuliingizia taifa pesa za kigeni," alisema Simbachawene.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema baraza limejipanga vizuri kwenda sambamba na sera ya uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

"Tunazo ofisi zetu katika kanda nane hapa nchini na hii inarahisisha upatikanaji wa huduma kwa wadau wa mazingira, hivyo nawaomba wafanyabiashara kutumia ofisi hizo ili kupata miongozo kanuni na sheria mbalimbali zinazosimamiwa na baraza ili kuepuka makosa ambayo yamekuwa yakifanywa na wadau kwa kutokujua," alisema Dk. Gwamaka.

Dk. Gwamaka alisema kuwa baraza litatekeleza maagizo yote ambayo waziri ameyatoa kwa baraza hilo na kutekeleza mikakati ya udhibiti katika biashara hiyo kwa lengo la kuhakikisha uhalali wa biashara na utunzaji wa mazingira unazingatiwa.

# Rais Magufuli kutunukiwa tuzo ya ujasiri, uzalendo

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli anatarajia kutunukiwa tuzo maalumu iitwayo 'Tuzo ya Wananchi kwa Rais', ambayo imetambua ujasiri, uzalendo, uthubutu na uadilifu aliofanya katika kusimamia rasilimali za taifa kwa maendeleo ya Watanzania wote.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Kamati ya Tuzo ya Wananchi kwa Rais, Nazar Nicholas, alisema Rais Magufuli amekuwa hodari na zaidi amekuwa jasiri, mzalendo, mwenye uthubutu na mwadilifu.

"Pamoja na kumkabidhi tuzo hiyo, pia atakabidhiwa kitabu chenye maneno bilioni moja, kitabu hiki kitabeba maudhui ya kumwambia asante kwa ujasiri, uzalendo, uthubutu na uadilifu wao, pia kitakuwa na maneno ya kumtia nguvu na kumwombea kwa Mungu ili afanikiwe zaidi," alisema Nicholas.

Alisema lengo la tuzo hiyo ni kusherehekea kipawa cha utendaji kazi ya Mungu aliyoiweka ndani ya Rais Magufuli.

Nicholas alisema tuzo hiyo pia inamtambua Rais Magufuli katika maeneo manne ambayo amefanikiwa kwa kiwango kikubwa ambayo ni ujasiri, uzalendo, uthubutu na uadilifu.

Aliongeza kuwa mchakato wa kumtunuku tuzo Rais Magufuli utachukua muda wa miezi 12 hadi kufikia kilele cha siku ambayo atakabidhiwa tuzo hiyo.

Alisema kabla ya kufikia kilele cha siku ya kumtunuku tuzo hiyo, shughuli mbalimbali zitatekelezwa kama vile shindano maalum la kutatua kero ya wananchi, uandishi wa kitabu cha tuzo ya wananchi ya Rais Magufuli, shindano la kuchora picha ya Rais, shindano la insha ya wanafunzi juu ya uzalendo, tamasha la vijana kumwombea Rais.

Alisema matukio mengine ni mashindano ya mchezo wa mpira wa miguu, midahalo juu ya uzalendo, shughuli za vikundi, ripoti ya kero zilizopatiwa suhulu.

# Kaya kuadhibiwa fedha za TASAF

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema endapo kaya itashindwa kutimiza masharti ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) kuhusu kuhakikisha watoto kuhudhuria shuleni au upelekaji watoto kliniki fedha hizo zitakatwa kama adhabu.

Kauli hiyo ilitolewa bungeni jana na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Tunduru Kaskazini (CCM),Ramo Makani.

Makani alihoji serikali itachukua hatua zipi za makusudi kurekebisha kasoro ambazo zinalalamikiwa na wananchi wa Tunduru ili wananchi wapate kunufaika vema zaidi na huduma za mpango husika.

Akijibu swali hilo, Mwanjelwa alisema malalamiko ya walengwa kuhusu makato ya fedha kipindi cha malipo, suala hilo wanaendelea kuelimishwa kwanini makato yanatokea.

"Sababu za kukatwa fedha za zao ni kutokana na kutimiza masharti ya kupokea ruzuku hasa kwa kaya zenye watoto walio shuleni na wale wanaotakiwa kuhudhuria kliniki ambao ni watoto wenye umri chini ya miaka Alibainisha endapo kaya itashindwa kutimiza masharti fedha zitakatwa kama adhabu na kuwaomba wabunge kwenye ziara zao kusaidia kutoa elimu ili kuepusha malalamiko ambayo si ya lazima.

Alieleza kuwa serikali kupitia TASAF changamoto kubwa ambayo Mpango unakumbana nao ni kilio kutoka kwa baadhi ya wananchi maskini ambao hawajafikiwa na huduma za Mpango huo kwenye vijiji, mitaa, shehia takribani 5,693 ambavyo havijafikiwa katika awamu ya kwanza ya Mpango huo.

Hata hivyo, aliwahakikishia wabunge kuwa utaratibu umeshaandaliwa wa kuweza kufikia kwenye vijiji, mitaa na shehia hizo mara tu baada ya mpango kuanza utekelezaji.

Katika awamu hiyo, alisema Tasaf imejipanga vizuri kuhakikisha kuwa yale malalamiko ya upendeleo, ubaguzi na kuachwa kwa watu maskini kuandikishwa kwenye mpango huo hayajirudii na mifumo ya kielektroniki itatumika.

Alitoa rai kwa wabunge kwamba muda utakapofika wahakikishe wanalisimamia vizuri zoezi la utambuzi wa walengwa ili wale wanaostahili ambao ni kaya maskini pekee waandikishwe kwenye mpango.

Alionya kuwa hatua kali zitachukuliwa kwa viongozi na watumishi katika ngazi zote ambao katika maeneo yao watabainika kuwepo watu au kaya zisizo na vigezo kwenye awamu ya pili ya mpango huo .



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, akizungumza jambo katika mkutano wa siku moja uliowakutanisha wafanyabiashara ya vyuma chakavu jijini Dar es Salaam kujadili na kutoa ufumbuzi juu ya changamoto zinazoendelea kujitokeza kwenye mfumo wa usimamizi na udhibiti wa biashara hiyo na taka hatarishi nchini na kuongozwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene (hayupo pichani). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizara yapitia mfumo usambazaji pembejeo

WIZARA ya Kilimo inapitia mfumo mzima wa usambazaji pembejeo za mazao ili kuondokana na ucheleweshaji na wizi unaoendelea katika usambazaji wa pembejeo ambao mwisho wa siku mkulima anabeba mzigo huo, Bunge limeelezwa.

Sambamba na hilo, Mfumo wa usambazaji pembejeo za pamba msimu ujao utabadilika na kwamba tathmini ya awamu imeonekana wakulima wa pamba mwaka huu wanalipia pembejeo ambazo aidha hawakuzitumia ama wanabebeshwa mzigo.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Bunda{CCM}, Boniface Getere aliyetaka kujua kama wakulima wa pamba katika msimu 2019/20 watakatwa fedha ya pembejeo.

"Msimu wa pamba 2018/19 walichanga Sh.100 kwa kila mkulima, kwa maelezo kuwa 2019/20 hatutakatwa pembejeo, naomba kupata maelezo ya serikali pembejeo wakulima wanakatwa au hawakatwi?" alihoji.

Akijibu, Bashe alisema katika msimu huu wa kilimo mambo mengi yatabadilishwa katika usambazaji wa pembejeo.

Naibu Waziri huyo alisema wakulima wa pamba watakatwa fedha za pembejeo msimu huu wa mwaka 2019/20 na kwamba katika msimu uliopita fedha walizokatwa zililipa madeni ambayo wakulima walipewa pembejeo katika msimu uliotangulia.

Bashe alisema wizara nguvu yake ni kupitia mchakato mzima na hatua zitachukuliwa kwa watu wote waliowaibia wakulima wa pamba kwa mwaka huu.

"Msimu ujao wa pamba mkulima atapewa fomu na bodi ya pamba ambazo tatu ambayo itaonesha mkulima aliyechukua pembejeo na thamani halisi ili msimu wakati wa kuuza pamba ijulikane bei halali kwa kuwa vyama vya ushirika vinawaibia wakulima wa pamba," alisema

Katika swali la msingi, Mbunge wa Ukerewe {CCM}, Joseph Mkundi, alihoji mkakati wa serikali wa kufanya utafiti wa kisayansi ili kushauri wananchi wa Ukerewe aina ya mazao yanayopaswa kulimwa na jinsi ya kutumia eneo dogo la ardhi kwa ufanisi.

Akijibu, Bashe alisema Mkakati wa serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania {TARI} ni kufanya utafiti wa tabaka na afya ya udongo katika kanda zote saba za kiikolojia za kilimo nchini ikiwemo kanda ya Mwanza.

Alisema utafiti huo wa kisayansi unalenga kubaini aina za virutubisho na tabia za udongo katika maeneo mbalimbali pamoja na kubaini mimea na mazao yanayostawi kwenye udongo husika ili kutoa elimu kwa wakulima kuhusu kiasi, aina na matumizi sahihi ya mbolea za viwandani na asili.

Aidha, alisema katika wilaya ya Ukerewe ambayo wananchi wengi hulima mihogo, mpunga, mtama, mahindi na viazi vitamu na machungwa. Alisema utafiti wa awali umeonyesha kwamba udongo wake una mboji kiasi kidogo chini ya asilimia 1.3 ukilinganisha na kiwango cha asilimia 2.5 hadi 3.5 ambacho ndicho kiwango cha mboji kwa udongo wenye rutuba nzuri.

Alisema sampuli za udongo zimechukuliwa katika kanda na mikoa mbalimbali nchini ukiwamo Mkoa wa Mwanza unaojumuisha Wilaya ya ukerewe kwa lengo la kubaini viwango vya virutubisho vilivyopo katika sampuli hizo ambapo kwasasa tathmini ya kina inaendelea kufanyika katika maabara ya TARI Selian.




# Ushirikiano wa athari tabiamchi

NAIBU Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima, amesema serikali itaendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi, kudhibiti mmomonyoko wa udongo na kukabiliana na uhaba wa udongo.

Sima alitoa kauli hiyo bungeni jana wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Mwamtumu Dau Haji(CCM) ambaye alisema kuwa kasi ya mmomonyoko wa ardhi na uhaba wa udongo katika visiwa vya Unguja na Pemba vinatishia uhai wa visiwa hivyo.

Alihoji ni hatua zipi za makusudi zimechukuliwa katika kuvinusuru visiwa hivyo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema visiwa vya Unguja na Pemba vina maeneo takribani 148 yaliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi(pemba 125 na Unguja 23).

Alisema athari hizo ni pamoja na mmomonyoko wa fukwe na kuingia kwa maji ya bahari katika mashamba na makazi ya watu.

Alieleza kuwa ili kuvinusuru visiwa hivyo dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi, Serikali imechukua hatua mbalimbali kupitia miradi inayofadhiliwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya tabianchi.

Alibainisha kuwa kupitia mradi wa kujenga uwezo wa jamii kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi- LDCF ambao umetekelezwa 2012-2018, shughuli zilizofanyika ni ujenzi wa kuta mbili za mita 25 kila moja katika eneo la kisiwa Panza-Pemba.

Nyingine ni ujenzi wa makinga bahari matano ya wastani wa urefu wa mita 100 kila moja katika eneo la urefu wa mita 538 Kilimani-Unguja, upandaji mikoko pemba maeneo ua kisiwa Panza hekta 200, Tumbe hekta 19, ukele hekta 7 na Tovuni hekta 1 na upandaji mikoko Unguja maeneo ya Kisakasaka hekta 8 na Kilimani hekta 1.4.

Aidha, alisema kupitia mradi wa kupunguza uharibifu wa ardhi na kuongeza uzalishaji wa chakula katika maeneo kame nchini (2017-2022), na shughuli zinazotakiwa kufanyika katika maeneo ya Micheweni kata ya Micheweni na Kiuyu Maziwang'ombe.

Alizitaja kazi hizo ni kujenga makinga maji katika mashamba ili kuzuia maji ya bahari kuingia katika mashamba, kutoa elimu kuhusu kilimo kinachokabiliana na mabadiliko ya tabianchi kupitia mashamba darasa.

Alitaja nyingine ni upandaji wa miti ili kuhifadhi udongo na kutunza mazingira na uanzishaji wa biashara ndogo ndogo ili kuwezesha jamii kuwa na shughuli mbadala za kujiongezea kipato.



## HABARI ARUSHA

# Wananchi wapiga kura kubaini wezi wa mifugo

**Na Allan Isack,** MBULU

WANANCHI wa Bonde la Yaeda Chini, wanaopakana na Wilaya za Mbulu mkoani Manyara na Karatu mkoa wa Arusha, wamepiga kura ya kuwafichua watuhumiwa wa wizi wa wa mifugo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Chelestino Mofuga na Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Theresia Mahongo, walisimamia kura hizo, ili kukomesha wizi wa mifugo eneo la mpakani mwa wilaya hizo.

Theresia alisema lengo la kupigwa kwa kura hizo ni kukomesha wizi kwenye eneo hilo, na kazi hiyo, ilifanyika kwa kuandika majina ya watu wanaodaiwa kuiba mifugo au wanaoshirikiana na wezi.

Mofuga alisema, pia waliwabaini mahalifu walioharibu miundombinu ya alama za mipaka ya bonde hilo na walipiga kura kwa kuandika majina ya wahusika wote.

"Hii ndiyo njia sahihi ya kutafuta wahalifu tunaamini hamtaweza kuandika majina ya watu kwa kuwaonea, na matumaini yangu tabia hii itafikia mwisho, na wizi huu utafikia kikomo maana wahusika wanajulikana na wakiendelea na tabia hii serikali itawashughulikia," alisema.

Mahongo alisema kwa sababu wameteuliwa na kula kiapo kuwa watawatumikia wananchi, hawatakubali kuona wezi wachache wanaharibu amani na kuwasababishia wananchi umaskini.

"Majina haya tutaondoka nayo ili kuyashughulika nyie wenyewe mtaona kwa vitendo na wezi hawa wataacha wizi kwani muda siyo mrefu watabainika.

Awali, baadhi ya wananchi wa eneo hilo, walituhumiana kuibiana mifugo ndipo serikali ikaandaa utaratibu wa kupiga kura za siri kwa kuandika majina ya wahusika wa matukio hayo ili kuwabaini wahalifu.

Mkazi wa Kijiji cha Matala, Julius John, alisema ana amini wezi wa mifugo wanashirikiana na mtandao mkubwa wa watu wanaoishi sehemu hizo, kuiba na kuuza mifugo hiyo.

John alisema haiwezekani mtu kutoka mbali kuiba mifugo kijijini hapo, kama hana mtandao wa watu wanaoshirikiana nao kutenda uhalifu huo.



Mmoja wa wakulima (kulia), akitoa elimu ya dawa za asili za kuhifadhia mazao pamoja na kuweka shambani katika maonyesho ya siku moja ya mbegu na vyakula vya asili yaliyoandaliwa na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima (MVIWATA), wilayani Karatu, mkoani Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA.**

# Watakiwa kurejea mbegu za asili

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

KATIBU Tawala Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, amewataka wakulima kuenzi mbegu za asili kuepukana na tishio la kutoweka kwa mbegu hizo.

Kutokana na mwingiliano wa matumizi ya mbegu za kisasa zinazoendelea kushamiri kwa wingi.

Alitoa angalizo hilo wakati wa kufungua maonyesho ya mbegu na vyakula vya asili yaliyoandaliwa na mtandao wa vikundi vya wakulima (Mviwata), yalifanyika kwa siku moja wilayani Karatu.

Katika mafunzo hayo, yaliwakutanisha wakulima wa mikoa mbalimbali nchini tena yaliyoambatana na maandamano ya kuonyesha mbegu za mazao mbalimbali ya asili.

Aidha, alisema changamoto inayoikabili mfumo wa mbegu ni pamoja na wataalamu kutokufika kwa wakati kwa wakulima kutoa uratibu wa usambazaji wa mbegu, kitendo ambacho kinasababisha wakulima wengi kutumia mbegu za kisasa zaidi kuliko za asili.

Alisema kupungua kwa uhifadhi wa mbegu kunakosababishwa na ukame kumeongeza changamoto na kuwataka wakulima kutumia maonyesho hayo, kupanua wigo kwa wakulima kutatua changamoto za utumiaji na upatikanaji wa mbegu za asili.

Mratibu wa Mviwata Mkoa wa Arusha, Richard Masandika, alisema kupitia mradi wa kilimo endelevu, sheria ya mbegu ya mwaka 2016, imekuwa kikwazo kikubwa kwa wakulima katika kuendeleza mfumo wa mbegu za asili.

Aliiomba serikali kutazama upya sheria hiyo, ili matumizi ya mfumo usio rasmi uweze kutambulika na kufufua matumaini mapya kwa mkulima.

Alisema wadau wa kilimo endelevu waliamua kuwasaidia wakulima kupunguza kero ya upatikanaji wa mbegu kwa kufufua mfumo wa matumizi ya mbegu za asili ambao wakulima wengi wanautumia kwa kuhamasisha uhuru wa mbegu.

Mwenyekiti wa Mviwata, John Safari, aliiomba serikali kutambua mfumo wa mbegu usio rasmi ili wakulima wapate uhuru wa matumizi yanayokubalika kwani sheria za mbegu hapa nchini, hazitambui mbegu za asili.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wengine waliohudhuria maonyesho hayo, Anastazia Tuta, aliiomba serikali kuzitambua mbegu za asili na kuweka sheria ya kuziandaa kwa mfumo ulio rasmi kwani mbegu hizo, hazitumii gharama kubwa kama zile zilizoboreshwa.

# Kiwanda chaomba serikali kuingilia mgogoro h/shauri

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KIWANDA cha kusindika nyama jijini Arusha, kimelalamikia Halmashauri ya Jiji la Arusha kukikwamisha na kuiomba serikali kuingilia kati kumaliza mgogoro huo.

Kiwanda cha Happy Sausage ndicho kinacholalamikia halmashauri hiyo na kuiomba Wizara ya Uvuvi na Mifugo, kuingilia kati kwani mgogoro huo unakwamisha shughuli za uzalishaji kiwandani hapo na kushindwa kufikia soko la kimataifa likiwamo la Afrika Mashariki.

Mwenyekiti wa Bodi ya Kiwanda hicho, Andrew George, alisema wakati akizungumza na vyombo vya habari kiwandani hapo, kuelezea shughuli zinazofanywa na kiwanda hicho, pamoja na changamoto zinazowakabili.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Arusha, imeendelea kukwamisha juhudi za ukarabati wa kiwanda hicho, kwa kukataa kutoa kibali cha ujenzi -bulding permit, wakati Wizara ya Mifugo na Bodi ya Nyama walishatoa maelekezo ya kufanyika kwa ukarabati.

Mwenyekiti huyo alieleza hatua hiyo, imetokana na mgogoro wa muda mrefu unaliodumu kwa kipindi cha miaka nane kati ya pande hizo kutokana na kushindwa kufikia makubaliano ya umiliki wa ardhi ya eneo la kiwanda ambalo hadi sasa kila upande umekuwa unavutia upande wake.

Alisema halmashauri hiyo ni mbia kati ya wabia 12, waliowekeza katika eneo la kiwanda hicho.

"Kiwanda kimeshindwa kufikia malengo ya uzalishaji kutokana na kukwama kufanya ukarabati wa eneo la usindikaji wa nyama kwa hali hiyo, serikali kwa nyakati tofauti imekuwa ikitutaka kufanya ukarabati na hii imekuwa ndio changamoto kubwa kwetu kufikia malengo ya uzalishaji," alisema George.

Aidha, alisema kiwanda hicho, licha ya misukosuko hiyo kwa kipindi cha miaka sita kimewalipa wafugaji wanaouza mazao ya mifugo kiwandani hapo kiasi cha Sh.bilioni 9.3.

Alisema malengo ya kiwanda hicho, kwa sasa ni kuelekeza nguvu katika masoko ya nje ya nchi yakiwamo ya Afrika ya Mashariki na soko la pamoja la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Alisema kiwanda hicho kina wawekezaji 12, akiwamo Halmashauri ya Jiji la Arusha, uwekezaji wake ulitokana na ardhi na ulilidhiwa na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Arusha mwaka 1990, ambapo kiwanda hicho kilijengwa ndani ya ardhi ya halmashauri hiyo.

Alieleza kuwa awali kiwanda hicho, kilikuwa kikifanyakazi na kiwanda cha Arusha Meat, ambacho kwa sasa kinamilikiwa na halmashauri ya Jiji la Arusha, na hapo mwanzo manispaa ilikuwa na umiliki wa asilimia 49, na kiwanda hicho kilikuwa na umiliki wa asilimia 51.

# Changamoto kwa wenye uziwi yatajwa

**Na Godfrey Mushi,** SAME

ENEO la ujengaji wa dhana au kuelewa dhana za kimaisha, dhana mbalimbali, tafsiri ya mambo kwa ujumla wake na namna ya kutawala mazingira ni miongoni mwa changamoto kubwa inayowatesa kwa sasa watu wenye 'uziwi kutoona', imeelezwa.

Ofisa Programu wa Shirika la Sense International Tanzania, Benjamin Kihwele, alisema hayo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu nini kifanyike ili kupata utatuzi wa changamoto hiyo.

Kwa mujibu wa Kihwele, kundi hilo la walemavu linahitaji kuondolewa kwa mikakati mahsusi ndani ya lindi hilo.

"Kuna kazi kubwa sana inahitajika kufanyika. Ingawa tumeanza kufanya hayo katika mikoa ya Kilimanjaro na Dar es Salaam, kimsingi aina hii ya ulemavu inafanya changamoto kubwa sana kwenye eneo la mawasiliano, kushindwa kutoa taarifa au kupokea taarifa kwenye eneo la uhusiano katika jamii kwa maana kwamba watu wanashindwa kuchangamana nao kwa sababu ya kushindwa kuwasiliana.

"Sasa eneo la ujengaji wa dhana au kuelewa dhana za kimaisha, dhana mbalimbali na tafsiri ya mambo kwa ujumla pamoja na mjongeo kwa maana ya kutawala mazingira kwa watu wenye uziwi kutoona, ndilo jambo ambalo linahitaji msukumo mkubwa wa wadau, serikali na hata wahisani," alisema.

Mpaka sasa, watoto 100 wenye ulemavu wa uziwi kutoona wameibuliwa katika mkoa wa Kilimanjaro na wadau hao wa Sense International Tanzania na kuandikishwa katika shule mbalimbali kupata elimu ya msingi.

Watoto hao husaidiwa kupata elimu kwa kutumia dhana ya msaidizi wa mwalimu ambaye amenolewa kitaaluma kuwasaidia walemavu wa aina hiyo kujua mambo mbalimbali.

Akizungumzia mkakati wa serikali na wadau hao wa maendeleo kuwatambua watu wenye ulemavu huo vijijini, Ofisa Elimu wa Elimu Maalum wa Wilaya ya Same, Marietha Shayo, kwa miaka mitatu wamewaibua na kufanya sensa ya kuwatambua kwa kushirikiana na waratibu wa elimu kata.

Alisema katika Wilaya ya Same, tayari wamewatambua watoto 12 katika kata tisa na sasa wanaendelea na masomo.

# Utata waibuka zabuni duka la hospitali

**Na Paul William,** MOSHI

UTATA kuhusu kutimizwa kwa masharti ya zabuni ya upangaji wa duka moja lililoko ndani ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi), umeiweka matatani menejimenti ya hospitali hiyo, huku mgogoro huo ukiacha maswali.

Hali hiyo imejitokeza baada ya mlalamikaji, Sezari Kimario, anayedai kushinda zabuni hiyo kihalali, kupaza sauti akidai kutoridhishwa na kinachoendelea kwa kuwa licha ya kutia saini mkataba wa upangaji na kulipa fedha Sh. milioni moja kama malipo ya awali ya kodi ya pango, hadi sasa hajaonyeshwa duka hilo ukiwa mwaka mmoja umepita.

Kwa mujibu wa Kimario, akiwa mfanyabiashara, alituma maombi ya zabuni (Nipashe imeona nakala yake) kwa ajili ya kuendesha duka hilo Septemba 13, mwaka jana, kama ilivyotangazwa katika zabuni namba MRRH/001/2018/2019/NCS/03 ya mwaka wa fedha wa 2018/19.

Baadaye, Novemba mwaka jana, hospitali hiyo iliingia mkataba wa miezi saba na mfanyabiashara huyo ya kuendesha duka hilo kwa kutakiwa kulipa kodi ya Sh. 250,000 kila mwezi, lakini hadi sasa Kimario ameshindwa kufanya biashara katika duka hilo kutokana na uongozi wa hospitali kushindwa kumkabidhi duka.

"Licha ya kuandika barua mara kwa mara katika Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) wa Kilimanjaro ili kukumbushia kukabidhiwa rasmi duka hilo, mpaka sasa sijapewa na ninafikiria kwenda mahakamani kudai fidia kwa sababu naona ni kama wamevunja mkataba," alisema.

Kipengele cha sita cha mkataba baina ya hospitali hiyo na mfanyabiashara huyo, kinaonya kuwa upande wowote utakaohusika kuvunja mkataba, utalipa hasara ambayo upande mwingine utakuwa umepata.

Aidha, mfanyabiashara huyo hivi sasa anadai kupata hasara ya zaidi ya Sh. milioni 20 kutokana na kununua bidhaa za kuuza katika duka hilo na baadhi yake tayari zimeharibika na zingine kwisha muda wake wa matumizi.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mhandisi Aisha Amour, alipofuatwa kutoa ufafanuzi juu ya hilo, alimtaka mfanyabiashara huyo kuwasiliana na uongozi wa hospitali kuhusiana na fedha alizolipa baada ya kutia saini mkataba huo.

Naye Mganga Mfawidhi Hospitali hiyo, Dk. Japhet Boniface, alisema wao hawakuvunja mkataba huo kama inavyoelezwa na kumtaka mwandishi wa habari hii kumtafuta RAS ambaye ndiye aliyeandika barua kwa mfanyabiashara huyo.

Mkataba huo ulitiwa saini Novemba 23, mwaka jana, ambako upande wa hospitali ulitiwa saini na Dk. Boniface na Katibu wa Hospitali, Richard Kafwila, wakati mzabuni alitia saini na kushuhudiwa na Eusebi Swai.



Kaimu Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara, Amoniche Mtweve, akizungumza na wadau kuhusu ustawi wa watoto wilayani humo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**.

# Wasongamana maabara moja

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari ya Sawe iliyoko Kata ya Masama Mashariki, Hai mkoani Kilimanjaro, wanarundikana katika chumba kimoja cha maabara kujifunza kwa vitendo masomo ya Fizikia, Baiolojia na Kemia.

Hali hiyo inatajwa kuathiri zaidi upatikanaji wa wanafaunzi waliofanya vizuri katika masomo hayo, hivyo kuendelea kuonyesha alama nyekundu juu ya upatikanaji wa wataalamu wa masomo ya sayansi na walimu wa masomo hayo, hasa kipindi hiki cha mabadiliko makubwa ya sayansi na teknolojia na uchumi wa viwanda tunaoutegemea.

Hayo yamo katika taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo, aliyoiwasilisha mbele ya kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro.

Katika taarifa yake, Sintoo alisema: "Kwa sasa serikali inafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba shule hiyo inapata maabara za masomo hayo na kumaliza tatizo hilo."

Upungufu wa maabara za sayansi kwenye shule za sekondari katika baadhi ya mikoa nchini umeendelea kuwa changamoto katika ufaulu wa wanafunzi wa masomo hayo.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) katika mwaka wa fedha 2018/19, serikali ilijenga maabara 165 za masomo ya sayansi katika shule mbalimbali nchini.

Kwa muktadha huo, serikali inataka kila shule inayofundisha masomo ya sayansi kuwa na maabara tatu za masomo ya Fizikia, Kemia na Baiolojia.

Mwaka 2017 kulikuwa na maabara 2,151 katika shule za sekondari nchini, mahitaji yalikuwa 4,797. Hali hii ilionyesha upungufu wa maabara 2,646. Hata hivyo, wilaya 18 kati ya 184 zilizorodheshwa zilikuwa na upungufu uliozidi asilimia 50.



JPM alipotoa 'dozi' nzito mara alipokabidhiwa SADC

Ukurasa 19



UCHUMI

KUJONGEA 'BREXIT BILA MKATABA'...

## Sekta viwanda, fedha zaanza kutafutana

Ukurasa 14

# BUFE

Ijumaa Septemba 6, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



MKURUGENZI KUNAMBI:

# Hivi ndivyo Mradi Uendelezaji Dodoma unavyoliunda upya jiji

Ukurasa 16

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

UCHUMI

**Na Nimi Mweta**

## KUJONGEA 'BREXIT BILA MKATABA'...

# Sekta viwanda, fe zaanza kutafutana

- Paundi yaporomoka; hofu zatawala
- Johnson ahaha, kizingiti 'backstop'

VIWANDA nchini Uingereza vinalalamika kushuka uzalishaji tangu mwaka 2012, tangu kipindi cha kumalizika msukosuko wa sekta ya fedha duniani wa 2008.

Mtazamo ni 'oda' ya bidhaa, kwa maana ya mahitaji ya kutengenezewa bidhaa na kupelekewa kwa wateja, zimeshuka kwa kiwango kikubwa ndani ya miaka saba iliyopita, wataalamu wakitafsiri kupitia msemo:"sekta ya biashara inajisikia vibaya, hadi suala la Brexit litatuliwe."

Sarafu ya Uingereza ambayo kwa kawaida ni zaidi ya Dola ya Marekani kwa kiwango mara moja na nusu, ilishuka kufika wastani wa 1.2 dhidi ya dola, hivi karibuni.

Watalaamu walikuwa wanajiuliza kama hali hiyo ya kukosa imani na shauku ya kuzalisha katika viwanda itadumu au itaanza kupotea baada ya Brexit kulamilika Oktoba 31.

Kuna suala moja katika mchakato mzima wa Brexit linaloendelea kujadiliwa, kati ya Uingereza na Umoja wa Ulaya (EU), ni kinachoitwa 'backstop' ambao ni mpaka wa Ireland ya Kaskazini na Jamhuri ya Ireland kubaki wazi, kwa kiasi kikubwa.

Hilo ni eneo linaloleta wasiwasi mkubwa kwa serikali ya Uingereza na Ulaya, hivyo Ujerumani na Ufaransa zinatafuta njia ya kulitatua.

Kwa mengine yaliyobaki, hakuna kitakachojadiliwa kati ya serikali ya Waziri Mkuu Boris Johnson na EU. Hivyo, uwezekano wa kutoka bila mkataba upo, labda mkataba uliopo uboreshwe kuhusiana na hiyo 'backstop.'

Ukifikiwa muafaka kuhusu mpaka, sehemu ya mzozo wa Brexit utapungua na Waziri Mkuu Johnson, anaweza kupitisha muswada wa sheria kujitoa EU, kama kanuni rasmi, ili mradi aungwe mkono na kundi la Ireland ya Kaskazini.

Hata chama cha kizalendo cha Scotland, nacho kinaweza kuafiki, licha ya kwamba zaidi ya upande wa chama cha Labour, kupinga 'Brexit.'

Inaangaliwa kwamba, maelewano yakipatikana, yatapunguza ugumu wa serikali ya Johnson kuweka mikakati ya kibajeti (ikiwamo bajeti ndogo ya dharura kuelekea mwisho wa mwaka) kutatua mikwamo inayoweza kutokea, Brexit itakapokamilika.

Hata hivyo, bado hakuna uhakika ni wa kiasi cha mkwamo Uingereza au kusitasita uzalishaji viwandani na kuzorota thamani ya fedha, kunakotokana na Brexit, vivyo hivyo, kwa nchi za Ulaya.

Kunatathminiwa kwamba 'kiwingu' cha kupungua ukuaji uchumi kutokana na vita ya kibiashara, kati ya Marekani na China na hata au upungufu wa mauzo nje, kutokana na vikwazo Marekani inavyolazimisha kwa Iran.

Pia, EU imejiwekea vikwazo vya kibiashara dhidi ya Russia, ambayo ilitengwa kutoka kudi la mataifa tajiri duniani maarufu G8, kutokana na uvamizi wa Crimea, eneo la Kaskazini ya Ukraine lenye raia wengi wanaozungumza Kirusi.



Bunge la EU likiendelea.

> **"Inaangaliwa kwamba, maelewano yakipatikana, yatapunguza ugumu wa serikali ya Johnson kuweka mikakati ya kibajeti (ikiwamo bajeti ndogo ya dharura kuelekea mwisho wa mwaka) kutatua mikwamo inayoweza kutokea, Brexit itakapokamilika.**

**Dira soko**

Watafiti wa uchumi, wanasema soko la dunia hivi sasa linajikongoja, huku mahitaji ya bidhaa za viwandani kutoka Ulaya kwenda Marekani na bara la Asia yamepungua.

Uingereza inatajwa kuwa na soko kubwa zaidi la bidhaa za viwanda barani Ulaya, lakini kuna watafiti wanaosema, kujitoa bila mkataba, kutasababisha kero na mkwamo wa bidhaa hizo, kutokana na janga la kodi.

Kuna mchambuzi aliyetumia mfano wa ubashiri, kwamba magari ya mizigo yatapanga foleni kwa siku tatu katika kituo cha Dover Mashariki ya Uingereza, ambako magari hujiandaa kupita katika barabara ya chini ya bahari kuingia Ufaransa. Kwa jumla ni hofu kila kona Ulaya.

Wanunuzi wa jumla wa bidhaa za viwanda, wanaelekeza 'oda' zao kwingineko na siyo Uingereza, wakihofia kupanda kodi Uingereza



James Gordon Brown, mkereketwa wa mada ya Brexit na Waziri Mkuu M

# dha

ikigeuka kuwa 'nchi ya tatu,' isiyo na uhusiano wa moja kwa moja na unafuu wa kodi.

Takwimu za mwezi Agosti zilionyesha uzalishaji viwandani umepungua, pamoja na mauzo ya nje na kupatikana nafasi za kazi.

Wataalamu wameanza kujiuliza kama uchumi unashuka kwa jumla (recession), kama ilivyoanza kuhofiwa nchini Marekani, kutokana na vita ya kibiashara na China.

Kwa upande wa Marekani, wasiwasi uliondoka muda, lakini Uingereza itapata tabu kujinasua.

**Johnson shakani**

Mchambuzi mwandamizi, James Gordon Brown, anaitazama kwa tabu serikali ya Johnson, kutokana na vitisho anavyotoa kuhusu kitakachotokea nchini humo Brexit, bila ya kuwapo mkataba ikitekelezwa.

Ni hofu inayotokana na ukweli, Brown ameshika nyadhifa za juu nchini humo, kwani alikuwa Waziri wa Fedha kati ya mwaka 1997 hadi 2007, halafu waziri mkuu kwa miaka minne.

Kwa vile sakata la uchumi duniani lilianza na mkwamo wa mabenki kadhaa katika soko la fedha nchini Marekani mwaka 2007, ulimkuta ndiyo kwanza anaingia katika uwaziri mkuu na akaondoka mkwamo ukiendelea. Hiyo, inadhaniwa kutawala mawazo



staafu. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson.

yake.

Brown ameibua hofu ya kwamba kutakuwapo uhaba mkubwa wa chakula nchini humo, endapo Brexit bila ya mkataba itafikiwa, akitoa mwito wa kuzuiwa kwa Brexit kabla ya majanga kuifika Uingereza.

Akiongea na wafanyakazi katika kiwanda cha mikate jijini Liverpool, ambako ni kikundi cha ushirika, anasisitiza kuwa umaskini utaongezeka nchini humo, endapo Brexit itatekelezwa kwa hali yake ya sasa.

Brown ni mmoja wanaounga mkono hoja kuwa "mradi Bunge la Uingereza limeshindwa kufikia mkataba wa kujitoa Umoja wa Ulaya, basi isijitoe sasa na ingoje hadi mkataba kama huo ufikiwe." Ni mchakato ambao chama tawala hakiukubali, pia EU.

**Uhaba chakula**

Michael Gove, Waziri wa Johnson anayesimamia matayarisho ya kujitoa bila ya mkataba, anasema baadhi ya bei za vyakula zinaweza kupanda, lakini hapatakuwapo uhaba wa aina 'hiyo au ile' ya bidhaa za vyakula, kama nafaka, maziwa na nyama. Ni mahitaji ambayo sehemu yake inaagizwa kutoka bara Ulaya.

Hata hivyo, alipotakiwa kueleza hitaji la ongezeko la bei, alifafanua kuwa baadhi ya vyakula vitapanda bei na vingine vitashuka bei, kutokana na kupungua kwa kiasi fulani mwingiliano wa soko la Uingereza na Ulaya kwa jumla.

Brown anatahadharisha kuwa umaskini utazidi, kwani wanaosaidia kutoa vyakula nao watakumbwa na uhaba.

Wachuuzi wa vyakula, ambao wanaagiza zaidi kutoka nchi za EU, wanakana kwa kusema hakutakuwapo uhaba wa vyakula EU.

Lakini, msemaji wa kundi lingine la waingizaji wa vyakula ambalo lina mwelekeo wa chama tawala, anasema kuwa haiwezekani kuondoa athari za kuvurugika kiasi fulani kwa mkondo wa uagizaji bidhaa, kwa sababu vyakula kama nyama na mboga, haziwezi kununuliwa kwa wingi na kuhifadhiwa.

Ofisa wa kikundi cha kutengeneza mikate alichotembelea Brown, anasema ameshaona malighafi wanazoagiza kwa ajili ya uzalishaji zimeshapanda bei.

Brown anasema, kujitoa EU bila ya mkataba kutaathiri kwa kiwango kikubwa biashara ya magari au viwanda vya kutengeneza magari nchini humo.

Haya hivyo, wapo wengi wana wasiwasi na anachosema Brown, akidaiwa anaongeza shauku kila kukicha. Mwezi Septemba mwaka jana, alisema 'dunia haina uongozi' akimaanisha kuparaganyika kwa dira ya Marekani katika uchumi wa dunia na utandawazi.

Mtazamo wake ni dunia inajongea, taratibu katika mkasa mkubwa wa uchumi kama ule wa 2008. Alirudia tahadhari ambazo hazikuchukuliwa wakati ule, ambazo baadhi ya wanaompinga wanabeza.

# Kulikoni Siku Wafanyakazi Marekani ni Septemba?

KWA Wamarekani, Siku ya Wafanyakazi kama ilivyo sehemu nyingine nyingi ni ya kitaifa, iliyoanzishwa kuwaenzi wafanyakazi wa Marekani na michango yao katika uchumi,wakisherehekea mwezi Septemba.

Ni tofauti na sehemu nyingi duniani, ikiwamo Tanzania wanakosherekea siku ya Mei Mosi ya kila mwaka.

Wamarekani wengi wanaitumia siku hiyo kuadhimisha kumalizika kwa kipindi cha joto, hapo ndipo inapojenga suala la kustaajabu juu ya chimbuko hilo linalotokana na harakati za wafanyakazi mwishoni mwa mwaka 1800.

Ilikuwa wakati wa mapinduzi ya viwandani yamefikia kileleni, Wamarekani walifanya kazi kwa saa 12 kwa siku, katika siku zote saba kwa wiki ndani ya katika mazingira magumu na malipo duni.

Hata watoto wadogo walikuwa wanafanya kazi viwandani. Karibu kila mwajiri hakutoa likizo ya ugonjwa kwa wafanyakazi, likizo ya kawaida au maslahi ya afya.

Kadri walivyoendelea kujipanga zaidi katika vyama vya wafanyakazi, walianza kwa kuandamana kupinga hali mbaya na hatarishi za maeneo ya kazi na kushawishi maslahi zaidi kutoka kwa waajiri.

Hatua hiyo ya kuwatambua wafanyakazi kwa kuwapa likizo, ilianza kwa serikali za majimbo zikipitisha sheria za kumjali mfanyakazi wa kawaida.

Bunge la Marekani lilianzisha sikukuu ya wafanyakazi kitaifa mnamo Juni 28, 1894, na kuweka Jumatatu ya kwanza ya mwezi Septemba kuwa Siku ya Wafanyakazi.

Tofauti yake na Siku ya Wafanyakazi ya Mei Mosi inaadhimishwa zaidi katika nchi zenye viwanda ulimwenguni.

Mnamo Mei 1886, maandamano ya wafanyakazi yalifanyika katika bustani ya Haymarket iliyoko Chicago, kushinikiza kazi zifanywe kwa saa nane.

Bomu lililipuka katika maandamano hayo na kumuua ofisa wa polisi na raia wanne. Ni tukio lililofanya habari hiyo kuvuma duniani kote na maadhimisho ya kila mwaka ya maandamano ya wafanyakazi, duniani.

Kwa nini hawaadhimishi Mei Mosi? Upinzani mkubwa dhidi ya harakati za umoja wa wafanyakazi uliibuka nchini Marekani.

Baada ya miaka kadhaa, Mei Mosi ikawa inanasibishwa na siasa za mlengo wa kushoto, wakati Siku ya Wafanyakazi, ilikuja kuongezeka kutambuliwa na manispaa na majimbo.

Wakati Marekani ilidhamiria kuanzisha sikukuu ya kitaifa ya wafanyakazi, Rais wake Grover Cleveland, hakutaka kuchagua siku ya tarehe halisi ya Mei Mosi, kwa sababu ya kuhusishwa siku hiyo na mlipuko wa bomu huko Haymaker, badala yake akachagua mbadala wa Septemba.

• **Kwa mujibu wa Mtandao.**




Wamarekani wakisherehekea Sikukuu ya Wafanyakazi. **PICHA: MTANDAO**

UCHUMI

MKURUGENZI KUNAMBI:

# Hivi ndivyo Mradi Uendelezaji Dodoma unavyoliunda upya jiji

- Kituoni: Nafasi VIP, mabasi 250, abiria 3,000
- Egesho malori 500; taa kona zote; soko kubwa
- Mapumziko Chinagali 'yamkosha' Majaliwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

TANGU serikali ianze kuhamishia shughuli zake jijini Dodoma miaka minne iliyopita, kumekuwapo utekelezaji wa miradi mbalimbali mikubwa,

Ni utekezaji na mpango ulioridhiwa mwaka 1975, makao makuu ya nchi na kinachofanyika sasa ni kuwezesha jiji hilo liendane na hadhi yake.

Majiji mengine nchini ni Mbeya, Arusha, Tanga, Mwanza, Dar es Salaam, sasa Dodoma inatekeleza Mradi wa Uendelezaji Miji Mkakati(TSCP), ambayo imepewa kipaumbele katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali, kutokana na hadhi hiyo.

Miradi wa ujenzi wa kituo kikubwa cha kisasa cha Mabasi yaendayo mkoani, chenye hadhi sawa na uwanja wa ndege.

Ujenzi wa soko kuu la Dodoma kwenye eneo la Nzuguni, pamoja na eneo la mapumziko maarufu kama Chinangali Park, ambayo ujenzi wa miradi hiyo unafanywa kwa mkataba wa ujenzi wa Sh. bilioni 35.4.

**Mratibu TSCP**

Ujenzi wa miundombinu hiyo, mratibu wa miradi hiyo, Mhandisi Emmanuel Manyanga, anasema jiji hilo limepewa kipaumbele kwenye miradi hiyo, pamoja na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, ili kulifanya liwe la kuvutia.

Anasema, kituo cha mabasi kina uwezo wa kuegesha mabasi 250 kwa wakati mmoja, huduma mbalimbali za ndani na eneo la kupumzikia abiria zaidi ya 3,000.

Pia, anasema eneo hilo ni la ghorofa hivyo yamewekwa maeneo ya biashara kama maduka, huduma za vyakula, eneo la wafanyabiashara ndogo, vyumba kwa ajili ya kukatia tiketi.

"Pia tumeweka 'VIP lounge' (abiria wenye hadhi maalum) kwa ajili ya huduma mbalimbali, pia tutaongeza majengo kwa ajili ya kupata huduma ya malazi kwa abiria wa mikoani,"anasema.

Manyaga anasema, kituo hicho kitakuwa na eneo la malazi kwa ajili ya abiria kwa gharama nafuu na itaendeshwa huduma hiyo na halmashauri ya jiji hilo.

"Hii ni stendi kubwa na nzuri hadhi yake ya kimataifa maana ni stendi kubwa kwa Afrika Mashariki, itatoa huduma za kimataifa," anasema.

Mtaalamu huyo anasema, usanifu wa kituo hicho wameuchukua kutoka nchi mbalimbali, ikiwamo Dubai na Afrika Kusini.

"Tumeangalia stendi za mikoa mingine tukaona upungufu tukajiongeza hadi kuwawekea vizimba wafanyabiashara," anasema.

Anaongeza kuwa "Usanifu wa jengo letu umekaa kwa muundo wa ndege mtu akiingia Dodoma akiangalia anaona kama ndege inataka kupaa kumbe ni jengo la stendi yetu."

Akizungumzia eneo la kupumzikia la Chinangali Park, mtaalam huyo anasema katika eneo hilo kutakuwa na viwanja vya michezo mbalimbali ya wakubwa na watoto.



Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi. **PICHA ZOTE: AGUSTA NJOJI.**

Kuhusu soko, anasema litakuwa jengo la ghorofa moja na wafanyabiashara zaidi ya 500 wanaweza kufanya biashara zao humo.

**Mkurugenzi Jiji**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji Dodoma, Godwin Kunambi, anasema wanatekeleza miradi hiyo, kwa ufadhili wa serikali kupitia mkopo wa Benki ya Dunia.

Anasema mradi TSCP unahusisha ujenzi wa miundombinu ya barabara katika maeneo ya Kikuyu, Chidachi, Kinyambwa, Itega, Njedengwa, Mapinduzi, Ilazo, Ipagala, Chamwino, Kilimani, Majengo, Mlezi pamoja na maingilio na Kituo cha mabasi na soko kuu.

Mkurugenzi huyo anasema, barabara hizo zinajengwa kwa kiwango cha lami, pia zitawekwa taa barabarani takriban 925 zinazotumia mfumo wa umeme wa jua.

Pia mradi huo unahusisha kituo cha maegesho ya malori makubwa utakuwa na uwezo wa kuwezesha takribani 300 katika eneo la Nala.

Anaongeza kuwa mbali na kituo kikuu cha mabasi na soko kuu, pia kuna ujenzi wa vituo sita vya watembea kwa miguu; vizimba saba vya kukusanya taka ngumu; uboreshaji mandhari ya eneo la kupumzika katika eneo la Chinangali.

Jingine analolitaja Kunambo ni ujenzi wa mtaro wa maji ya mvua wenye urefu wa kilomita 6.5 katika eneo la Ipagala .

Kwa mujibu wa Kunambi, Jiji la Dodoma limepata miradi ambayo inagharimu takribani Sh. bilioni na anafafanua: "Kupitia miradi hii Jiji la Dodoma linaenda kutekeleza azma yake ya maandalizi ya kujitegemea kupitia mapato yake ya ndani, Sh.Bilioni 20 zitapatikana kutoka kituo cha mabasi, soko, maegesho ya malori."



Dampo la Chidaye, ambalo limeanza kutumika.

> "Hatuwezi kuwa tumejaza nyumba kila eneo, watu hawana mahali pa kupumzika na kukutana na marafiki zao. 'Plan' (mpango) ya Chinangali Park ni nzuri. Jiji la Dar es Salaam 'plan ya awali kulikuwa na maeneo ya ma-



Ujenzi wa soko la kisasa.

Kunambi anasema kwa sasa wanategemea mapato kwenye uuzaji viwanja, lakini miradi hiyo ndio mbadala wa mapato ya ndani.

"Kupitia miradi hii tunashukuru serikali kwa kutupatia fedha kwa ajili ya miradi hii, na itasaidia jiji kuwekeza kwenye vyanzo vingine,"anasema Kunambi.

**Mweka Hazina**

Mweka Hazina wa Jiji la Dodoma, Alfred Mlowe, anasema mradi wa TSCP katika mfumo wa ukusanyaji mapato, zimenunuliwa mashine za kusaidia kukusanya 211, ambazo zimeziba mianya ya upotevu wa mapato.

"Kwa miaka mitatu 2016/17 zilikusanywa Sh. bilioni 4.7, mwaka 2017/18 na jiji lilikusanya Sh. bilioni 24.7 na mwaka 2018/19, limekusanya Sh. bilioni 71 sawa na asilimia 105. Hivyo, utaona mchango wa TSCP ni mkubwa sana."

Mlowe anasema, vitega uchumi vilivyojengwa kupitia mradi wa TSCP vinatarajiwa kupaisha mapato zaidi kwa mwaka wa fedha 2019/20, kwamba zitapatikana Sh. bilioni tisa, kwa kipindi cha miezi sita na baada ya mwaka mmoja vitaloingizia jiji la Dodoma, zaidi ya Sh. blioni 20.

Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Profesa Davis Mwamfupe, anatoa wito kwa wananchi kutumia fursa zilizopo kwenye miradi na kuilinda.

"Baada ya Dodoma kutangazwa kuwa makao makuu, mahitaji ni makubwa na kwa bajeti ya jiji, tusingeweza kutekeleza miradi kwa kiasi hiki. Kwa kuwa serikali imechukua jukumu hili, naishukuru sana serikali," anasema.

**Waziri Mkuu**

Mwishoni mwa mwaka jana, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alitembelea Mradi wa Uendelezaji wa Miji ya Kimkakati katika jiji la Dodoma na alikagua ujenzi wa maegesho ya malori makubwa katika eneo la Nala na uboreshwaji mandhari ya eneo la kupumzikia la Chinangali.

Katika hilo, alimuagiza Mkurugenzi wa Jiji, Kunambi, aendelee kutenga maeneo ya mapumziko, ili wananchi wapate sehemu za kukutana, baada ya kumaliza kufanya kazi.

Waziri Mkuu anaupongeza uongozi wa jiji Dodoma kwa kubuni wazo hilo na anahimiza umuhimu kwa miji mikubwa kutenga maeneo kwa ajili ya mapumziko na yatumike kwa madhumuni yaloyopangwa .

"Hatuwezi kuwa tumejaza nyumba kila eneo, watu hawana mahali pa kupumzika na kukutana na marafiki zao. 'Plan' (mpango) ya Chinangali Park ni nzuri. Jiji la Dar es Salaam 'plan ya awali kulikuwa na maeneo ya mapumziko, lakini watu wa Idara ya Ardhi waliyauza," anasema Majaliwa.

## BIASHARA KATIKA PICHA



Mchuuzi wa mastafeli akisaka wateja katika Mtaa wa Samora, katikati ya Jiji la Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**




Mkurugenzi wa Uhusiano wa kampuni ya Said Bakhresa Group, Hussein Sufian (kushoto) na Mkurugenzi wa Masoko wa kampuni hiyo, Ahmed Jaruan, wakionyesha muonekano mpya wa vifungashio vya unga wa ngano wa Azam ujulikanao kama Ngano Bora, kwa waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, ikiwa ni mkakati wa kulinda ubora na kutambulisha bidhaa zake kwa wateja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mchuuzi wa ndizi za kuchoma na mishkaki akiwa amepaki na kufanya biashara yake barabarani katika Mtaa wa Zanaki, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

UCHUMI

# KILIO MWANGA;

# Ndege walivyoteketeza ekari za mtama, alizeti na ufuta shamba

## • Pata dodoso la mtama unavyokomboa njaa

**Na James Lanka, aliyekuwa Mwanga.**

HIVI karibuni taarifa ya hali ya uzalishaji na upatikanaji mazao ya chakula nchini, inaonyesha hali imeendelea kuwa nzuri katika miaka kadhaa, kujitosheleza kwa mahitaji.

Kimsingi, tathmini ya hali ya chakula, uzalishaji wa mazao ya chakula na usalama wake, unaangaliwa katika baadhi ya mazao muhimu yanayohitajika zaidi, kama vile mahindi, mtama, ulezi, mchele, jamii ya kunde, ngano, ndizi, muhogo na viazi.

Katika kipindi hicho, nchini kumekuwapo na kiwango toshelevu kinachovuka mahitaji. Ni mafanikio yanayotajwa kutokana na sababu mbalimbali.

Hiyo inajumuisha, hali nzuri ya hewa, usimamizi na utekelezaji mzuri wa sera na mikakati mbalimbali ya kiserikali na wadau wengine wa masuala ya kilimo ili kuongeza tija na uzalishaji.

Wizara ya Kilimo mwezi Mei hadi Juni maka huu, ilifanya tathmini ya hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa mwaka 2018/2019 na upatikanaji wa chakula kwa kipindi kilichopo cha mwaka 2019/2020 katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kwa lengo la kubaini kiwango cha uzalishaji na mahitaji.

### Zao Mtama

Inajulikana, chakula kikuu kwa jamii nchini ni ugali, hasa utokanao na zao la mahindi, inayozalishwa kwa wingi katika maeneo mengi nchini.

Kwa mantiki hiyo, iwapo kutakuwapo upungufu wa zao hilo halitazalishwa kwa wingi, basi taifa linaweza kuingia katika baa la njaa. Mtama unaingia katika suluhisho la tatizo hilo, kutokana na kuhimili ukame.

Mtama inaangukia katika kundi la mbegu, punje ndogo katika jamii ya nafaka, ambayo ina kiasi kikubwa cha kabohaidreti.

Zao hilo kimazingira hilo lina uwezo mkubwa kuvumilia hali ya ukame kuliko mengine ya jamii yake, hali inayoifanya kulimwa katika maeneo mengi duniani, hata penye uhaba wa mvua.

Unga wa mtama hutumika kuandaa ugali, kuoka mikate, kupika ubwabwa na unaweza kuchemshwa na kuliwa.

Viwanda vya bia, navyo hutumia mtama kuwa malighafi kuu, majani na mabua yake yanaweza kutumika kama chakula cha mifugo. Pia, mabua makavu yanatumika kujengea mabanda ya mifugo na makazi.

Zipo aina za mtama na mbegu zake. Hizo hutofautiana, kulingana na rangi zake; nyekundu, kahawia, nyeupe zinazojumuisha aina zaidi ya 20 duniani.

Mtama una aina zake. Zipo chachu, hasa mbegu za kahawia na nyekundu, mtamu; hasa rangi nyeupe na wakulima wengi hupendelea kuilima.

Mbegu za kisasa za mtama ni laini kuliko mbegu za asili ambazo unakuwa 'mtama mgumu' au 'mtama wa asili.'

Hizo zina mbegu ndefu kwenda juu na huchukua muda mrefu kupanda hadi kuvuna, kuliko mtama wa kisasa, ambao ni mfupi na huchukua muda mfupi, huku ikitoa mavuno bora zaidi, kuliko ya asili.

Kwa kawaida, mtama ukilimwa vizuri, unatoa wastani wa tani moja hadi mbili na nusu kwa shamba la ekari moja .

Pamoja na uhaba wa mvua za mwaka huu, lakini mtama umo katika mavuno bora.

### Ndege wa mtama

Hivi karibuni makundi ya ndege aina ya Kweleakwelea yalivamia mashamba ya mtama, ufuta na alizeti wilayani Mwanga Mkoa wa Kilimanjaro na kuteketeza ekari zaidi ya 40 za mazao hayo na kusababisha hasara kubwa.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wakazi eneo la Kitopeni katika Kata ya Kifaru wilayani Mwanga, mkoani Kilimanjaro.

Wanasema makundi hayo ya ndege yalianza kuvamia mashamba mwishoni mwa mwezi Juni iliyopita na mavuno yakiwa yamemea vizuri.

Mkulima wa mtama, Kuria Msuya, anasema ndege hao wamewaletea uharibifu mkubwa, pia hofu ya kuwapo balaa la njaa, badaa ya wakulima hao kukosa mavuno waliyoyategemea.

> **"Ni kuanzia kulima shamba, kuotesha, palizi, ilitumia zaidi ya Sh. milioni tatu katika kuitikia wito huo wa serikali, lakini zote zimeishia chini kufuatia uharibifu uliofanywa na ndege hao."**

"Ndege hawa wameharibu mazao yote. Mimi mwenyewe nimelima ekari sita za mtama, nao umeliwa wote. Sikuvuna hata punje moja. Nitoe rai kwa serikali kuingilia kati," anafafanua Msuya.

Anasema, serikali imekuwa ikihamasisha walime mtama kwa vile linakabiliana na ukame na binafsi kama walivyo wenzake wamelima.

Msuya anasema, amelima ekari sita za zao hilo, lakini ndege aina ya kweleakwelea walivamia shamba lake na kula mtama wote, jambo analosema limenyima mavuno.

Anasimulia:"Kutokana na makundi ya hawa ndege, sijaweza hata kupata punje moja ya mtama kwa msimu huu nililima ekari sita za mtama.

"Ni kuanzia kulima shamba, kuotesha, palizi, ilitumia zaidi ya Sh. milioni tatu katika kuitikia wito huo wa serikali, lakini zote zimeishia chini kufuatia uharibifu uliofanywa na ndege hao."

Msuya, ambaye ni Diwani wa Kata ya Kileo, anafafanua kwamba ni jambo linalowahatarisha kukata tamaa na vyema serikali kuwasaidia kukabili athari hiyo.

Mkulima mwingine wa eneo hilo, Mohammed Rashid, aliyelima ekari 20 za ufuta, lakini hakuweza kuvuna chochote kutokana na mazao yake kuliwa na wavamizi kweleakwelea.

"Ndege hawa wana akili sana. Licha ya kuweka vijana kwa ajili ya kulinda, bado ndege hawa walivamia mashamba na kula mazao haya," anasema.

Anafafanua kuwa, ndege hao hutokea upande wa safu ya milima ya Usambara na kuvamia mashamba yao, pamoja na kuweka vijana kulinda mashamba hayo, bado ndege wanavamia na kumaliza mazao yao yote.

Selemani Mfinanga, mkulima wa ekari 10 za alizeti, analalamika kwamba hali ni tete kwa wakulima wa mazao hayo, ambao kweleakwelea wameshambulia mazao yao.

### DC Mwanga

Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Thomas Apson, anakiri changamoto hiyo na kuongeza kwamba, mbali na suala hilo, zipo kero kadhaa za wakulima na wafugaji.

Apson anaahidi kuzifanyia kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa kilimo na ufugaji katika wilaya hiyo, ili kuziondoa haraka iwezekanavyo.



Mkulima Salum Rashid, akionyesha shamba lake la mtama, lililoharibiwa vibaya na ndege wilayani Mwanga.
PICHA: JAMES LANKA

UCHUMI

Na Beatrice Moses



Rais Dk. John Magufuli akisalimiana na Dk.Stergomena Laurance Tax. **PICHA: MTANDAO.**

# JPM alipotoa 'dozi' nzito mara alipokabidhiwa SADC

## • Aanika uchochoro wanakokwama
## • Sekretarieti SADC ijitathmini upya

MWAKA 2015 wakati wa kampeni akiwa mgombea wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk John Magufuli, akiwa miongoni mwa wagombea, moja ya vionjo alivyotumia ni kunongesha kampeni ilikuwa ni kupiga 'push up' na ngoma.

Kwa wana - mazoezi wanataambua maana ya 'push up.' Ina mchango mkubwa katika kujiweka sawa kiafya na misuli ya mwili, usiwe mlegevu.

Alipotangazwa mshindi na kuapishwa, akaja na kaulimbiu isemayo 'hapa kazi tu' ambayo pia ni usemi unaopatikana sana katika nyimbo za mazoezini (...kuruta nyama, aah! hapa kazi tu!...), hivyo hivyo 'push up.'

Kauli hiyo ya Dk. Magufuli maarufu kama JPM, ilinogeshwa na 'push up' alizotumia, ikibeba tafsiri kwamba mchapa kazi, ni lazima awe shupavu kimwili na kiakili na akiwa mlegevu anaharibu kazi.

Rais Dk. Magufuli hakusita kuwaondoa kwenye nafasi za uongozi viongozi kadhaa, aliowahisi au kubaini kuwa wanafanya kazi kwa ulegevu tofauti na mwongozo wake na msimamo wake tangu kampeni za urais.

**Aliokabidiwa SADC**

Ilikuwa tarehe 17 ya mwezi uliopita, ndio Rais Dk. Magufuli alikabidhiwa uenyekiti wa Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kutoka kwa Rais wa Namibia, Dk. Hage Geingob, aliyetumikia wadhifa huo kwa mwaka mmoja, kama ilivyo kanuni ya chombo hicho.

Wakati anapokaribishwa kuzungumza mbele ya wakuu wa nchi na viongozi wa serikali kutoka nchi 16 za jumuiya hiyo, Rais Dk. Magufuli, kamwe hakuficha hisia zake za maumivu juu ya namna nchi wanachama wa SADC zilivyoshindwa kufikia malengo ya ukuaji uchumi.

Wakati malengo yalikuwa asilimia saba, ambayo na Tanzania ilifanikiwa kufikia, baadhi ziliambulia asilimia tatu pekee.

Kutokana na hali hiyo, Rais Dk. Magufuli alieleza haja ya kuimarisha Sera za Uchumi na Fedha kwa nchi wanachama, ili kufanikisha malengo iliyojiwekea.

Akitumia rungu la uanachama na uenyekiti wake, aliiagiza Sekretarieti ya SADC kujitathmini, kwani bado haijaonyesha mchango wake kuwa na mwongozo mzuri unaozisaidia nchi wanachama, kufikia hatua za mafanikio kiuchumi.

"Hakuna sababu ya kuficha bado sekretarieti ya SADC haijanifurahisha, takwimu za kiuchumi zimekuwa zikishuka siku hadi siku na sekretarieti haina msaada unaotosha. Hii ni changamoto kwenu ninyi na mjitathimini," Rais Dk.Magufuli alitamka katika mkutano huo.

Ni kauli iliyopokewa kwa shangwe na wajumbe wengi waliohudhuria mkutano huo, unaofanyika mara moja kila mwaka katika nchi inayopangwa kuwa mwenyeji.

Sekrtetarieti hiyo, inaongozwa na Katibu Mkuu wa SADC, Dk.Stergomena Laurance Tax, Mtanzania, aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Wizara, ambaye katika hatua nyingine ya hotuba, alimtangaza mwanamke wa Kitanazania mahiri.

Awali, alipofungua Maonyesho ya Viwanda Kwa Nchi za SADC, ikiwa ni hatua ya utangulizi ya mkutano wa wakuu wa nchi, Rais Dk. Magufuli, alibainisha viwanda ni eneo muhimu la uwekeazaji katika ukuzaji uchumi, kwa kuwa ndiyo inayoongeza ajira na kutokomeza umasikini.

Dk. Magufuli anasema, historia kutoka mataifa yaliyoendelea, unaonyesha ni lazima kupitia mapinduzi ya viwanda, ili kufanikiwa katika uchumi, badala ya kuwa mwagizaji bidhaa, nchi inapokuwa mzalishaji na muuzaji, inaweka ushindani wa kibiashara sokoni.

"Mchango wa sekta ya viwanda katika nchi za Afrika na SADC bado ni mdogo sana. Sekta hii inachangia wastani wa asilimia 10 ya pato la taifa na katika jumuiya ya SADC, inachangia asilimia 11 pekee," anasema.

Rai ya Dk. Magufuli ni kwa SADC ijikite katika kukuza na kuendelela ubunifu, ikiwamo kuendeleza teknolojia rahisi ya viwanda, kuwaendeleza vijana na viwanda vidogo.

"Ukosefu wa viwanda unaifanya Afrika iendelee kuwa na uchumi tegemezi. Hivyo, kubaki katika mduara wa umaskini, hii ndio gharama ya kutokuwa na viwanda. Vijana wanageuzwa kuwa rasilimali watu kwa nchi za Ulaya ,"anasema.

> "Mchango wa sekta ya viwanda katika nchi za Afrika na SADC bado ni mdogo sana. Sekta hii inachangia wastani wa asilimia 10 ya pato la taifa na katika jumuiya ya SADC, inachangia asilimia 11 pekee," anasema.

Nini kifanyike? Dk. Magufuli, anayejulikana sio wa 'kummunya maneno' anataka kushughulikiwa vikwazo vinavyochelewesha maendeleo ya sekta ya viwanda ndani ya SADC na Afrika kwa jumla.

Akiwa mzoefu wa muda mrefu kuongoza Wizara ya Ujenzi, anataja maeneo kama uboreshaji miundombinu kupitia kujenga wa barabara zinazounganisha nchi hizo, kwamba yanarahisisha usafirishaji bidhaa wanazozalisha.

"Ndani ya nchi za SADC kuna fursa nyingi za uwekezaji wa viwanda, ikiwamo madini, kilimo, uvuvi, ufugaji, hivyo tuchangamkie soko hili," anasema.

Pia, aliiitahadhartisha Sekretarieti ya SADC kujitathmini, akipiga marufuku matumzi ya bajeti kwa semina na kongamano, badala yake ijikite katika maendeleo zaidi.

**Dk. Tax anena**

Katika maelezo yake kwa wana - SADC walioudhuria mkutano huo Dk Tax, anabainisha nchi zote zimekuwa zikifanya jitihada kufikia kiwango uchumi cha asilimia saba na hadi sasa, Tanzania pekee ndio imefikia kigezo hicho. Anataja njia ya mafanikio ni kuwa na uchumi mpana.

Anashauri, viongozi wa nchi za SADC wanajipanga upya kupata ufumbuzi wa pamoja, ikiwamo kuzingatia taratibu za mtangamano (integration) zilizowekwa.

"SADC ilikuwa imejipangia kuwa na uchumi wa zaidi ya asilimia saba lakini nchi nyingi zimefikia asilimia 3.1, hiyo ikiwa chini ya asilimia ya Umoja wa Afika(AU) iliyofikia asilimia tatu," anasema.

Dk. Tax anataja sababu inayodidimiza SADC, ni kasi yake ya ukuaji uchumi, Afrika Mashariki iko katika wastani wa asilimia 5.7; Afrika Kaskazini, asilimia 4.8; na Afrika Magharibi asilimia 3.3.

Mwenyekiti msatafu

Mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Rais Geingob, alibainisha umuhimu wa nchi za SADC kuwashirikisha vijana kuleta maendeleo ya kila nchi.

"Kwa kutambua robo tatu ya wananchi wao ni vijana, hakuna sababu ya vijana kwenda nchi za Ulaya kwa ajili ya kutafuta ajira, wakati rasilimali tunazo," anasema Rais Geingob.

Anashauri ni vyema SADC kuwa na mikakati madhubuti itakayofanikisha vijana kupata nafasi ya kushiriki katika masuala ya uchumi kwa hatua, hivyo kuchochea maendeleo kwa nchi za jumuiya hiyo.

**Baraza Biashara**

Mwenyekiti wa Baraza la Biashara nchi za SADC, Charity Mwiya, kutoka Namibia, anasema ni muhimu kuwawekea mazingira wezeshi wanawake kibiashara, katika kufikia malengo ya kukuza uchumi kwa nchi za SADC.

"Wanawake wengi ndiyo wapo kwenye biashara na ujasiriamali, hivyo mazingira wezeshi yanafaa kuwekwa ili nchi hizo zifikie malengo.hatuwezi kuzungumzia biashara bila kumtaja mwanamke," anasema Mwiya.

UCHUMI

## UTEKELEZAJI AGIZO LA SADC

# Sido Dodoma imemuacha 'hoi' Naibu Waziri Stella Manyanya

**Na Renatha Msungu, Dodoma**

BAADA ya mkutano wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kumalizika hivi karibuni jijini Dar es Salaam, serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, ilitoa maagizo kwa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo nchini (Sido), kusimamia uanzishwaji viwanda vidogo mbalimbali kwa ajili ya kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa, ambavyo baadae vitazaa viwanda kikubwa.

Katika moja ya makubaliano ya pamoja ya viongozi wa nchi hizo, ni ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa nchini, utakaosaidia nchi hizo kujikwamua dhidi ya umaskini.

Huo ni mtazamo wa pamoja wa viongozi wa nchi hizo ambao umelenga zaidi katika uongezaji thamani ya bidhaa ambazo huzalishwa kutokana na nchi husika.

Kutokana na hilo, wizara husika ya viwanda, ilikuja na mkakati wa kutengeneza maeneo katika mikoa mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogo, vitakavyosaidia uongezaji thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini.

Hiyo iliifanya wizara husika ya viwanda, kuamua kushirikiana na Sido kwa kuipa kazi ya uanzishaji na usimamizi wa kazi hiyo, kwa sababu ni shirika kongwe (tangu mwaka 1972) katika utoaji mafunzo ya ujasiriamali, ikiwamo uchakataji mazao yazalishwayo nchini.

Pia, hiyo inafanywa kuwa sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali inayolenga kufikia Uchumi wa Kati ifikapo mwaka 2025.

**NAIBU WAZIRI**

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Injinia Stella Manyanya, katika ziara ya kutembelea utendaji kazi wa shirika hilo jijini Dodoma amesema Sido Dodoma na kukagua utekelezaji wa agizo lililotolewa na wizara baada ya mkutano wa SADC, aliiambia kuwa ina kila sababu ya kupongezwa.

Anasema, waliyoyafanya katika ujenzi wa majengo hayo ni kituo cha kufundisha uongezaji thamani ya bidhaa za ngozi, ambacho kinawasaidia wajasiriamali wengi wanaokuja kupata mafunzo ya utengenezaji bidhaa za ngozi.

Stella anasema hiyo inaonyesha jitihada kubwa inayoitia moyo serikali kupitia wizara husika. Anasema: "Naomba niwapongeze sana, mnatakiwa muendelee hivi hivi, Dodoma ni makao makuu kila kitu kinatakiwa kuwa safi mbele ya jamii."

Anasema kuwa lengo lao ni kuona Sido mikoani zinafanikisha kutekeleza azma ya usimamizi wa uanzishwaji wa viwanda vidogo, kwa sababu wao ni wakongwe na wanaelewa nini wanatakiwa kukifanya.

Injinia Stella, anasema kutokana na hilo, wizara imeamua kuitumia Sido kama wasimamizi na Dodoma mmeonyesha mfano mzuri kwa hiki mlichokifanya ndani ya muda mfupi kina manufaa kwa wajasiriamali na taifa kwa ujumla.

Naibu Waziri anasema kuwa, mkoani Mtwara nako imefanya makubwa katika kiwanda cha kubangulia korosho, kama ilivyo kwa manyara, Kigoma, Chato, Bukoba Simiyu na Ruvuma, lengo ni kitaka kila mkoa wajasiriamali wake wawe sehemu ya kuongeza thamani ya bidhaa.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, alipokagua shughuli za Sido, Dodoma. **PICHA RENATHA MSUNGU.**

> **"Wajasiriamali tumekuwa kwa kiasi kikubwa sana tunahitaji Sido iongeze kiasi cha utoaji mikopo lakini pia serikali iongeze fungu kwa Sido ili nao watoe mikopo inayostahili kwa wajasiriamali," anasema Asela.**

**SIDO DODOMA**

Meneja wa Sido jijini Dodoma, Sempeho Manongi, anasema lengo la kuanzisha kituo hicho, wanahitaji kukifanya kiunagnishe vituo vyote katika utengenezaji bidhaa za ngozi na kuwaongezea ujuzi wajasiriamali ambao tayari wameshapata mafunzo ya kutengeneza bidhaa hizo.

Manongi anasema, wanafanya hivyo kwa sababu Dodoma hivi sasa ni jiji na inaendelea kuwa na ongezeko la watu, hivyo wajasiriamali wanapaswa kuzalisha bidhaa bora ambazo zitapata soko kirahisi.

Anasema, Sido Dodoma imejipanga kuhakikisha wajasiriamali wa jiji wanashiriki katika maonyesho makubwa ya kimataifa na bidhaa zao zitoe ushindani hasa ukizingatia wanapata mafunzo ya kila mara, kutoka kwa wakufunzi wa kituo chao

"Vijana wakike kwa kiume jitokezeni kwa wingi kwa ajili ya kupata mafunzo ya utengenezaji bidhaa za ngozi hususani kutumia mashine mpya ya kuboresha bidhaa," amesema Manongi.

Meneja Manongi anasema, wameandaa majengo makubwa kwa ajili ya kulea wajasiriamali wenye malengo ya haraka ya kupiga hatua dhidi ya ujasiriamali wanaofanya jambo ambalo watawasaidia usindikaji wa vyakula kwa wakulima na wafugaji wa jiji la Dodoma.

Anafafanua zaidi majengo hayo yanauwezo wa kuweka wajasiriamali 32 kila moja, ambayo watakuwa wakifanya biashara kupitia bidhaa mbalimbali za kilimo na ufugaji, yatakayowasaidia wakulima na wafugaji kusindika vyakula.

"Kwa kweli tumejipanga kuhakikisha tunasonga mbele, wizara ituangalie kwa jicho la karibu ili tuweze kufikia malengo tuliojiweka," anasema Manongi.

Anafafanua juhudi za Sido Dodoma kwa kushirikiana na wadau wa kawaida, wamesaidia kwa kiasi kikubwa kuleta mashine ambazo hutumika kwa ajili ya kufundisha wajasiriamali.

Manongi anasema, baada ya maagizo kutoka wizara husika, walianza mchakato kwa usaidizi wa serikali pamoja na wadau mbalimbali ambao wanasaidia kuhakikisha inafikia malengo yake.

**WAJASIRIAMALI**

Wajasiriamali kwa nyakati tofauti wanasema moja ya vitu Sido imepiga hatua ni kuwaboreshea majengo wajasiriamali kwa ajili kufanyia biashara zao mbalimbali hapa jijini.

Mjasiriamali Mzee Njau, anasema juhudi za Sido zinapaswa kuungwa mkono na serikali hasa ukizingatia tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda.

Anafafanua kwamba, kutokana na uboreshaji huo wanaomba kiwango cha mikopo kinachotolewa kiongezwe kwa sababu wamekuwa hivi sasa na juhudi za shirika hilo zinaonekana kwa sababu zimesaidia waja wengi kuinuka kiuchumi.

Asela Mkisi, naye anasema wajasiriamali hivi sasa wamekuwa kwa kiasi kikubwa, kwa hiyo kiwango cha mtaji wanachokopeshwa kikue.

"Wajasiriamali tumekuwa kwa kiasi kikubwa sana tunahitaji Sido iongeze kiasi cha utoaji mikopo lakini pia serikali iongeze fungu kwa Sido ili nao watoe mikopo inayostahili kwa wajasiriamali," anasema Asela.

Meneja Manongi anasema, wamejipanga kufanya centa ya uboreshaji bidhaa za ngozi katika cents ya Dodoma nakuwa ya mfano katika mikoa mingine.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, anawasisitiza wajasiriamali wanaochukua mikopo, wairejeshe kwa wakati ili wengine nao wakope ili kuendeleza biashara wanazofanya.

# Chalamila aipa changamoto Mbeya- WSSA

**Na Nebart Msokwa**, MBEYA

MAMLAKA ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mkoa wa Mbeya, (Mbeya-WSSA) imetakiwa kushughulikia haraka changamoto ya miundombinu ya majitaka inayofumuka na kusababisha adha kwa wananchi.

Changamoto hiyo imeelezwa kuwa ni kubwa katika Kata za Mbalizi Road na Mabatini jijini Mbeya, ambako inadaiwa kuwa miundombinu imekuwa ikifumuka na kusababisha majitaka yaliyochanganyika na vinyesi kutapakaa kwenye makazi ya watu na barabarani.

Akizungumza wakati wa mikutano ya kusikiliza kero za wananchi na kueleza mambo mbalimbali yaliyofanywa na serikali, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliitaka mamlaka hiyo kuhakikisha inashughulikia changamoto hiyo mapema kabla wananchi hawajaathirika.

Alisema maji hayo ni hatari kwa afya za wananchi kwa maelezo kuwa yanaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko kikiwamo kipindupindu na kwamba hata harufu ya maji hayo ni mbaya na inaleta kero kwa wananchi wa maeneo hayo.

Alisema kwenye mikutano yake wananchi walilalamika wakidai kuwa wamekuwa wakitoa taarifa za matatizo hayo kwa mamlaka hiyo, lakini hatua hazichukuliwi kwa muda mwafaka.

"Wananchi wanapotoa taarifa mnatakiwa muwe wepesi wa kushtuka na kuwahi eneo la tukio, msisubiri walalamike kwetu tunapokuja kwenye mikutano kama hii, hii inasababisha hata uhusiano kuwa mbovu," alisema Chalamila.

Diwani wa Mbalizi Road, Adam Simbaya alisema kwenye kata hiyo kuna baadhi ya mitaa haipitiki na haifai kukalika kutokana na kusambaa kwa vinyesi baada ya miundombinu kufumuka.

Alisema watoto wako hatarini zaidi kwa kuwa baadhi yao kwa kutokujua athari wamekuwa wakijikuta wanacheza maeneo yaliyo na majitaka yaliyosambaa na kuhatarisha afya zao.

"Kuna maeneo hapa pana bwawa kubwa la maji taka, tunawatafuta wenzetu wa idara ya maji kila siku lakini hawaji kudhibiti uvujaji huo na imekuwa kero kubwa sana kwetu," alisema Simbaya.

Mkazi wa kata hiyo, Zuberi Shaban, alisema kuna dimbwi kubwa la majitaka katika barabara inayotokea eneo la Mabatini kwenda Simike hatua aliyosema inahatarisha afya za watoto hasa wanafunzi ambao wamekuwa wakiitumia njia hiyo kwenda shule ya msingi Mabatini.

Akizungumzia mikakati ya Mbeya –WSSA kwenye kukabiliana na changamoto hiyo kwa niaba ya Mkurugenzi wa mamlaka hiyo, Mhandisi Eline Gerson, alisema mamlaka imetenga bajeti kwa ajili ya kukarabati miundombinu iliyochakaa ili kuwaondolea wananchi adha wanayokabiliana nayo.

# Vifo vya mama, mtoto sasa tishio

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAKWIMU za vifo vya mama na mtoto katika Mkoa wa Mbeya zinaonyesha mwaka 2018 watoto wachanga 500 walifariki wakati wa kuzaliwa, huku kinamama 75 wakipoteza maisha wakati wa kujifungua.

Hayo yalisemwa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, wakati wa mafunzo ya matumizi ya dawa za usingizi wakati wa kufanya upasuaji. Mafunzo hayo yalitolewa kwa wataalamu wa afya wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema chanzo cha vifo hivyo ni kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya dawa za usingizi ambapo alisema takwimu hizo za watoto ni wenye umri wa kuanzia siku sifuri mpaka siku 28.

Alisema mafunzo hayo ya matumizi ya dawa za usingizi yanayotolewa kwa wataalamu yamekuja muda mwafaka kwa maelezo kuwa yatasaidia kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Dk. Manyatta alisema katika Mkoa wa Mbeya kuna hospitali 25 zinazotoa huduma ya usingizi na kwamba kati ya vituo vya afya 16 ni vituo sita vinavyotoa huduma hiyo.

Aliishauri serikali kuwaacha wataalamu waliopata mafunzo hayo kuendelea kufanya kazi hiyo badala ya kubadilishiwa majukumu kama ambavyo imekuwa ikitokea kwa taaluma zingine.

Mratibu wa mafunzo hayo, Dk. Neimar Yusuph ambaye ni mtaalamu wa usingizi kutoka katika Hospitali ya Mkoa wa Tanga, alisema waliamua kutoa mafunzo hayo baada ya kubaini kuwa kuna changamoto kubwa ya matumizi ya dawa za usingizi.

Alisema walipita katika vituo vingi vya afya pamoja na hospitali na wakabaini kuwa kuna tatizo hilo ambalo linasababisha matatizo ya kiafya hasa kwa mama na mtoto wakati wa kujifungua.

Baada ya kutoa mafunzo haya tunakusudia kuanza ufuatiliaji ili tupate mrejesho wa kile tunachofundisha ikiwamo kuwafuatilia hawa wataalamu kuona kama kuna mabadiliko ya takwimu za vifo vya mama na mtoto.

Mtaalamu wa dawa za usingizi kutoka katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Rukwa, Dk. Prosper Massawe, alisema katika mkoa wake vifo vya mama na mtoto vimekuwa vikipungua lakini kutokana na mafunzo hayo anaamini vitapungua zaidi.

Alisema watahakikisha wanawafundisha wataalamu wengine kutoa dawa za usingizi kwa usahihi wakati wa kufanya upasuaji wa aina yoyote ili kuwaepusha wagonjwa na hatari ya kupoteza maisha.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, akisaka wateja wa mmea wa alovera, katika Barabara ya Mtaa wa Mkunguni eneo la Kisutu, jijini humo, jana. Aloevera ni mmea unaotumiwa sana na watu wengi kutokana na faida zake kiafya. **PICHA: JOHN BADI**

# Shughuli za binadamu zaweka shoroba hatarini

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

NJIA za kupita wanyamapori maarufu kama shoroba zinazounganisha hifadhi za taifa na mapori ya akiba na nchini, yako hatarini kutoweka kutokana na wananchi kuvamia kwa kasi na kufanya shughuli za kibinadamu.

Mratibu wa Mradi wa kulinda ushoroba wa eneo la wazi la Rungwa linalounganisha Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, mapori ya akiba ya Rungwa, Kizigo na Muhesi kwa upande wa Mashariki na Hifadhi ya Taifa ya Katavi, mapori ya akiba ya Piti na Lukwati kwa upande wa magharibi, Richard Ndaskoi, alisema kuwa kwa sasa kasi ya uvamizi wa shoroba hizo imeongezeka mara dufu hali ambayo inatishia njia hizo kujifunga kabisa.

Alisema kuwa endapo hatua za haraka hazitachukuliwa kudhibiti hali hiyo kuna hatari ya ikolojia ya hifadhi za taifa kuathirika ikiwamo kupungua kwa ubora wa wanyamapori hasa tembo ambao ni kivutio kikubwa cha watalii.

"Utafiti ambao ulimefanyika unaonyesha kuwa kama hatua za haraka hazitachukuliwa kudhibiti kasi ya uvamizi wa shoroba nchini, huwenda shoroba hizi zikajifunga kabisa ndani ya miaka mitatu ijayo na endapo hili litatokea kutakuwa na athari kubwa kwenye hifadhi zetu hasa kuhusiana na ikolojia ya wanyama," alisema Ndaskoi.

Alisema wanyama wakishindwa kuhama kutoka hifadhi moja kwenda nyingine, kitakachotokea ni kwamba wanyama hao hawataweza kuwa na mwingiliano wa damu wakati wa kuzaliana na matokeo yake wanyama wa aina moja na pori moja watazaliana wao kwa wao hali ambayo itasababisha kupatikana kwa kizazi cha wanyama ambacho hakiwezi kuhimili magonjwa.

Ndaskoi alisema kuwa kwa kuliona hilo ndio sababu wameshirikiana na wadau wa uhifadhi ili kuangana uwezekano wa kulinda shoroba hilo kwa kushirikiana na wananchi wa vijiji vinavyozunguka maeneo hayo.

Alisema kuwa katika mradi huo watashirikisha wananchi ili na wao wanufaike kiuchumi na uwepo wa wanyama jirani na maeneo yao kwa lengo la kuwafanya na wao kuwa walinzi wa shoroba hizo dhidi ya wavamizi.

Aidha, alisema kuwa katika mradi huo wameona pia ni muhimu kuwashirikisha wakuu wa wilaya za Chunya, Sikonge na Manyoni ambazo ndizo zinapitiwa na shoroba hizo kwa vile wao kwa nyadhifa zao pia ni wakuu wa kamati za ulinzi na usalama kwenye maeneo yao hivyo wanaweza kusaidia katika suala zima la ulinzi wa shoroba.

Mkuu wa Kitengo cha Ulinzi wa Wanyamapori katika mapori ya Akiba ya Rungwa, Kizigo na Muhesi, Sylivester Mdoe, alisema kuwa mbali na uvamizi wa shoroba hizo pia kuna changamoto nyingi za kiulinzi zinazotokana na uwepo wa wananchi jirani na hifadhi.

Alisema kuwa mapori ya akiba ya Rungwa, Kizigo na Muhesi yanazungukwa na vijiji 36 ambavyo baadhi ya wananchi wa vijiji hivyo wanaingia hifadhini kufanya ujangili unaoathiri kwa kiwango kikubwa uhai wa hifadhi na wanyama.





# Mkakati waja kuboresha haki jinai

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema inakuja na mkakati wa miaka mitano utakaotekelezwa na wizara na taasisi mbalimbali katika maeneo yanayohitaji mfumo wa maboresho ya haki jinai nchini.

Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Augustine Mahiga, alisema hayo wakati akifungua kikao cha mawaziri, makatibu wakuu wa wizara na wakuu wa taasisi zinazounda jukwaa la haki jinai.

Mkutano huo wa kujadili hitimisho la mchakato wa sekta ndogo ya mfumo wa haki za jinai, majadiliano yalianza Julai, mwaka huu.

Balozi Mahiga alisema mara ya mwisho kupitia mfumo huo na kuufanyia maboresho ni takribani miaka 20 hivyo ni muhimu kupitia ili kuendana na wakati uliopo.

Alisema baada ya mapitio ya mfumo huo yatapitishwa na kujadili maeneo yaliyopendekezwa kuboreshwa ili kufanya mfumo huo kuwa rafiki kwa wadau wote wa haki jinai.

"Katika kipindi cha miezi miwili sasa wataalamu kutoka wizara na taasisi za serikali na asasi za kiraia wamekuwa hapa wakichambua na kujadili masuala mbalimbali katika mfumo wa haki jinai ambayo wamekuwa kikwazo katika kushughulikia na kusimamia masuala ya jinai nchini," alisema Balozi Mahiga.

Alisema mfumo huo unahusisha mnyororo wa hatua mbalimbali zinazotolewa wakati wa kushughulikia uhalifu wa kuanzia katika ngazi ya kuzuia uhalifu usitokee kutambua unapotokea ikiwamo kukamata wanaofanya uhalifu kutekeleza kitendo vya kihalifu kushtaki mahakamani kutoa adhabu kurekebisha tabia za wahalifu na kufuatilia mienendo yao wanapomaliza kutumikia adhabu.

Alifafanua kuwa katika mnyonyoro huo mambo mbalimbali yamewekwa kisheria ya namna ya kushughulika na wahalifu ambayo yanashughulikiwa na vyombo au taasisi mbalimbali za jukwaa la haki jinai hivyo lazima kufanya maboresho.

Naye Katibu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Profesa Sifuni Mchome, alisema kikao hicho ni muhimu kwa sababu kina lenga kufanya majadiliano ya hitimisho la mchakato wa maboresho ya sekta ndogo ya mfumo wa haki jinai.

Alisema ni vema wataalamu waliopo wakatumia nafasi hiyo kujadili maboresho hayo ili yalete tija kwa jamii.

Pia, alisema wanapaswa kutumia nafasi hiyo kutekeleza kile kinachotakiwa ndani ya majadiliano hayo.

Naye Kamishna wa polisi mstaafu Laurean Tibasana, alisema wanaipongeza serikali kutokana na jitihada inazofanya katika maboresho ya sekta ndogo ya sheria ya mfumo wa haki jinai.

# Usalama barabarani yatamba kupunguza ajali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAKWIMU zilizotolewa ndani ya 24 kwa nchi nzima zinaonyesha kuwa ni ajali mbili pekee zimetokea katika mikoa ya Kigoma na Katavi.

Akitoa takwimu hizo Kamanda wa Polisi wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Fortunatus Musilim, alisema kwa majeruhi wa ajali za magari tangu Januari hadi Julai 2018 ilikuwa 2381, wakati Januari hadi Julai, mwaka huu zimetokea ajali 1,741.

Alisema takwimu hizo zinaonyesha kufanikiwa kupunguza ajali 640 ambazo ni sawa na asilimia 27.

Alisema katika kipindi cha Januari hadi Julai, mwaka jana, vimetokea vifo 1,139, wakati Januari hadi Julai 2019 vimetokea vifo 896 na jeshi hilo limefanikiwa kupunguza vifo 243 sawa na asilimia 21.

Kwa upande wa majeruhi, alisema kuanzia Januari hadi Julai, wakati Januari hadi Julai mwaka huu, walikuwa 1,759, wamefanikiwa kupunguza majeruhi 619 sawa na asilimia 26.

Alisema kwa upande wa ajali za pikipiki kuanzia Januari hadi Julai, mwaka jana majeruhi walikuwa 556, huku Januari hadi Julai, mwaka huu imefikia 388 na kufanikiwa kupunguza majeruhi 619 sawa na asilimia 26.

Pia alisema vifo vitokanavyo na pikipiki kuanzia Januari hadi Julai, 2018 ni 233 na Januari hadi Julai, mwaka huu ni 208 na kufanikiwa kupunguza vifo 25 ambavyo ni sawa na asilimia 11.

Majeruhi Januari hadi Julai mwaka jana ni 450 wakati mwaka huu ni 329.

Vile vile, alisema wameanza operesheni ya kukamata madereva ambao hawasimami katika vivuko vya watembea kwa miguu, wakiwamo wanaokwepa kulipa madeni ya faini ndani ya siku saba baada ya kufanya kosa barabarani.

Kamanda Musilim alisema wataendelea kusimamia suala la uwapo wa madereva wawili katika magari yanayokwenda safari za mbali, ikiwamo kuweka askari katika vituo.

Pia alisema wamebaini madereva wa magari makubwa kuchomoa breki za nyuma ambazo zinasababisha gari kuwashinda katika mteremko.



Paroko wa Parokia ya Jimbo Kuu Katoliki la Dodoma, Padri Onesmo Wise (kushoto), akimpaka mafuta mtoto Luna Anold ambaye ni wa Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mara, Agnes Marwa (aliyembeba mtoto), baada ya Ibada ya ubatizo wa mtoto huyo, iliyofanyika kanisa dogo bungeni jijini Dodoma. Wengine ni mume wa mbunge huyo, Anold Nyambelwa (kulia) na (wa pili kushoto) ni Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu, Jenista Mhagama. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Viongozi watumwa kushirikisha wananchi afya

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) anayeshughulikia afya, Dk. Dorothy Gwajima, amewaagiza watumishi wa sekta ya afya ngazi ya msingi kuhakikisha wanashirikisha viongozi wa mitaa, vijiji na kata mipango yote ya afya inayohitaji ushirikishwaji wa wananchi.

Dk. Gwajima aliyasema hayo jana wakati alipokuwa kwenye ziara ya kujionea maendeleo ya utoaji wa huduma za afya kwa jamii pamoja na matayarisho ya vituo hivyo katika kushiriki huduma za afya ya kinga katika Kijiji cha Mkoyo, Kata ya Hombolo, jijini Dodoma.

Aliwataka watumishi hao kuhakikisha wanawashirikisha viongozi wa dini na madhehebu mbalimbali ili somo la afya liweze kuwafikia wananchi wa makundi yote kokote waliko kwa kuwa ushirikiano huo ni muhimu katika kujenga uelewa na kufanyakazi kwa pamoja.

Dk. Gwajima alifafanua kuwa watumishi wa sekta ya afya ngazi ya msingi wanatakiwa kuwasiliana na viongozi wa ngazi zote kuanzia kitongoji, mtaa, kijiji, kata hadi ngazi ya juu katika halmashauri na mkoa kuhusu masuala yote ya afya yanayohitaji ushiriki wa wananchi ili kuwezesha viongozi hao kuibeba vizuri ajenda ya afya na kuwaelewesha wananchi.

Aliwahimiza watumishi wa sekta ya afya ngazi ya msingi kuhakikisha wanagonga milango ya viongozi na kuwapa ajenda za afya zinazohitaji ushiriki wa wananchi kwa kuwa viongozi hao ndiyo wenye dhamana ya kwanza kwa wananchi, hivyo ni fursa kubwa endapo wataendelea kushirikiana nao kwa karibu zaidi.

"Kufanya kazi pamoja na viongozi wa serikali katika ngazi ya kitongoji, mtaa, kijiji, kata na ngazi zingine zote za uongozi wa serikali na jamii kutasaidia kuharakisha uelewa wa wananchi kuhusu ajenda za afya na juhudi za serikali na hatimaye, kuwezesha wananchi wengi zaidi kushiriki shughuli za kijamii zinazolenga kuboresha afya ya jamii kwa ujumla ili, kujenga taifa lenye afya bora kwa gharama nafuu maana kinga ni bora kuliko tiba," alisema Dk. Gwajima.

Alisema viongozi wa ngazi ya kitongoji, mtaa, kijiji, kata na ngazi zingine zote wakielewa vizuri sera, miongozo na mipango mbalimbali ya serikali kuhusu afya ya jamii wataendelea kuwa mabalozi na wasimamizi wazuri wa kufikisha ujumbe kwa jamii kwa haraka na kuwezesha kuhamasisha jamii husika kushiriki katika masuala ya afya yanayohitaji wananchi.

Dk. Gwajima aliwashukuru viongozi mbalimbali wa serikali na jamii ngazi zote kwa ushirikiano wao wakati wote katika kuibeba ajenda ya afya na kufanikisha mambo mengi ikiwamo ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya unaoendelea nchi nzima na masuala yote ya elimu ya afya kwa jamii na kuhamasisha wananchi kupata huduma za afya ya kinga.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Mkoyo katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Henry Kubesi, alisema yeye na uongozi wote wa kijiji hicho wanaishukuru serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Dk. John Magufuli kwa kuhakikisha uongozi wa ngazi ya msingi unatambuliwa, unaheshimiwa na unashirikishwa katika masuala mbalimbali ya kimaendeleo.

Alisema, ngazi ya msingi ndio nguzo muhimu katika jamii kwa kuwa wao ndio wanawafikia wananchi kirahisi zaidi hivyo wanaishukuru serikali kwa kulitambua hilo ili kuweza kuongea lugha moja ya kuleta maendeleo kwa jamii.



# Dk. Shein kufungua mkutano wa UTPC

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, anatarajiwa kufungua mkutano mkuu wa Umoja wa Klabu za waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), unaotarajiwa kufanyika Septemba 7.

Akizungumza na waandishi wa habari, Rais wa UTPC Tanzania, Deograpias Nsokolo, alisema mkutano huo, unatarajiwa kufanyika ukumbi wa Shehe Idrisa Abdul-Wakil, Kikwajuni mjini Unguja.

Alisema mkutano huo ni mara ya kwanza kufanyika Zanzibar na utahudhuriwa na viongozi na wanachama mbalimbali wa klabu hizo utakaojadili mambo mbalimbali ikiwamo vipi wanawake wanaweza kufanya kazi waandishi wa habari wa Tanzania.

Pia alisema ni jambo la kujivunia kwa Rais wa nchi kukubali mwaliko wa klabu hizo na kuonyesha wazi kuwa serikali imekuwa ikithamini mchango unaotolewa na waandishi wa habari.

"Tunashukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa heshima tuliyoipata na kukubaliwa kwa Rais wa Zanzibar Dk. Shein kuwa mgeni rasmi, katika shughuli zetu hazijawahi kuhudhuriwa na kiongozi mkuu wa nchi, hii kwa kweli ni mara yetu ya kwanza hivyo tunampongeza sana Rais wa Zanzibar," alisema.

Aliishukuru serikali kwa kutoa ushirikiano mkubwa kwa waandishi wa habari kwa kuwa wameweza kutoa taarifa bila ya vikwazo jambo linalowapa moyo katika utendaji wao wa kazi.

Nsokolo alisema kazi za waandishi wa habari ni kuelimisha jamii na kuisaidia serikali kuibua matatizo na kuyafanyia kazi kwa wakati mwafaka na kuyatangaza kwa wakati.

Alisema waandishi wa habari, sio maadui wa serikali wala viongozi wake, bali wamekuwa wakifanya kazi kwa mujibu wa maadili yao na kufichua changamoto zinazowakabili wananchi na jamii na serikali ikitekeleza wajibu wake kivitendo.

Ujumbe wa mwaka huo katika mkutano huo, ni uhuru haki na wajibu ni msingi wa maendeleo.

Wakati huo huo, Rais wa UTPC, alisema kuwa UTPC itafanya maadhimisho ya Siku ya Daudi Mwangosi itakayofanyika katika ukumbi wa Studio uliopo Rahaleo mjini Unguja.

Alisema mkutano huo, unatarajiwa kufanyika Septemba 6 na unatarajiwa kufunguliwa na Balozi Mkazi wa Sweden nchini Tanzania ukiwa na lengo la kuadhimisha miaka saba ya kuuawa kwa mwandishi huyo mjini Iringa.

Alisema maadhimisho hayo yatakwenda sambamba na utoaji wa tunzo kwa waandishi wa habari na ujumbe wa mwaka huu ni 'Ulinzi kwa waandishi wa habari ni jukumu letu sote'.

Mapema Mkurugenzi Mtendaji wa UTPC, Aboubakar Karsan, alisema jumla ya kesi 30 zilipokelewa na waliahidi kuyafanyia kazi.




Spika wa Bunge la Kenya, Justin Muturi (kulia), akimkabidhi zawadi aliyekuwa Katibu Msaidizi wa Chama cha Mabunge Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika, Demetrius Mgalami, kwa utumishi uliotukuka na mchango wake wa maendeleo kwa jumuiya hiyo, baada ya kufunga Mkutano wa 50 wa Mabunge ya Jumuiya hiyo, mjini Zanzibar jana. Kushoto ni Katibu wa Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika, Stephen Kagaigai. **PICHA: OFISI YA BUNGE**.

# Viongozi watakiwa kuongoza kwa kufuata sheria

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

UONGOZI wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ umetakiwa kuongoza kwa kufuata sheria, kanuni na Katiba ya nchi ili watekeleze vyema majukumu yao.

Wito huo ulitolewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, wakati alipokutana na uongozi wa ofisi hiyo ulipowasilisha taarifa za utekelezaji wa Mpango Kazi wa mwaka 2018/2019.

Dk. Shein alisema, uteuzi alioufanya kwa viongozi wa ofisi hiyo hakuangalia uzuri wa mtu ukiwamo wa sura bali ni kwa uaminifu wao, uwezo walionao wa kufanya kazi, nidhamu pamoja na taaluma walizonazo.

"Bado nina imani na uongozi huu hivyo nakuhimizeni mtekeleze wajibu wenu kwa kutumia Sheria za Zanzibar, kanuni zilizopo pamoja na Katiba kwani hata mimi natumia nyenzo hizi hizi kutekeleza majukumu yangu," alisema Dk. Shein.

Aliwaeleza viongozi hao kuwa matatizo yote watakayopambana nayo yatatatuliwa kirahisi iwapo watafuata sheria zikiwamo za ardhi na kusisitiza kuwa iwapo watafuata sheria hizo hawatopata ugumu katika kutekeleza majukumu yao.

Kuhusu suala la ugatuzi, Rais Shein alisema, serikali imeamua kuanza na sekta tatu za afya, elimu na kilimo, lakini hata hivyo umeanza vizuri na fedha nyingi zimepelekwa katika halmashauri na aliutaka uongozi huo kuzisimamia vyema kwa kuwa ni fedha za wananchi kwa ajili ya huduma zao.

Alitoa pongezi kwa uongozi wa ofisi hiyo Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kukusanya mapato ya Sh. bilioni 12.032 sawa na asilimia 93.55 ya makadirio ikiwa ni mafanikio makubwa na kuwataka wakiri na kutambua kwamba mwaka huu, fedha walizoingiziwa katika bajeti yao ni za kutosha na kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa kuliko siku za nyuma.

Dk. Shein alisema hatua zitakazochukuliwa kuhakikisha huduma za afya zinaimarika katika hospitali za visiwani ikiwa ni pamoja na kuwapeleka madaktari na wakunga.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Haji Omar Kheir, akisoma muhtasari wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa ofisi hiyo, alisema hali ya usalama katika Wilaya na Shehia imeimarishwa na wananchi wanaendelea kufanya shughuli zao za kujiletea maendeleo kwa amani na utulivu.

Katika kuimarisha taarifa za usajili wa matukio ya kijamii, waziri huyo alisema kuwa ofisi imesimamia uandikishaji wa vitambulisho vipya vya Mzanzibari Mkazi, uliofanyika katika shehia zote 388 za Zanzibar.

Alisema kuwa ofisi hiyo tayari imeshaanza kazi ya kuzisimamia jumuiya zisizo za kiserikali (NGO), kwa kuzisajili zenye sifa ya kusajiliwa.

# Aagiza polisi kuondoa usumbufu kituo kipya Kijangwani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mkoa Mjini Magharibi imeliagiza Jeshi la Polisi kitengo cha Usalama Barabarani katika mkoa huo kusimamia matumizi ya kituo kipya cha daladala Kijangwani ili kuondoa usumbufu wanaoupata abiria tangu kutangazwa kutumika.

Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, alitoa wito huo katika ziara maalum kituo cha daladala Mnazi Mmoja na Kijangwani kwa ajili ya kutoa ufafanuzi kuhusu matumizi ya kituo hicho kipya, kufuatia malalamiko kuhusu kutumika kwa kituo hicho na usumbufu wanaoupata abiria.

Alisema serikali imeshatoa agizo na maelekezo ya kutumika kwa kituo cha Kijangwani, hivyo Jeshi la Polisi lina wajibu wa kusimamia agizo hilo ili kuona lengo la serikali katika kuondoa msongamano katika maeneo ya mji linafanikiwa.

"Serikali imeshatoa agizo la kutumika kwa kituo hiki kipya na maamuzi ya serikali yanapotolewa basi yatekelezwe na si vyema kuona baadhi ya watu wanakaidi na kushindwa kutekeleza maagizo, sasa wenzetu wa polisi watusaidie kuwaongoza madereva utaratibu ulivyo ili kuondoa usumbufu wanaoupata wananchi wetu," alisema Ayoub.

Aliwataka wananchi wa Mkoa Mjini kukitumia kituo kipya cha Kijangwani huku serikali ikiendelea kuzitatua changamoto ndogondogo ikiwamo ujenzi wa vibanda vya kupumzikia abiria pamoja na daladala zote za mkoa huo kutumia kituo hicho.

Hata hivyo, alisema hakutakuwa na mabadiliko ya ulipaji wa nauli za daladala na kuwataka madereva na makondakta kuacha mara moja tabia ya kuzidisha nauli endapo mtu yeyote ataibainika hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

## KUMUENZI NYERERE

# Makumbusho yakarabati nyumba Butiama

**Na Mwandishi Wetu,** BUTIAMA

MAKUMBUSHO ya Taifa imekarabati na kuikabidhi kwa familia, nyumba ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, iliyojengwa miaka 67 iliyopita.

Nyumba hiyo iliyoko katika makazi ya Chifu Wanzagi Nyerere, kitongoji cha Muhunda, nyumbani kwa Baba wa Taifa kijijini Butiama, Mwalimu aliijenga mwaka 1952.

Alijenga nyumba hiyo wakati akijiandaa kuoa kwa sababu katika mila za kabila lake la Kizanaki, kijana hawezi kuoa asipokuwa na mji wake hivyo awe amejenga nyumba yake.

Nyumba hiyo ilikarabatiwa na Makumbusho ya Taifa kwa kushirikiana na Benki Kuu (BoT), iliyotoa fedha za kugharamia ujenzi.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa, Dk. Gwakisa Kamatula, akiongea katika hafla ya makabidhiano alisema ukarabati huo ulikuwa muhimu katika uhifadhi wa historia ya nchi yetu.

Alisema kuwa nyumba hiyo ambayo alitumia Mwalimu tangu mwaka 1967 hadi 1976, kipindi cha miaka 10 ya uongozi wake, ilikuwa imechakaa sana baada ya kukaa muda mrefu bila kutumika.

"Nyumba hiyo ilikuwa imeharibika katika maeneo mbalimbali kuanzia dari, kuta, madirisha na sakafu," alisema Dk. Kamatula

Baada ya kuona tatizo hilo Benki ya Kuu ilikubali kuifanyia ukarabati kwa gharama ya Sh. milioni 50, ambapo ukarabati ulifanyika kuanzia mwaka 2016 takribani miaka mitatu.

Dk. Kamatula alisema kuwa Makumbusho ya Taifa imeamua kuikabidhi nyumba hiyo kwa familia ya Mwalimu kama sehemu ya kuadhimisha miaka 20 ya kumbukizi ya kifo cha Mwalimu Nyerere ambaye alifariki tarehe 14/10/1999.

"Tunatoa shukrani kwa Benki Kuu kwa kazi nzuri ya kugharamia ukarabati wa nyumba hii," alisema Dk. Kamatula.

Alitoa wito kwa wadau wengine wa Makumbusho ya Taifa kujitokeza kufadhili miradi mbalimbali ya kuendeleza urithi wa Tanzania.

Mwakilishi wa Benki Kuu, Florence Kazimoto, ambaye ni Mkurugenzi wa Benki Kuu Kanda ya Ziwa aliishukuru Makumbusho ya Taifa, kwa kutekeleza azma ya ofisi yake ya kukarabati jengo hilo na kwamba BoT imefanya kazi kwa niaba ya Watanzania wote.

"Mwalimu Nyerere alikuwa baba yetu sote kwa hiyo ukarabati huu ni kazi yetu sote," alisema Kazimoto.

Mtoto wa Mwalimu Nyerere, Madaraka Nyerere, alizipongeza juhudi mbalimbali zinazofanywa na wadau mbalimbali za kumuenzi baba yake. "Kuna wakati mwingine naona kuna watu wengine wana uchungu mkubwa na Mwalimu Nyerere kuliko hata familia yake yenyewe," alisema Madaraka Nyerere.

Madaraka Nyerere alisema familiya iko tayari kuunga mkono juhudi za watu mbalimbali, taasisi na mashirika mbalimbali za kuendeleza urithi na urathi wa Mwalimu Nyerere.

"Tunaomba taasisi au mtu binafsi anapotaka kufanyakazi ya sanaa ambayo wanataka watu wote waone watushirikishe ili tuweze kuwasaidia kuwapa taarifa sahihi," alisema Madaraka.

Chifu Japhet Wazangi Nyerere, akizungumza kwenye makabidhiano, aliipongeza Makumbusho ya Taifa kwa juhudi zake za kuendeleza uhifadhi wa asili wa nchi yetu.

Alisema Nyerere alifanyakazi kubwa katika nchi hii na hivyo kuna haja ya kutunza na kuhifadhi historia ya kazi zake ambayo inafanywa vema na Makumbusho ya Taifa.

"Nawapongeza sana mmepewa dhamana ya kutunza uhifadhi huo maana bila ninyi historia hiyo inaweza kupotea," alisema Chief Wanzagi.

Nyumba ya Mwalimu ilikuwa na vyumba viwili vya kulala sebule na 'slabu' za kukalia na siyo makochi na alikuwa ameridhika. Mwalimu alitumia sana mahali pale kwa ajili ya maamuzi mbalimbali ya kiserikali.

"Kama maneno ya Mungu yanavyosema historia ya mwenye haki haiwezi kupotea," alisema Chifu Wanzagi.



Mkuu wa Kitengo cha Dijitali cha Benki ya UBA Tanzania, Asupya Nalingigwa (wa tatu kulia), akikabidhi msaada wa vitabu vya fasihi kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Ugombolwa, Simon Machia, katika hafla iliyofanyika shuleni hapo, eneo la Tabata, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Tasaf yanufaisha 7,000 Singida Vijijini

**Na Elizabeth Zaya,** SINGIDA

TAKRIBANI kaya 7,760 wilayani Singida Vijijini mkoani Singida, zimenufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini unaoendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Kaya hizo zilizonufaika ni za wananchi wanaoishi ndani ya vijiji 40 kati ya 84 vya Singida Vijijini vilivyonusuriwa na umaskini chini ya mpango huo.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida Vijijini, Rashid Mandoa, alipozungumza na baadhi ya watendaji wa Tasaf waliokwenda kufanya tathmini ya mpango huo.

Mandoa alisema tangu kuanza kwa mpango wa kunusuru kaya maskini wilayani humo mwaka 2014 wanavijiji wengi wamejikwamua kwa kuongeza vipato vyao.

"Hiki mnachokifanya ni kutoa mbegu kwa wahitaji ambao jukumu lao ni kuhakikisha mbegu hiyo inaota na kutoa mazao bora na endelevu.

"Kazi kubwa sana inafanywa na Tasaf nawapongeza kwanza mnawekeza kwenye rasilimali watu hasa eneo la afya na elimu hili ni jambo la mfano kwa jamii yenye kiu ya maendeleo.

"Naamini kupitia ruzuku ya afya, watoto wengi hivi sasa wanapelekwa kliniki na idadi ya wanafunzi hasa wa kike pia imeongezeka shuleni maana wanapata ruzuku ya wasichana rika inayowasaidia kununua taulo za kike," alisisitiza Mandoa.

Alisema shuhuda za wanufaika wa mpango huo zinatia hamasa na kuonyesha namna inavyowezekana kwa mtu wa kipato cha chini kabisa kuwezeshwa na kuchangia pato la taifa.

# Usafiri kwa mtandao kutanua wigo miji mikubwa nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI inayokua kwa kasi katika utoaji wa huduma za usafiri kwa njia ya mtandaoni barani Ulaya na Afrika- BOLT, inatarajia kuzindua huduma zake katika miji mikubwa miwili nchini ikiwa ni hatua mojawapo ya kuendelea kupanua huduma za usafiri katika soko lake la ndani ya nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Arusha, Meneja Mkazi wa Bolt Tanzania, Remmy Eseka, alisema huduma hiyo pia itaanza kupatikana wiki ijayo Visiwani Zanzibar.

Alisema uzinduzi huo wa Bolt katika jiji la Arusha na Visiwani Zanzibar unaongeza idadi ya miji ya Kitanzania inayohudumiwa na kampuni hiyo kutoka mikoa mitatu hadi mitano, na kuifanya Bolt kuwa mtoaji huduma mkubwa wa usafiri kwa njia ya mtandao katika ukanda huu wa Afrika.

Alisema kuwa dhamira ya Bolt ni kufanya usafirishaji wa mijini kuwa rahisi zaidi na wa bei nafuu kwa watu wote na hivyo kufikia malengo ya kampuni katika utoaji huduma za usafiri na ajira ikiwa ni moja ya mchango Bolt kwa jamii.

"Baada ya miji ya Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma, imeendelea kukua kwa kasi nchini kote. Sasa tunakusudia kujenga jamii mpya Arusha na Zanzibar kutokana na uaminifu tunaoendelea kuupata kwa Watanzania," alisema Eseka.

"Huduma hiyo ni rahisi kutumia kwani abiria wanatakiwa kupakua programu ya Bolt kutoka kwenye maduka ya programu ya iOS au ya Android na kujaza wasifu wa mtumiaji. Wakati wapo tayari kusafiri, watumiaji hufungua program na kuweka eneo lao walilopo na mahali walipokusudia kufika," alisema.

" Programu itatoa makisio ya gharama kwa safari hiyo. Mara baada ya abiria kuomba safari, programu humwonesha madereva wa karibu ambao wanakubali safari hiyo.

"Mara tu dereva anapokubali safari hiyo, abiria wataweza kuona jina la dereva wao, picha, muundo wa gari na usajili, na kuweza kufuatilia dereva anayewafuata kwa wakati muafaka na wa kweli lakini pia program hiyo hufanya iwe rahisi kuwa na uhakika kuwa wanaingia salama kwenye gari sahihi na dereva sahihi. Abiria pia wanaweza kutoa maelezo ya safari yao kwa kutumia program 'ETA' iliyomo katika kipengele cha ziada kwenye suala la usalama" alisema.

## HABARI KIMATAIFA

## Njaa yainyemelea Somalia

**MOGADISHU, Somalia**

WANAHARAKATI wa haki za binadamu wametoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuchangia ili kuepuka janga lingine nchini Somalia.

Kulingana na Umoja wa Mataifa (UN), ikiwa misaada haitoimarishwa haraka, zaidi ya watu milioni mbili wako katika hatari ya kukumbwa na baa la njaa ifikapo Desemba.

Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula (FAO) kiwango cha tahadhari kiko kwenye alama nyekundu.

Limesema msimu wa mwaka jana mvua haikuwa kubwa na mavuno ya nafaka hayakuwa mazuri tangu mwaka 2011.

Ilieleza kuwa watu wasiopungua milioni mbili wako katika hatari kubwa ya kukumbwa na baa la nja ifikapo Desemba.

Ilieleza kuwa hadi kufikia mwishoni mwa mwaka huu, Wasomalia zaidi ya milioni sita watapata maradhi ya utapiamlo, sawa na karibu nusu ya idadi ya wakazi wa Somalia. Hali hii inatokana na mtikisiko wa tabia nchi.

Rais wa Somalia, Hassan Sheikh Mohamoud, aliitaka jamii ya kimataifa kutuma misaada ya dharura katika maeneo yanayokabiliwa na ukame na baa la njaa nchini humo.

Rais huyo pia aliwataka Wasomali waishio nje ya nchi kuwajali ndugu zao wanaokabiliwa na njaa na kiu kutokana na ukame unaoitafuna nchi hiyo ya Pembe ya Afrika.

Aliongeza kuwa msimu wa masika umepita bila ya kuwapo na mvua zozote nchini humo, hivyo maeneo mengi yanakabiliwa na ukame.

Aliitaka jamii ya kimataifa kuingilia kati na kutuma misaada ya dharura katika maeneo hayo kabla hali haijawa mbaya zaidi.

Mpango wa kibinadamu wa miezi sita, wenye thamani ya dola za Marekani milioni 487, ulizinduliwa Juni. Lakini mpaka sasa michango hiyo haijafikia hata nusu.

**RFI**

# Nigeria kutuma ndege kuokoa raia wake Afrika Kusini

**LAGOS, Nigeria**

RAIA wa Nigeria wanaoishi Afrika Kusini wamepewa ofa ya ndege za bure kurejea nyumbani kukwepa vurugu za kibaguzi zinazoendelea nchini humo.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Nigeria imesema mmliliki wa Shirika la Ndege la Air Peace yupo tayari kuwasafirisha bure wale wote watakaotaka siku ya Ijumaa.

"Wote watakaotaka huduma hiyo wanashauriwa kuwasiliana na ubalozi wa Nigeria jijini Pretoria na ofisi ndogo za ubalozi jijini Johannesburg kwa matayarisho muhimu," taarifa ya wizara ilieleza.

Mashambulizi ya biashara zinazomilikiwa na wageni nchini Afrika Kusini zimepokelewa kwa hasira kali na Wanaigeria ambao wanahisi wanalengwa na kuonewa.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Nigeria, Geoffrey Onyeama, aliwaambia wanahabari siku ya Jumatano kuwa kulingana na taarifa zilizowafikia, hakuna raia wa Nigeria aliyepoteza maisha kwenye ghasia zinazoendelea.

Hata hivyo, alisema kuwa serikali inaangalia uwezekano wa kumrejesha nyumbani balozi wake kutoka Afrika Kusini na kudai fidia kwa biashara zote za raia wa nchi hiyo zilizoshambuliwa. Nigeria imesusia kuhudhuria Mkutano wa Kimataifa wa Uchumi unaofanyika Afrika Kusini kutokana na ghasia zinazoendelea.

Pia Serikali ya Nigeria tayari imeshatoa onyo kwa raia wake waliopo Afrika Kusini wakiwataka kutosafiri ama kuelekea kwenye maeneo ambayo ghasia hizo zimeshamiri mpaka pale hali itakapotengemaa.

Mashambulizi ya kulipa kisasi kwa kampuni ya Afrika Kusini yaliyowekeza Nigeria pia yamefanyika, hali iliyoilazimu kampuni kubwa ya mawasiliano ya simu- MTN - kufunga vituo vyake vya biashara kote nchini Nigeria. Mwanzoni mwa wiki Rais Muhammadu Buhari alisema kuwa anamtuma mwakilishi wake kwenda Afrika Kusini kueleza ghadhabu zao juu ya vurugu zinazoendelea.

Mwanamuziki nchini Nigeria, Tiwa Savage, amejiondoa kwenye tamasha alilokuwa amepanga kushiriki nchini Afrika Kusini baadaye mwezi huu kwa sababu ya ghasia zinazoendelea dhidi ya raia wa kigeni.

Mwanamuziki huyo wa nyota wa mtindo wa Afrobeats alikuwa amepangiwa kufanya shoo katika jukwaa kuu la tamasha la DSTV Delicious Septemba 21 mjini Johannesburg, mji ambao kumeshuhudiwa ghasia kubwa na uporaji wa maduka mengi yanayomilikiwa na raia wa kigeni kutoka mataifa ya Afrika.

Kabla yake, msanii Burna Boy pia kutoka nchini Nigeria ameapa kutokanyaga Afrika Kusini baada ya ghasia dhidi ya raia wa kigeni kuzuka upya nchini humo.

Katika ujumbe kadhaa kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter masanii huyo mwenye miaka 28 alisema hajawahi kuzuru nchi hiyo tangu mwaka 2017 na hataki kurudi tena hadi serikali ya Afrika Kusini itakaposhughulikia suala hilo.

**BBC**




Raia wa Afrika Kusini wakiwa wameshika silaha za kijadi kwa ajili ya kuwashambulia raia wa kigeni wanaoishi nchini humo na kuchukua mali zao. **PICHA: REUTERS**

# Elimu bure yatua Congo, madarasa yafurika

**KINSHASA, Congo**

SERIKALI ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) jana iliidhinisha elimu bure katika shule za msingi za umma kwa lengo la kutekeleza yaliomo katika katiba ya mwaka 2005, ambayo inasisitiza elimu ya bure kwa watoto wa shule za msingi.

Tangu mwaka 1993, wazazi wamekuwa wakilipa ada ya mafunzo kwa walimu, hivi sasa serikali imeamua kuwalipa mishahara.

Lakini baadhi ya walimu mpaka hadi sasa wana shaka kuhusu utekelezaji wa hatua hiyo mpya ya serikali.

Ndani ya darasa moja katika Shule ya Msingi ya Kilimani, iliopo mjini Kinshasa mwalimu anawafundisha watoto lugha ya Kifaransa.

Mmoja wa mzazi katika shule hiyo aitwaye Mijinga alisema: "Nimekuja kumwandikisha mtoto wangu hapa, lakini alikuwa anasoma kwenye shule ya serikali. Kipya ni kwamba sitalipa tena pesa, kwa sababu watoto walikuwa hawasomi tena vizuri, walikuwa wakifukuzwa kila wakati ikiwa sijalipa," alisema na kuongeza:

"Namshukuru Rais Felix Tshisekedi kwa kile anachotenda kwa sisi raia wa Congo."

Mwalimu Nsumbu Coneil anayefundisha katika Shule ya Msingi ya Kilimani kwa muda wa miaka 15, lakini anapokea ada ya dola za Marekani 60 kila mwezi kutoka kwa wazazi. Lakini amejumuishwa katika orodha rasmi ya wafanyakazi wa serikali, mpaka sasa anasema ana shaka na serikali kutekeleza hatua ya kuwalipa mishahara.

Mkurugenzi wa Shule ya Kilimani, Godé Moju alisema kwa sasa watoto wengi wameanza kukaa sakafuni kutokana na ukosefu wa viti na madarasa yamekuwa madogo kuweza kupokea idadi inayoongezeka ya wanafunzi.

Anasema hali hiyo huenda ikachangia watoto kusoma katika mazingira mabovu.

"Licha ya watoto sasa kuwa wengi, walisema tupokee watoto wote, hivi nimeweka kila darasa wawili wawili, watoto wengi sasa wameanza kukaa chini sababu tu wafundishwe," alisema Moju.

Alisema walimu wanatishia kuanza mgomo ikifika Septemba 20 endapo serikali haitawalipa mshahara wa kutosha.

"Amechukuwa (Felix Tshisekedi) hatua hiyo ya kusema wazazi wasilete tena pesa, sisi tumemuunga mkono, hapa kwani nina walimu ambao hawajawahi kupokea pesa kutoka kwa serikali, nadhani ni muhimu kuwalipa walimu, kama walimu hawatalipwa haraka, itakuwa na athari sana," alisema Moju. Alisema gharama ya elimu ya bure kwa watoto wa shule ya msingi ni kama asilimia 40 ya bajeti ya nchi ambayo ni dola za Marekani bilioni sita.

Wachambuzi wa uchumi wana mashaka iwapo hatua hiyo ya serikali itafanikiwa, lakini Rais Tshisekedi ana matumaini mengi.

Serikali mpya iliahidi kufuatilia kwa karibu pia uamuzi huu wa Rais wa kutoa elimu ya bure kwa watoto wa shule za msingi.

Congo inafuata mifano ya mataifa mengine katika eneo la Afrika Mashariki kama Kenya, Tanzania, Uganda, Rwanda na Burundi katika kutoa elimu ya bure katika shule za msingi.

Katika miongo kadhaa ya nyuma, elimu ya bure katika shule ya msingi iliidhinishwa katika baadhi ya mataifa Kusini mwa Jangwa la Sahara kama sehemu ya jitihada za kufufua mfumo wa elimu.

**BBC**

# Kilio usitishaji ghalani chapelekwa Ikulu

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

MWENYEKITI wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini, Dk. Titus Kamani, amekosoa uamuzi wa kusitishwa kwa mfumo wenye maslahi kwa wakulima (Stakabadhi Ghalani) uliobuniwa kwa ajili ya ununuzi wa mazao vijijini.

Dk. Kamani, aliyewahi kuwa Waziri wa Mifugo katika serikali ya awamu ya nne, alidai kuwa chini ya mfumo huo, wakulima nchini walikuwa katika nafasi nzuri kupata faida ya kazi zao.

"Ninavyojua kuhusu hili, tunawarudisha nyuma wakulima wetu, kwa kuwa serikali ya awamu ya tano inasisitiza kuwakwamua watu maskini na maskini wenyewe ndiyo wakulima," alisema.

Alisema Tanzania inaongozwa na sera na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), na kwamba viongozi waliopo madarakani hivi sasa wanatokana na chama hicho.

Dk. Kamani alisema tayari kuna mafanikio makubwa katika suala la matumizi ya mfumo huo kwenye maeneo ambayo vyama vilipewa ruhusa kuutumia, baada ya kutolewa kwa elimu na wananchi walifurahia.

"Sasa badala ya kurudi nyuma, tulipaswa kuchukua kama mfano, kwa maeneo yaliyofanya vizuri, badala ya kuufuta huku baadhi ya vyama vya ushirika vikiwa tayari vimeanza kukusanya mazao kwenye maghala makubwa, wakisubiri minada," alisema.

Aliomba Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, kuingilia kati kama alivyofanya Shinyanga na Mwanza.

"Ninamwomba sana Katibu Mkuu wetu wa CCM, atusaidie kulifikisha jambo hili juu, kwa kuwa maamuzi yaliyochukuliwa hayamsaidii mwananchi," alisema.

Alipotafutwa kwa njia ya simu kuzungumzia suala hilo, Dk. Bashiru, alisema yupo kwenye vikao na kuahidi kulifuatilia.

"Nimelisikia jambo hilo juu juu tu, lakini limeniumiza sana, najaribu kutafuta ushauri kujua tunaelekea wapi, kwa maamuzi kama hayo na kwa kipindi hiki," alisema Dk. Bashiru.

Wakulima wanaopinga kusitishwa kwa mfumo huo, wamedai kupeleka waraka wa malalamiko kuhusu uamuzi huo

kwa Rais Dk. John Magufuli, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Waraka huo wenye kurasa saba, pia umenakiliwa kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Waziri wa Kilimo Japhet Hasunga, Katibu Mkuu wa

CCM Taifa, Dk. Bashiru Ally, Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika

Dk. Kamani na Kaimu Mrajis wa Ushirika nchini, Tito Haule na umesainiwa na Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Wakulima mkoa wa Ruvuma (SONAMCU),



Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya (aliyevaa shati la blue), akiwa amebeba moja kati ya mapipa 42 ya kutengeneza pombe haramu ya moshi 'gongo' aliyoyakamata katika kiwanda kidogo kilichopo Kijiji cha Mtakuja, Kata ya Kia mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Polisi lawamani mtuhumiwa kutoroka kituo cha polisi

**Na Ahmed Makongo, BUNDA**

MKAZI wa Rorya wilayani Bunda, Sophia John, amewatuhumu polisi kwa kitendo cha kumwachia mtuhumiwa anayedaiwa kumpa mimba mwanafunzi, kutoroka chini ya ulinzi wa jeshi hilo.

Mwananchi huyo amelitupia lawama Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Tarime wilayani Rorya mkoani Mara.

Akiongea na mwandishi wa habari hizi mjini Bunda, shangazi wa mwanafunzi huyo, Sophia John, alidai mtoto wao aliyekuwa anasoma kidato cha tatu alipewa ujauzito na mtu huyo na kusababisha afukuzwe shuleni.

Alidai kuwa mwanafunzi huyo Agosti 8, mwaka huu, alitoweka nyumbani na kwenda kwa mwanaume huyo na mzazi wake alipomfuatilia Agosti 18, alimkuta kwa mtuhumiwa huyo na kuwakamata wote wawili na kuwapeleka Kituo cha Polisi Sota, kilichoko katika wilaya hiyo.

Alidai mtu huyo aliwekwa mahabusu huku yeye na binti yake wakirudi nyumbani na kuambiwa waende Agosti 21, lakini waliporudi siku hiyo, polisi waliwaambia kuwa mtuhumiwa huyo alitoroka.

Alidai baada ya kuhoji mtuhumwa atatorokaje akiwa chini ya ulinzi wa polisi, alifokewa na askari hao na kufukuzwa.

"Tulipokwenda kituoni hapo siku hiyo tukaambiwa kwamba eti mtuhumiwa wetu alitoroka tukahoji kwamba atatorokaje akiwa chini ya ulinzi wa polisi na hiyo ilikuwa ni siku ya tatu bila kumpeleka mahakamani," alidai.

Pia alidai yeye ndiye aliyemlea mwanafunzi huyo na ulipofika umri wa kwenda shule alimpeleka kwa bibi yake katika Kijiji cha Sota kwa ajili ya masomo.

Aliiomba serikali kuingilia kati suala hilo ili mtuhumiwa huyo aweze kukamatwa.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Tai, Koroso Wambura, akiongea na mwandishi wa habari hii kwa njia ya simu, alisema kuwa tukio lipo na mwanafunzi huyo (jina linahifadhiwa), walimfukuza shule kutokana na kuwa na mimba baada ya yeye mwenyewe kukiri kwa maandishi kwamba alipewa ujauzito na mtuhumiwa.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Tarime na Rorya, Henry Mwaibambe, alipohojiwa kwa njia ya simu, alisema yuko likizo na alipotafutwa msaidizi wake alisema kuwa hana kumbukumbu na tukio hilo na kuahidi kulifuatilia.

## Mahakama yaruhusu waandishi kuripoti kesi ya ugaidi

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imeruhusu waandishi wa habari kuripoti kesi ya ugaidi inayowakabili viongozi wa Uamsho na Mihadhara ya Kiislamu (Jumiki) na Jumuiya ya Maimamu Zanzibar, Shekhe Farid Hadi Ahmed na wenzake 22 hadi itakapoanza kusikilizwa.

Kadhalika imeushauri upande wa Jamhuri kukamilisha upelelezi kwa muda mfupi na ikiwa watakwama wawachie washtakiwa huru mpaka watakapokamilisha upelelezi huo.

Uamuzi huo, ulitolewa jana na Hakimu Mkazi, Maira Kasonde, baada ya washtakiwa kuwasilisha maombi mawili ikiwamo kumtaka Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), kukamilisha upelelezi ndani ya mwezi mmoja na kuruhusu waandishi kuripoti habari za kesi yao.

Alisema amri iliyotolewa awali na mahakama hiyo kuzuia waandishi kuripoti kesi hiyo haikuwa sahihi.

Alisema kifungu cha 34 (3) cha Sheria ya Kuzuia Ugaidi kinazuia kuripoti wakati wa usikilizwaji ambapo majina ya mashahidi hutajwa.

Hakimu Kasonde alisema hatua iliyopo katika kesi hiyo waandishi wa habari wanaruhusiwa kuripoti kwa sababu haijaanza kusikilizwa.

Katika kesi hiyo namba 29/2014 upande wa mashtaka uliongozwa na Wakili wa Serikali, Faraja Nguka, huku mawakili wa utetezi ni Abubakari Salim, Abdul Fatah, Obeid Hamid na Daim Khalfan.

Mbali na Shekhe Farid, washtakiwa wengine ni Jamal Nooridin Swalehe (38), Nassoro Hamad, Hassan Bakari, Ahtari Humoud, Mohamed Isihaka, Abdallah Hassan, Hussein Mohamed, Juma Sadala, Said Kassim, Hamis Amour, Abubakar Abdallah, Salum Ali, Salum Amour, Alawi Othman, Rashid Ally, Amir Hamis, Kassim Salum na Said Shehe.

Kwa pamoja wanadaiwa kuwa kati ya Januari 2013 na Juni 2014 walipanga njama ya kutenda makosa hayo na kuwezesha kufanyika kwa vitendo vya kigaidi.

Katika kipindi hicho na maeneo tofauti nchini, Shekhe Farid, anadaiwa kuwa aliwaingiza Sadick Absaloum na Farah Omary, nchini ili kushiriki kutenda makosa ya ugaidi.

Pia Sheikh Farid anadaiwa kuwa kwa makusudi na akijua kuwa anatenda kosa alitoa msaada kwa watu hao kutenda vitendo vya kigaidi kinyume cha sheria na anadaiwa kuwa katika kipindi hicho akiwa anajua kuwa Absaloum na Omary wametenda makosa ya kigaidi, aliwahifadhi. Washtakiwa hao hawakuruhusiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kuisikiliza kesi hiyo hadi Mahakama Kuu.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO



**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**au piga simu: 0767 223311**


## KUPOTEA KWA CHETI



**Linus R. Leopord** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2423/0082** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2008 katika Shule ya Sekondari Kyerwa.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chcochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KAR/RB/2013/2011**

215406902

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MKOA MWANZA**

**MAOMBI NAMBA 359/2018**

**PHILIBERT CLAVERY BAKACHUBA.......... MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **ACCESS BANK TANZANIA LTD**
2. **ANTHONY NESTORY MDULA**
3. **BOSTON AUCT. MART.......................WAJIBU MAOMBI**

### KUITWA SHAURINI

**WAJIBU MAOMBI POPOTE PALE MLIPO,** KWA KUWA, mleta maombi ameleta madai yake ya kesi ya madai na yameelezwa baraza la ardhi na nyumba la wilaya Mwanza. Shauri lilipangwa kusikilizwa tarehe 16/09/ 2019 saa tatu kamili mbele ya maheshimiwa **DOROTHY HIVYO BASI,** Mnatakiwa kufika baraza la ardhi na nyumba la wilaya Mwanza ninyi wenyewe au wakili wenu au mtu aliye ruhusiwa kisheria na kutakiwa kuleta majibu yenu kwa maandaishi kuanzia tarehe mliyopata taarifa hii kupitia tangazo hili. **BOSTON AUCTION MART AND GENERAL AGENCY CO.LTD NA ANTHONY N. MDULA** mnatakiwa kufika siku hiyo kwakuwa mjibu maombi wa kwanza anafika na tayari amesha leta majibu katika baraza hili isipo nyinyi wawili.
ANGALIA, Kama hamtahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, mahakama itasikiliza shauri hili bila uwepo wenu na kutoa uamuzi upande mmoja.

**IMETOLEWA NA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MKOA WA MWANZA**
**TAREHE 26/08/2019**
**MHESHIMIWA DOROTHY**

115406102

---

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**MWAJUMA BULEMBO MAKUNGU**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya NISSAN CIVILIAN yenye namba za usajili T 314 ALV Chassis No. MW40012916 Engine No. ED33060271 Yenye rangi NYEUPE NA BLUU.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa Polisi.

Taarifa ya Polisi: GE/TR/RB/4822/2019

215406702

---

IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MOSHI DISTRICT REGISTRY
AT MOSHI
MISC LAND APPLICATION NO.18 OF 2019
EDWARD HELGARD SAM..................APPLICANT
VERSUS
1. PRIDE –TANZANIA –MOSHI BRANCH...............1st RESPONDENT
2. GRM AUCTIONEERS & COURT BROKER ..........2nd RESPONDENT
3. ROBERT KIMARIO..............................3rd RESPONDENT

TO: PRIDE TANZANIA - MOSHI BRANCH,

**NOTICE FOR MENTION,**

**TAKE NOTICE :** That the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at Moshi on 2nd October ,2019 at 09:00 am before Honourable **DR F.A.TWAIB-JUDGE**

**WHEREAS:** Service on you has been Ordered to be published in the Nipashe newspaper.

You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NORE THAT:** in default of your non appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

GIVEN UNDER my hand and seal of the Court this 26th day of August, 2019

115406502

---

## POLICE LOSS REPORT

**TAN/RB/1162/2019**

**DATE 04/09/2019**

**TO WHOM IT MAY CONCERN**

**REF: CERTIFICATE IN LOSS /THEFT FOR INSURANCE**

**I Certify that GEOFF SONS ENTREPRENEURSHIP** (Name of complainant) report to have been Stolen/lost on 30/08/2019 (Date) at Mikanjuni.

That the following item/property has/have been stolen **REG CARD OF M/VEHICLE NO. T751 CGQ LBR. SPJB 53C9029135 ENGINE 12970312**

115407102

---

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**PRIYANKA VINESH PATEL**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T 886 AZY. Aina Yake TOYOTA CHASER. Yenye chassis namba SX903022088 na Engine namba 4S1372157.

Yeyote atakaeiona anaomba atoe taarifa kituo cha polisi,

Taarifa ya Polisi: MOR/MOR/RB/260491/2019.

115406002

---

**YAH: SHAURI NAMBA 49 LA 2019**

**FLORANCE DAMIAN........................... MDAI**

**DHIDI YA**

**SELEMANI HASSAN SELEMANI ............WADAIWA**

**KWA: SELEMANI HASSAN SELEMANI - POPOTE ULIPO**

**FLORANCE DAMIANI**, amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Tanga dhidi yako. Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 25/9/2019 saa tatu kamili asubuhi (3:00). Hivyo basi, unatakiwa kufika katika Baraza hili bila kukosa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Tanga. Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande mmoja.

AMRI hii imetolewa na kutiwa Saini Muhuri/Lakiri wa Baraza hili leo tarehe 2/09/2019.

115407202

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: **MJINI MOROGORO** Usimamizi wa mirathi

Ombi la **SAUM MOHAMED JUMA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **KARIM MOHAMED JUMA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **16/09/2019** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **04/09/2019.**

215405702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**FORM II**

**Katika Mahakama ya Mwanzo: DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi No. 61/2019**

**Ombi la METHEW SYEMBE kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu NISILE MATHEW SYEMBE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 17/09/2019. kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 4/09/2019.

115406302

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MKOA MWANZA**

**MAOMBI NAMBA 514/2018**

**ESMAIL. I. MOHAMED NA MWENZAKE................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **ACCESS BANK TANZANIA LTD**
2. **NKAYA COMPANY LTD.......................WAJIBU MAOMBI**

### KUITWA SHAURINI

**MJIBU MAOMBI POPOTE PALE ULIPO,** KWA KUWA, Waleta maombi wameleta madai yao ya kesi ya madai na yameelezwa baraza la ardhi na nyumba la wilaya Mwanza. Shauri lilipangwa kusikilizwa tarehe 26/09/ 2019 saa tatu kamili mbele ya maheshimiwa **DOROTHY HIVYO BASI,** unatakiwa kufika baraza la ardhi na nyumba la wilaya Mwanza wewe mwenyewe au wakili wako au mtu aliye ruhusiwa kisheria na kutakiwa kuleta majibu yako kwa maandaishi kuanzia tarehe uliyopata taarifa hii kupitia tangazo hili. **NKAYA COMPANY LTD** Unatakiwa kufika siku hiyo kwakuwa mjibu maombi wa kwanza anafika na tayari amesha leta majibu katika baraza hili isipo kuwa wewe.
**ANGALIA,** Kama hautahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, mahakama itasikiliza shauri hili bila uwepo wako na kutoa uamuzi upande mmoja.

**IMETOLEWA NA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MKOA WA MWANZA**
**TAREHE 23/08/2019**
**MHESHIMIWA DOROTHY**

115406202

---

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT AT TANGA**

**CIVIL CASE NO 2 OF 2019**

**ZINGARO GIMEPPE...............PLAINTIFF**

**VERSUS**

**ELIZABETH MUSTAFA KIMARO .......DEFENDANT**

**TO: ELIZABETH MUSTAFA KIMARO**

**NOTICE OF MENTION/ HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case/appear will be Heard by the Resident Magistrate Court, at Tanga on 12th day of Sept 2019 at 8:30 O'clock in the forenoon.

You must produce on the day all the documents upon which you fated to rely in supporting of your case.
**ALSO TAKE NOTICE** that in default of your non appearance on that day the case will be heard and determined in you absence.

GIVEN under my hand and seal of the Court this 26 Day of August, 2019

**RESIDENT MAGISTRATE**
**TANGA**

115407302

---


**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# LOVREN

## NUSURU AONDOKE LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

DEJAN Lovren amebainisha alitaka kuondoka Liverpool kipindi cha majira ya joto, lakini amekubali sababu ya Jurgen Klopp kumbakisha.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 30 amekosa nafasi hapo Liverpool mbele ya mabeki wa kati, Virgil van Dijk, Joel Matip na Joe Gomez.

Bado hajaichezea Liverpool msimu huu na alikuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na AS Roma ya Italia.

Akizungumza na gazeti la nchini Croatia la Sportske Novosti, Lovren amesema: "Ndio, nilifikiria kuondoka. Najua nilijitahidi kwa hali na mali Liverpool, tulishinda taji la ligi ya mabingwa Ulaya na mimi sio aina ya mchezaji ninayefikiria zaidi fedha.

"Najisikia furaha kwa sababu wakati wote nilihisi Liverpool ilikuwa ni mimi. Naheshimu hilo. (Jurgen) Klopp aliniambia "sikiliza rafiki, wewe ni mchezaji wa daraja la juu, hatutakuachia uondoke kwa mkopo. Tunakuhitaji."

"Nilitaka kuondoka, haikutokea, niliambiwa Liverpool inanihitaji mimi na nilikubali hilo.

"Wiki iliyopita nilizungumza tena na Klopp, aliniambia ananielewa, anajua kwamba sina furaha, lakini pia alisema "angalia sasa kila kitu kimekwisha, nakutaka upambane kwa sababu wewe ni muhimu.

"Nipo kwenye umri sahihi, nikiwa na akili timamu na nipo tayari kupambana kuhakikisha napata nafasi."

# MANDZUKIC KUTUA WEST HAM

**LONDON, England**

KLABU ya West Ham inaangalia uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Juventus, Mario Mandzukic na wanaweza kumchukua wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari.

Mandzukic mwenye umri wa miaka 33, alikuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa kule Manchester United kipindi cha majira ya joto wakati kocha Ole Gunnar Solskjaer alipokuwa akisaka mrithi wa Romelu Lukaku aliyetimkia Inter Milan.

Lakini raia huyo wa Croatia alionekana kutofiti katika mfumo wa United ambayo ilikuwa inahitaji zaidi wachezaji vijana ambapo Solskjaer kwa sasa ameamua kuwa na imani nao.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Daily Mirror, Mandzukic anaweza kutua kwenye Ligi Kuu ya Englnd Januari, kwani West Ham wameonesha nia ya wazi ya kutaka kumsajili.




Wagonga nyundo hao wa jiji la London wameachwa wakiwa hawana safu imara ya ushambuliaji huku Marko Arnautovic, Javier Hernandez, Lucas Perez na Andy Carroll waliruhusiwa kuondoka kipindi cha majira ya joto.

Na mambo yanaonekana kuwa mabaya zaidi kwa kikosi hicho cha kocha Manuel Pellegrini kwani tayari amempoteza Michail Antonio ambaye atakuwa nje ya dimba kwa kipindi cha miezi minne baada ya kuumia wiki iliyopita kwenye mchezo wa Carabao Cup dhidi ya Newport County.

Na hilo limewaacha West Ham wakiwa na washambuliaji wawili tu wa kutegemewa ambao ni Sebastien Haller na Albian Ajeti waliowasajili kipindi cha majira ya joto.

Mandzukic msimu huu hataraji kuwa sehemu ya kikosi cha Juventus, kwani tayari kocha Maurizio Sarri hajamhusisha kwenye mechi mbili za ufunguzi wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, na amemwondoa kwenye kikosi cha Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kama West Ham watamsajili bingwa huyo mara nne wa Serie A, basi itakuwa ni kwa mkopo na sio mkataba wa kudumu.

Mchezaji huyo alifunga bao kwenye fainali ya kombe la Dunia mwaka jana jijini Moscow wakati Croatia ikipoteza kwa kufungwa 4-2 na Ufaransa.

## AZPILICUETA AGOMBEWA HISPANIA

**MADRID, Hispania**

MIAMBA wa Ligi Kuu ya Hispania, Athletic Bilbao na Real Sociedad ipo kwenye mbio moja za kumwania beki wa Chelsea, Cesar Azpilicueta, kwa mujibu wa gazeti la The Sun.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 anakabiliwa na ushindani wa namba kwani Reece James anatarajia kurudi dimbani baada ya kufanyiwa operesheni ya kifundo cha mguu.

James mwenye umri wa miaka 19, ambaye bado hajaanza kuichezea Chelsea, anatarajiwa kuwa beki wa kulia chaguo la kwanza kwa kocha Frank Lampard baada ya kuthibitisha ufiti wake.

James anaweza kuwa tayari kwenye mchezo ujao wa Chelsea wa Ligi Kuu dhidi ya Wolves Septemba 14.

Hilo litaongeza presha kwa Azpilicueta, ambaye amekuwa hapo Chelsea kwa miaka saba na ni nahodha wa klabu.

Bilbao na Real Sociedad wana matumaini ya kumshawishi Azpilicueta kurudi katika Jimbo la Basque nchini Hispania ambako ndiko alikozaliwa.





# MARADONA

## AKARIBIA KURUDI KWENYE UKOCHA ARGENTINA

**BUENOS AIRES, Argentina**

GWIJI wa Argentina, Diego Maradona, anakaribia kurudi kwenye nafasi ya ukocha kwa kuinoa klabu ya ligi daraja la kwanza ya Gimnasia Esgrima La Plata, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Maradona alikutana na klabu hiyo Jumatano na "dili hili limefikia asilimia 80", mwanasheria wa Maradonna, Matias Morla ameiambia ESPN FC, na jana Alhamisi alitarajiwa kutangazwa rasmi.

Hata hivyo, Maradona alibainisha Jumanne kwamba angependa kufundisha soka kwenye ardhi ya nyumbani kwake, lakini Jumatano alikanusha kwamba amefikia makubaliano ya kuinoa Gimnasia, au kukutana na kiongozi yoyote wa klabu hiyo.

"Sidhani kama matumaini hayo ni ya kweli," aliandika Maradona kwenye ukurasa wake wa Twitter. "Bado sijakutana na yoyote."

Lakini mwanasheria wake, Morla baadaye Jumatano hiyo aliposti video ikimwonesha Maradona akiwaambia mashabiki wa Gimnasia: "Nataka kuweka wazi, hivi karibuni nimefanyiwa upasuaji. Sijakutana na watu kutoka Gimnasia, na pia sijazungumza na mtu yoyote hivi karibuni."

Mkongwe huyo mwenye umri wa miaka 58 aliifundisha klabu ya Dorados de Sinaloa ya nchini Mexico kwa mwaka mmoja.

Lakini Maradona aliondoka katikati ya Juni na kwenda kufanyiwa operesheni ya goti.

# Guardiola kununua beki wa kati Januari

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola ataangalia uwezekano wa kusajili beki mpya wa kati wakati wa dirisha dogo la Januari baada ya beki Manchester City, Aymeric Laporte kuripotiwa kwamba atakuwa nje ya dimba kwa mwaka huu wote.

Laporte, ambaye aliondolewa uwanjani kwa machela kwenye mchezo wa Jumamosi wa ushindi wa 4-0 dhidi ya Brighton kwenye dimba la Etihad, alifanyiwa operesheni ya goti la kulia jijini Barcelona na anatarajiwa kuwa nje ya uwanja kwa zaidi ya miezi minne.

Kukosekana kwake kunamucha Guardiola akiwa na mabeki wawili tu wa kati, Nicolas Otamendi na John Stones, ambaye alikosa mechi tatu zilizopita kutokana na majeruhi ya nyama za paja.

Na pia inaibua maswali kwanini City walishindwa kufanya maamuzi ya kusajili beki wa kati kipindi cha majira ya joto baada ya kuondoka kwa Vincent Company aliyetua Anderlecht.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England walikuwa wakishindana na Manchester United kumwania Harry Maguire, lakini walijiondoa baada ya kushindwa kufikia bei, kwani wao walikuwa wametangaza ofa ya pauni milioni 65 ambayo ilikataliwa.



Guardiola, ambaye alitumia pauni milioni 122 kwa kuwasajili Rodri na Joao Cancelo, alidai wikendi iliyopita kwamba hakuwa na fedha za kutosha kununua beki wa kwanza baada ya kushuhudia Laporte akiumia baada ya kugongana na Adam Webster wa Brighton.

"Klabu iliniambia kwamba wamefikia mwisho wa matumizi hawaweze kwenda mbele zaidi," alisema Guardiola.

Kiungo mkabaji Fernandinho alichukua nafasi ya Laporte kwenye mchezo huo wa Jumamosi na atakuwa suluhisho la muda mfupi.

# Lloris: Spurs haiwezi kushinda EPL msimu huu

**LONDON, England**

HUGO Lloris amebainisha kwamba, Tottenham haitashinda taji la Ligi Kuu England msimu huu na inatakiwa kuendelea kuimarika na kutoa changamoto kwa timu mbili za juu.

Spurs imeaanza msimu huu kwa sare dhidi ya Manchester City na Arsenal, huku ikifungwa na Newcastle na imepata ushindi dhidi ya Aston Villa na ipo kwenye nafasi ya tisa.


Huku hivi sasa wachezaji wakiwa kwenye majukumu ya timu zao za taifa Spurs watarudi uwanjani dhidi ya Crystal Palace Septemba 14, na Lloris amesisitiza bado kuna nafasi ya kupanda kileleni.

Lloris amesema: "Liverpool na Man City wana uzoefu na kwa uhakika wanashindana.

"Nafikiri kwa sasa, kuna kitu fulani kinakosekana kwetu. Tutaangalia baadaye kwenye msimu kwa sababu mambo yanabadilika haraka kwenye soka.

"Jambo la msingi ni sisi wenyewe kujikuta kwa malengo yetu, kupata pointi na kucheza kwa kiwango kilekile. Na tutaona wapi tutakuwa kwenye msimamo wa ligi Aprili na Machi.

"Huo ni wakati ambao unaweza kushinda au kupoteza nafasi ya Ulaya au mataji. Kwa wakati huu hatutaki kujikita kwenye aina hiyo ya maswali."



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BAYERN YAONGEZA NGUVU KWA SANE

●●●Mabingwa hao wa Bundesliga wajipanga kuwasilisha ofa nono kwa winga huyo wa City...

**MUNICH, Ujerumani**

BAYERN Munich imesema kuwa iko tayari kuanza upya mchakato wa kumsajili winga wa Manchester City, Leroy Sane, katika dirisha dogo la usajili la Januari, licha ya nyota huyo anayeichezea Timu ya Taifa ya Ujerumani kuwa na majeruhi ya mguu ya muda mrefu, gazeti la The Sun limeandika.

Lakini inaelezwa kuwa klabu yake ya Manchester City bado inaendelea kumshawishi winga huyo kusaini mkataba mpya wa kuendelea kubakia katika klabu hiyo inayotumia Uwanja wa Etihad.

Winga huyo alihusishwa na mpango wa kuhamia kwa mabingwa hao wa Ligi ya Bundesliga kwa dau la pauni milioni 135 kabla ya kupatwa na majeruhi ya mguu katika mechi ya Ngao ya Jamii iliyochezwa mwezi uliopita.

Sane ambaye ana umri wa miaka 23 anatarajiwa kurejea uwanjani msimu huu baada ya kufanyiwa upasuaji wenye mafanikio.

Nyota huyo alisafiri kuelekea Austria kwa ajili ya upasuaji huyo uliofanywa na Profesa, Christian Fink, kufuatia mapendekezo yaliyofanywa na madaktari wenzake wa Timu ya Taifa ya Ujerumani.

Sane alipata majeruhi hayo katika dakika za mapema katika mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Liverpool uliochezwa Agosti 4 mwaka huu kwenye Uwanja wa Wembley.

Sane ameacha kucheza licha ya kuwapo kwa tetezi kwamba hatima yake ya kurejea uwanjani msimu huu itakuwa na mashaka.

Baada ya kuwa na wakati mgumu katika msimu uliopita, Bayern Munich imewasilisha tena ofa ya kutaka kumsajili nyota huyo ili aweze kwenda kukisaidia kikosi chao.

Kufuatia uhamisho wa Sane kuingia dosari, Bayern iliamua kumsajili kwa mkopo winga, Ivan Perisic kutoka Inter Milan ya Italia.

Sane alikuwa katika kikosi cha Manchester City kilichomaliza mechi kwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Tottenham Spurs msimu uliopita.

Taarifa zaidi zinasema kuwa Bayern Munich imemwandalia kitita cha mshahara cha pauni 400,000 kwa wiki, na kama atakubali kujiunga na timu yao, atakuwa ndiye mchezaji ghali.

Kocha Pep Guardiola tayari ameelaeza mabosi wa City kuhakikisha wanafanikiwa kumbakisha winga huyo, huku akiwa tayari amemtakia baraka endapo atafanikisha mchakato wake wa kuondoka klabuni hapo.

Kocha huyo alisema: "Ana uhuru wa kuamua. Kama anataka kuondoka na ana makubaliano, hiyo itakuwa vema. "Lakini kama anataka kuondoka, anaweza kwenda. Tutakuwa na huzuni - tunaamini kwamba atabakia."

## KWA UFUPI

**DAU LAMKWAMISHA MOURA**
BARCELONA ilikaribia kumsajili straika wa Tottenham, Lucas Moura (27), katika kipindi cha majira ya joto mwaka huu, lakini ilishindwa kukamilisha mchakato huo kutokana na dau la pauni milioni 45 ambalo klabu yake ilihitaji kulipwa. ***(Mundo Deportivo)***

**MANDZUKIC, CAN SOKONI**
KLABU ya Juventus inatarajia kufanya mchakato wa kumsajili straika Mario Mandzukic (33), na kiungo, Emre Can ambaye ana umri wa miaka 25, katika dirisha la usajili la Januari litakapofunguliwa. ***(Goal)***

**WEST HAM KUJIIMARISHA**
MABOSI wa West Ham wamemweka katika orodha ya wachezaji inaowahitaji, straika wa Timu ya Taifa ya Croatia, Mandzukic katika dirisha la usajili la Januari lilipofunguliwa. ***(Mirror)***

**ATLETICO YAMFUATA ERIKSEN**
ATLETICO Madrid imeweka wazi nia yake ya kutaka kumsajili kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen (27), na wamesema wako tayari kuwasilisha kiasi kikubwa cha ofa ili waweze kumnasa mchezaji huyo katika kipindi cha Januari. ***(AS - Spanish)***

**DE GEA ATAKIWA JUVE**
JUVENTUS imeweka wazi nia yake ya kuwasajili wachezaji watatu wa Manchester United ambao ni pamoja na David de Gea (28), Eric Bailly (25), na Nemanja Matic (31), kabla ya dirisha la usajili la majira ya joto la msimu ujao litakapofunguliwa. ***(Daily Mirror via Gazzetta Dello Sport)***

**LOVREN KUONDOKA LIVERPOOL**
BEKI wa Liverpool, Dejan Lovren (30), amesema kuwa anatarajia kukubali ofa ya kujiunga na timu zote mbili za AC Milan na Roma katika kipindi cha majira ya joto kitakapofika. ***(Sportske Novosti via Liverpool Echo)***

**NEYMAR AANGUSHA KILIO**
MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Neymar (27), amelia baada ya kuelezwa kwamba mchakato wa yeye kurejea kuwa hataweza kurejea katika klabu yake ya zamani ya Barcelona. ***(El Chiringuito radio via Esporte - Portuguese)***

**SUAREZ: NEYMAR ALIPAMBANA**
STRAIKA wa Barcelona, Luis Suarez (32), amesema kuwa Neymar alifanya kila kitu kinachowezekana kukakikisha mchakato wake wa kuondoka Paris St-Germain unafanikiwa. ***(Fox Sports Radio via Barca Blaugranes)***

**HUDSON-ODOI KIMEELEWEKA**
MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi (18), yuko tayari kusaini mkataba mpya ambao utamfanya akae klabuni hapo kwa muda mrefu. ***(Football.london)***

**FERNANDES KUJIFUNGA LISBON**
KIUNGO anayetakiwa na Manchester United, Bruno Fernandes (24), anajiandaa kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia klabu yake ya Sporting Lisbon. ***(Record via Manchester Evening News)***

**VILLA YAMWANIA SISTO**
KLABU ya Aston Villa imewasilisha ofa ya pauni milioni 9 kwa Celta Vigo ili kumnasa mshambuliaji, Pione Sisto ambaye ana umri wa miaka 24 katika kipindi cha majira ya joto. ***(Faro de Vigo - Spain)***

**AZPILICUETA AGOMBEWA**
KLABU za Real Sociedad na Athletic Bilbao zote kutoka Hispania, zimeweka wazi nia ya kumwania beki wa Chelsea, Cesar Azpilicueta (30), kama atakuwa mchezaji huru. ***(Express)***

HABARI MICHEZO

# MTIBWA SUGAR YAJIPANGA KUWAKWAMISHA SIMBA SC

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI hatima ya wachezaji wa Mtibwa Sugar, Juma Luizio na Jafari Kibaya ambao walikwenda kufanya majaribio ya kucheza soka la kulipwa nchini Misri inatarajiwa kujulikana wakati wowote kuanzia leo, kikosi hicho kimeanza kujipanga kuwakabili mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Zuberi Katwila, alisema kuwa taarifa za awali zinasema kuwa wachezaji hao wanaendelea vizuri katika majaribio waliyofanya na sasa wanachosubiri ni majibu ya mwisho kutoka kwa makocha waliokuwa wanasimamia mchakato wao.

"Wiki hii tunatarajia kupokea majibu ya wachezaji wetu kutoka Misri ambapo walikwenda kufanya majaribio, kama watakuwa wamefaulu, watasajiliwa rasmi na kuanza kibarua huko," alisema Katwila.

Kocha huyo aliongeza kuwa kwa mujibu wa wakala wa wachezaji hao, alisema maendeleo yao yanaendelea vizuri na wakifanikiwa kusajiliwa huko, watasaidia kuleta maendeleo kwenye kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars).

"Tutakuwa hatuna hiyana kabisa kama wakifuzu tutawapa uhamisho ili wakatafute maisha mengine kupitia soka," alisema Katwila.

Kocha huyo alisema kikosi chake kinaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kuwakabili mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba katika mchezo utakaochezwa Septemba 17 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa wataingia uwanjani kucheza mechi hiyo kwa tahadhari kwa sababu wanafahamu ubora wa wapinzani wao ambao ni mabingwa watetezi wa ligi hiyo yenye kushirikisha timu 20.

"Tutaingia kwa tahadhari kubwa, pamoja na kujiamini tutakapokutana na Simba, hatutaki kupoteza mchezo huo," Katwila alisema.

Alisema morali ya kila mchezaji katika kikosi chake ipo juu na kuongeza kuwa hana majeruhi hata mmoja.

"Katika mechi ya kwanza nilibaini makosa, alisema katika machache ya kiufundi ambayo nimeshayafanyia kazi, naamini hali hiyo haitajitokeza tena katika mchezo dhidi ya Simba," aliongeza Katwila.

Mtibwa Sugar ilianza vibaya msimu huu kwa kukubali kupokea kichapo cha mabao 3-1 dhidi ya Lipuli FC ya Iringa.




Golikipa wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Juma Kaseja (katikati), akiwa na mashabiki wa timu hiyo baada ya kumalizika mchezo wa kuwania nafasi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia dhidi ya Burundi ambao ulichezwa juzi mjini Bujumbura. Timu hizo zilitoka sare ya goli 1-1. **PICHA:MTANDAO**

# Mbeya City mambo bado

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Mbeya City, Juma Mwambusi, amesema kuwa ili timu yake iweze kuwa katika kiwango bora inahitaji kucheza michezo 10 ya Ligi Kuu Tanzania ambayo itawapa uzoefu wachezaji wake iliyowasajili kwa ajili ya msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwambusi, alisema kuwa kikosi chake kinaundwa na idadi kubwa ya wachezaji "wachanga" na anaamini baada ya kushuka uwanjani katika michezo hiyo, nyota wake watakuwa tayari kupambana na timu yoyote.

"Kwa sasa nahitaji michezo 10 ili kuwa imara, naamini kikosi changu kitakuwa kimeshazoea mazingira ya Ligi Kuu, hasa ukizingatia msimu huu nimesajili wachezaji wachanga," alisema Mwambusi.

Kocha huyo aliongeza kuwa kikosi chake kina wachezaji wageni ambao ndio mara yao ya kwanza kushiriki Ligi Kuu, hivyo amelazimika kuandaa programu maalumu ya mazoezi ili waweze kuendana na kasi ya ligi.

Kuhusu maandalizi ya mchezo dhidi ya Yanga, Katwila alisema kuwa wako katika hatua nzuri na kila mchezaji ameahidi atapambana kuhakikisha wanaondoka na pointi tatu.

"Yanga wakae sawa, hatutakubali kuachia pointi tatu nyumbani, ndio maana naendelea kufanyia marekebisho idara zote," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa tayari ameshayafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi yao iliyopita dhidi ya Tanzania Prisons ambayo ilimalizika kwa suluhu na anatarajia kucheza michezo miwili ya kirafiki kabla ya kukutana na Yanga.

## Salamba apata ulaji Kuwait

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Adam Salamba, amepata mkataba wa kujiunga na klabu ya Al Jahra ya Kuwait, imefahamika.

Salamba ambaye alitua Simba akitokea Lipuli FC ya mkoani Iringa, alikuwa amepelekwa Namungo FC ya Ruangwa Lindi kwa mkopo.

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam zinaeleza kuwa, Simba inatarajia kulipwa kitita cha Sh. milioni 100 kwa ajili ya kumuuza mshambuliaji huyo ambaye anatarajiwa kusaini mkataba wa miaka mitano na klabu hiyo.

Chanzo chetu kinasema kuwa, mshambuliaji huyo pia anatarajiwa kulipwa mshahara wa Sh. milioni 9.5 katika mkataba wake mpya na klabu hiyo.

"Mafanikio huja kutokana na kupambana na kutokata tamaa, Mungu mkubwa," alisema Salamba baada ya kufanikisha mazungumzo ya kujiunga na Al Jahra.

Mshambuliaji huyo hakuwa na namba katika kikosi cha kwanza cha Simba na hivyo kusababisha kutolewa kwa mkopo ili kwenda kuimarisha kiwango chake.

## Azam yajiimarisha kuwakabili Wazimbabwe

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa wawakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Azam FC, umesema kuwa kikosi chao kinaendelea kujiimarisha ili kuhakikisha wanafanya vema katika mchezo wao dhidi ya Triangle FC ya Zimbabwe.

Azam FC inatarajia kukutana na Triangle FC katika mechi ya kwanza utakaochezwa kati ya Septemba 13 na 15 mwaka huu saa 10: 00 jioni kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, aliliambia gazeti hili kuwa maandalizi kuelekea mchezo huo yanakwenda vizuri na wanaamini wachezaji wao wataendelea na kasi waliyoianza kwenye mashindano hayo.

Cheche alisema kuwa nia yao kubwa ni kuona wanasonga mbele kwenye michuano hiyo na kupeperusha vema bendera ya Tanzania kwenye ngazi ya kimataifa.


"Tunatambua kwamba utakuwa mchezo mgumu na kila mchezaji yuko tayari kwa ajili ya kupambana, tunahitaji kupata matokeo mazuri na sasa kilichobakia ni kuona mashabiki wetu wa nyumbani wanatuunga mkono ili tuweze kufikia malengo kabla ya kusafiri kwenda ugenini kumalizia kazi tutakayoianza hapa kwetu," Cheche alisema.

Azam FC ilisonga mbele katika mashindano hayo baada ya kuwaondoa Fasil Kenema wa Ethiopia.

Michezo

Ijumaa Septemba 6, 2019

Nipashe



## Bayern yaongeza nguvu kwa Sane

HABARI UK 30



Mshambuliaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Simon Msuva, akijiandaa kuwatoka wachezaji wa Burundi, Amissi Mohammed na Frederic Nsabiyumva katika mechi ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia iliyochezwa juzi mjini Bujumbura. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# STARS: TUTASONGA MBELE

### Yajipanga kufanya makubwa katika mechi ya marudiano Jumapili, lakini...

**Na Mwandishi Wetu, BUJUMBURA**

WAKATI kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kikirejea nchini jana jioni, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Suleiman Matola, amesema kuwa anaamini watamaliza vema kibarua walichonacho dhidi ya Burundi ambacho walikianza wakiwa ugenini.

Taifa Stars ambayo ililazimisha sare ya bao 1-1 katika mchezo wa kwanza, inatarajia kurudiana na Burundi Jumapili na mshindi wa jumla atatinga hatua ya makundi ya mashindano ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia zinazotarajiwa kuchezwa mwaka 2022 nchini Qatar.

Akizungumza na gazeti hili jana, Matola, alisema kuwa mechi ya juzi ilikuwa ngumu, lakini wachezaji wa timu hiyo walipambana na kucheza kwa nguvu na hatimaye kufanikiwa kusawazisha.

Matola, Kocha mpya wa Polisi Tanzania inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, alisema kuwa wachezaji wa timu hiyo sasa wameanza kucheza soka "linaloeleweka" na waamini baada ya kurejea nyumbani, watajipanga vema ili kuhakikisha wanashinda na kusonga mbele katika mashindano hayo.

"Tunapenda kuwapongeza wachezaji, wameweza kucheza kwa nguvu na maelekezo zaidi, japokuwa kipindi cha pili tulionekana kuchoka, nafikiri ni kutokana na hali ya hewa na uchovu wa safari, tunasema hatutawaangusha, kutokana tunarudi nyumbani, tutajipanga na tutafanya kile kitu ambacho kila Mtanzania anakihitaji, nina imani tutasonga mbele," alisema Matola.

Kocha huyo aliongeza kuwa bado Stars inahitaji kupewa ushirikiano na wadau wote na kwa kufanya hivyo, anaamini wataendelea kupeperusha vema bendera ya Tanzania kwa kutinga hatua ya makundi ya mashindano hayo.

Nahodha wa Stars, Mbwana Samatta, alisema kuwa ilikuwa ni mechi ngumu na yenye ushindani, lakini matokeo ya sare waliyopata, yatawasaidia kujipanga upya kuelekea mchezo wa marudiano.

"Kwanza nina furaha kwa jitihada ambazo zimeonyeshwa na wachezaji wenzangu, tumejitahidi kwa pamoja na kupata matokeo ambayo yatatusaidia kwa ajili ya mchezo ujao, mechi ya kwanza imeisha, tumepata sare, tunaenda nyumbani, tunaamini Watanzania watajitokeza kutushangilia ili kutufanya tusonge katika raundi inayofuata," Samatta alisema.

Naye kipa Juma Kaseja, alisema kuwa mshikamano na umoja unahitajika zaidi ili Taifa Stars iweze kufanya vema katika mashindano mbalimbali inayoshiriki.

"Sare ya 1-1 ni faida kwetu, tushikamane, kila siku mimi ninasema, Tanzania ni ya kwetu, timu ni yetu, mechi ya marudiano itakuwa ngumu zaidi ya leo, tushikamane ili tuweze kutinga hatua ya makundi," Kaseja, ambaye amerejeshwa katika kikosi hicho na Kaimu Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije alisema.

Burundi ndiyo ilikuwa ya kwanza kupata bao katika mchezo huo kupitia kwa Amissi Cedric na Simon Msuva aliisawazishia Stars na kuamsha furaha ya Watanzania wote waliokuwa wanaufuatilia mchezo huo.

## Simba yajipanga kulinda heshima

**Na Shufaa Lyimo**

MAWINDONI! Kikosi cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, kimeanza maandalizi ya kuwakaribisha Mtibwa Sugar katika mechi ya ligi hiyo inayotarajiwa kuchezwa Septemba 17 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, aliliambia gazeti hili kwamba wameanza programu maalumu ambayo itawaimarisha wachezaji wao na kuwa tayari kuendelea na mbio za kutetea taji hilo wanalolishikilia msimu wa pili mfululizo.

Rweyemamu alisema kuwa anaamini mara baada ya nyota wao walioko kwenye timu za Taifa mbalimbali kurejea, watakamilisha baadhi ya mbinu muhimu ambazo zitawafanya kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kushinda kila mchezo watakaocheza.

"Mikakati ya kocha wetu (Patrick Aussems), ni kuhakikisha hatupotezi mchezo hata mmoja katika Ligi Kuu msimu huu na kulinda heshima, lengo letu ni kutetea taji mapema, leo (jana) tunatarajia kupeana programu kamili baada ya kuanza mazoezi upya baada ya mapumziko mafupi," alisema meneja huyo.

Aliongeza kuwa baada ya kutolewa mapema katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, nguvu zao zote zinaitazama Ligi Kuu Bara, hivyo wanahitaji kuona wanawapa furaha mashabiki na wanachama wao.

Baada ya kucheza na Mtibwa Sugar, mabingwa hao watetezi wataendelea kubakia jijini Dar es Salaam kwa kusubiri Lipuli FC, mchezo mwingine wa ligi hiyo utakaochezwa Septemba 22 mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >